**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| MHE. ZUBEIR ALI MAULID | - | SPIKA |
| 1. Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake |
| 2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani |
| 3. Mhe. Shehe Hamad Mattar | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda |
| 5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu |
| 7. Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi |
| 8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |

| | | |
|---|---|---|
| 9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge |
| 10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | - | MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 11. Mhe. Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake |
| 12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali | - | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume | - | MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. Rashid Ali Juma | - | MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani |
| 15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais |
| 16. Mhe. Maudline Cyrus Castico | - | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais |
| 17. Mhe. Salama Aboud Talib | - | MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake |
| 18. Mhe. Juma Ali Khatib | - | MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais |

| | | |
|---|---|---|
| 19. Mhe. Said Soud Said | - | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais |
| 20. Mhe. Khamis Juma Mwalim | - | Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe |
| 21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera |
| 22. Mhe. Shamata Shaame Khamis | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni |
| 23. Mhe. Harusi Said Suleiman | - | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete |
| 24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri | - | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani |
| 25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi |
| 26. Mhe. Chum Kombo Khamis | - | Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake |
| 27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | - | Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake |

| | | |
|---|---|---|
| 28. Mhe. Lulu Msham Abdalla | - | Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake |
| 29. Mhe. Juma Makungu Juma | - | Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini |
| 30. Mhe. Abdalla Ali Kombo | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 32. Mhe. Ali Khamis Bakar | - | Jimbo la Tumbe |
| 33. Mhe. Ali Salum Haji | - | Jimbo la Kwahani |
| 34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) | - | Jimbo la Kijitoupele |
| 35. Mhe. Ame Haji Ali | - | Jimbo la Nungwi |
| 33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | - | Nafasi za Wanawake |
| 37. Mhe. Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Kiwengwa |
| 38. Mhe. Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid | - | Jimbo la Wawi |
| 41. Mhe. Hamida Abdalla Issa | - | Nafasi za Wanawake |
| 42. Mhe. Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Shaurimoyo |
| 43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 44. Mhe. Hidaya Ali Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) | - | Jimbo la Mtoni |
| 46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub | - | Jimbo la Paje |
| 47. Mhe. Khadija Omar Kibano | - | Jimbo la Mtambwe |
| 48. Mhe. Machano Othman Said | - | Jimbo la Mfenesini |
| 49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti | - | Jimbo la Mtopepo |
| 50. Mhe. Makame Said Juma | - | Jimbo la Kojani |
| 51. Mhe. Maryam Thani Juma | - | Jimbo la Gando |
| 52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud | - | Jimbo la Bububu |
| 53. Mhe. Miraji Khamis Mussa | - | Jimbo la Chumbuni |
| 54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha | - | Jimbo la Mtambile |
| 55. Mhe. Mohamed Said Mohamed | - | Jimbo la Mpendae |

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 01 Machi, 2017**

*(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Bahati Khamis Kombo (kny) Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa kamati naomba kuweka hati mezani Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 90**

**Kuimarishwa Michezo ya Asili**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said -** Aliuliza**:-**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi kuendeleza utamaduni wa michezo ya asili ili isipotee au kusahaulika kabisa. Lakini mpaka sasa michezo hiyo kama mchezo wa ngombe na ngoma za asili mbalimbali hazina hamasa za kushindana na kupandisha morali kwa wanamichezo hao.

a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha ushindani wa ngoma na michezo hiyo ili kuithamini, kuilinda na kupelekea michezo hiyo kuendelea kimataifa zaidi.

b) Je, Serikali imejipanga vipi katika kuipandisha hadhi kimataifa michezo hiyo ili isiwe michezo ya jadi tu au kutumika kwenye sherehe za mavuno tu.

c) Ni michezo gani ambayo Serikali imeianzisha na kuitoa kwenye michezo ya jadi au sherehe ya mavuno mpaka kufikia kimataifa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo** - Alijibu**:-**

Mhe. Spika**,** Kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake nambari 90 lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Serikali imeona umuhimu wa kuanzisha ushindani wa ngoma na michezo ili kuithamini, kuilinda na kuiendeleza Kimataifa kwa sasa wizara ipo katika hatua ya kuitambua ilipo kuifufua na kuisajili, ili baadae iweze kuingia katika mashindano ya Kitaifa , Kikanda na Kimataifa.

b) Mhe. Spika**,** Serikali kwa muda mrefu sasa ilikuwa inaiingiza michezo hiyo katika tamasha ili kuitangaza Kitaifa na Kimataifa pamoja na kuzungumza na Balozi za nchi mbali mbali kama vile China, Oman na Iran.

c) Mhe. Spika, Sherehe za mwaka kongwa kwa sasa zipo katika hatua za kimataifa na mchezo wa nage nao pia unasogea sote ni mashahidi. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Mhe. Spika, na namshukuru Mhe. Naibu Spika, kwa majibu yake mazuri. Mhe. Spika, nikiangalia katika utaratibu ni kwamba michezo yote hii ya jadi naweza kusema asilimia 90 yote inatoka Pemba na wakati wa zamani tulikupokuwa mashule tulikuwa mtoto wa darasa la nne umeshamjua kipaji chake.

(a) Je, una ushirikiano gani wewe na Wizara ya Elimu katika kufufua vipaji hivi vya ngoma za asili.

(b) Huoni umuhimu wa kuanzisha tamasha maalum la ngoma za asili katika kisiwa cha Pemba ili kuzitangaza kimataifa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nichukuwe fursa hii niishukuru Wizara ya Elimu kwa hatua ambazo wamezifikia. Hii inaonesha ushirikiano mkubwa baina ya Wizara ya Habari na Wizara ya Elimu, lakini pia tunashirikiana kwa kuwa hizi ngoma zinaanzia mashuleni na hatimae watu wanapokuwa *age* ya utu uzima ndio wanakuja kitaifa kwa kupitia *age* ile.

(a) Kwa hiyo, hii inaonesha kwamba tuna mashirikiano mazuri na Wizara ya Elimu kwa kuwa ngoma zile zimeanzishwa mashuleni.

(b) Mhe. Spika, naomba nipokee ushauri wa Mhe. Suleiman Sarahan Said kwamba sasa hivi tutakuwa tayari wizara kwenda kujenga kambi kule Pemba ya kuona kwamba matamasha haya nayo kule Pemba yanaoenkana na yaingie katika kimataifa.

**Mhe. Rashid Makame Shamsi:** Mhe. Spika, nakumbuka kwamba katika Radio Zanzibar lakini vile vile katika Televisheni yetu kulikuwa na vipindi ambavyo vinatoa burudani zile za ngoma za asili ambazo siku hizi sizisikii.

Je, Mhe. Waziri una utaratibu wa kuvirejesha vipindi vile japo Suleiman Juma Kimea keshakuwa si mfanyakazi wenu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, nakiri kwamba vipindi hivi vilikuwepo katika orodha au taratibu wa vipindi vyetu vya *ZBC* ambavyo vilikuwa vimetengewa siku zake maalum ya kuonekana vipindi hivi. Lakini napenda nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba:

Kama imefikia kipindi ambacho vipindi hivi havioni napenda nimjibu tutachukuwa hatua ya kuvirejesha vipindi hivi na vionekane na wananchi nao pia waone vipindi hivi ambavyo ni vipindi vya utamaduni wao.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy:** Mhe. Spika, kwa kuwa tuna michezo mingi ya kiasili kama ya ngombe na mingine iliyoongelewa pamoja na nage hivi karibuni imeanzishwa niwapongeze kwa kuanzisha nage kwenye Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar.

(a) Ni lini sasa serikali itaweza kujenga kiwanja japo kimoja maalum cha michezo ya ng'ombe wale wanaopigana au wale wanaoshindana na mtu wale ndani ya Zanzibar.

(b) Kwa kuwa Zanzibar ina utamaduni mkubwa na ina michezo mingi ya kiasili kama huu wa nage ulianzishwa mzuri umevutia na mbali mingineyo ya kucheza na ya ngombe. Ni lini sasa ataanzisha Mhe. Waziri ndani ya Zanzibar *festival* maalum ya michezo hii *special* isiingizwe na waimbaji na watu wengine ni vitu ambavyo vya utamaduni tu wa Kizanzibari *festival* maalum itaanzishwa Zanzibar ni lini sasa atafikiria kuanzisha hapa Zanzibar.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, kwa kuwa serikali imeazimia sasa hivi kujenga viwanja vya wilaya kila wilaya

na viwanja hivi vitajumuisha michezo na lengo na madhumuni ni kuonekana michezo inachezwa katika wilaya zote. Kwa hiyo, naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba na hii michezo ya nage pale ikibidi siku za mashindano yake kwa kuwa mashindano yale yamefanyika Amani na kiwanja kile cha Amani kinachezwa *football* wakati mwengine *Volleyball***.**

(a) Naomba nimwambie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba na michezo hii ikibidi yale mashindano yake yataoneshwa katika viwanja vyetu hivi hivi vya wilaya ambavyo vitajengwa.

(b) Mhe. Spika, napenda pia nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba matamasha haya ya *festival* ni mara nyingi yapo na tunaonesha katika srikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar na ni juzi tu matamasha haya yalikuwepo na pia pale tumejionea vikundi vya utamaduni vikishiriki pale lakini sio vya Zanzibar tu hata vikundi kutoka nje ya nchi vimeshiriki katika matamasha haya ya *festival* na mengineYO.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba niwambie Mheshimiwa Mwakilishi wakati yanapokuja matamasha haya basi na sisi Wazanzibari hasa sisi Waheshimiwa basi tuchukuwe familia zetu tuende pale ili kuona zile tamaduni zetu tunavyozithamini. Lakini pia na wageni wanapokuja pale kuona tamaduni zetu kwani nimeshiriki na nimejionea mwenyewe matamasha ambayo sherehe za *festival* ambayo yameoneshwa hivi karibuni tu walikuwepo wageni wengi sana kutoka nje ya nchi, lakini na sisi Wazanzibari niombe sana tushiriki ili tukuze utamaduni wetu. Ahsante Mhe. Spika.

**Nam. 61**

**Ukosefu wa Umeme kwa Vijiji vya Kichwele, Mbaleni na Boma**

**Mhe. Asha Abdalla Mussa -** Aliuliza**:-**

Kumekuwa na tatizo kubwa la umeme katika vijiji vya Kichwele, Mbaleni na Boma toka kuanzishwa kwa vijiji hivyo.

Je, ni lini Serikali itawapelekea umeme wananchi wa vijiji hivyo na wao waweze kunufaika na huduma hiyo kiuchumi na kwa huduma mbali mbali za kijamii.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira** - Alijibu**:-**

Mhe. Spika**,** kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 61 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kuwa huduma ya umeme inawafikia wananchi wake wote popote walipo. Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme imeratibu mpango wa miaka mitano (5) kuanzia 2015/2020 na kuvipatia huduma ya umeme vijiji vyote vya Unguja na Pemba ambavyo havijafikiwa na huduma hiyo.

Hivyo, namuomba Mheshimiwa Mwakilishi awe na subira, na vijiji hivyo vitaingizwa katika utekelezaji wa mpango huo kulingana na uwezo na upatikanaji wa fedha. Ahsante sana.

**Mhe. Asha Abdalla Mussa:** Mhe. Spika, kwa kuwa vijiji hivi viko katika hali hatarishi kimazingira yake.

Je, wizara yako ina mpango gani mbadala wa kuhakikisha kwamba wanapatiwa japo umeme wa *solar* kama kijiji cha Mgonjoni ili waepukane na madhara ambayo watakayoweza kuyapata.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Mhe. Spika, kwanza hakueleza hatarishi ya namna gani lakini napenda nimwambie kwamba tutashirikiana na wizara pamoja na yeye binafsi kwenda kuangalia hali halisi ya vijiji hivyo na kuona namna gani tunaweza tukafanya kwa kukidhi haja.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Mhe. Spika, kwa kuwa majibu ya wizara yalisema kuwa wizara ina mpango wa miaka 5 ya kuvifikia vijiji vyote na kuvitia umeme.

(a) Katika hatua hiyo ya mpango ilioandaliwa na wizara, je, wizara yako mpaka sasa imeshafanya utafiti wa kuvitambua vyote ambavyo havijafikiwa na umeme.

(b) Kama bado hawajafanya utafiti ni lini utafiti huu utaanza ili kukamilisha huo mpango wa kuvitambua hivi vijiji ambavyo havijapatiwa umeme.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Mhe. Spika, ni kwamba tumefanya na tunaendelea kufanya kwa sababu shughuli zetu zilivyo kila mahala. Kwa hivyo, tumefanya na tunaendelea kufanya hivi. Ahsante sana.
.

**Mhe. Shaib Said Ali:** Mhe. Spika, pamoja na ahadi za Mhe. Rais wakati alipokuwa akiinadi ilani ya CCM wakati wa uchaguzi alisema kwamba Kijiji cha Limani katika jimbo langu atakitumia umeme.

Je, ni lini kijiji hicho kitafaidika na nishati hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Mhe. Spika, kwa furaha kabisa naomba niseme si kwa yeye tu Mwakilishi alieuliza swali bali kwa sote kuanzia tarehe sita Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira atakuweko Pemba kusudi kuangalia wapi kulikuwa na ahadi ya Mhe. Rais na kijiji gani kitaanza na ilani hiyo.

Sasa ni wakati muafaka kukutana nae huko na kuona ni lini itafanywa hiyo kazi ya kuanganishwa. Ahsante sana.

**Nam. 77**

**Matumizi ya Eneo la Tibirizi**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said -** Aliuliza**:-**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi katika kuendeleza maendeleo ya wananchi kwa kuwatengea maeneo mazuri ya kupumzika na kuwatembeza watoto na wageni. Katika eneo la Tibizinzi kwa hapo asili palikuwa ndio eneo husika kuutumia ufukwe huo kwa mapumziko lakini maeneo hayo kwa sasa yameachiwa kuoteshwa mikoko na kuna taarifa kuwa maeneo hayo yameshapimwa kwa ajili ya kujengwa.

a) Je, ni kweli maeneo hayo yamepimwa na kutolewa hati na kama ni kweli, wamepimiwa nani.

b) Je, Serikali haioni kuwa maeneo hayo ndio maeneo pekee ya wazi yaliyobakia katika mipango miji kwa kupumzikia wananchi.

c) Je, Serikali ina mipango gani katika eneo hilo kwa utumiaji mzuri wa ardhi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira** - Alijibu**:-**

Mhe. Spika**,** Kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 77 lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo :-

Mhe. Spika, Eneo linalozungumziwa lipo Mkabala na jengo la *ZSSF* Tibirinzi, eneo hilo lilipimwa awali na kugaiwa wananchi kwa ajili ya makaazi. Hata hivyo, kwa vile eneo hilo liko karibu ya Ikulu, paliamuliwa kubadilishwa matumizi kutoka makaazi nakwenda ujenzi wa ofisi za Serikali. Baadhi ya ofisi za Serikali, zilipewa viwanja katika sehemu hiyo ni pamoja na *ZECO, ZIPA* na *BIMA*. Kiwanja kimoja alipewa mtu binafsi.

Hata hivyo, muda mwingi umepita tangu maamuzi hayo yalipofanywa. Hali ya eneo hilo nalo imebadilika sana, kwa kuota mikoko na kuwa ni sehemu muhimu kwa njia na hata kwa maeneo ya wazi. Kutokana na mabadiliko hayo, Wizara imeiona hoja ya Mhe. Mwakilishi Jimbo la Chake. Aidha, kwa vile tayari tuko katika harakati za kutaka kuanzisha mpango wa kutaka kuanzisha mpango wa kutengeneza *Master Plan* ya Mji wa Chake Chake. Hoja ya Mheshimiwa Mwakilishi itazingatiwa ipasavyo katika kazi hii na maamuzi ya busara yatafanywa wakati huo. Na ikionekana kuwa eneo hili ni zuri zaidi kuwa eneo la wazi kwa Mji wa Chake Chake na bila ya kuleta athari yeyote wizara haitasita kuchukuwa maamuzi hayo.

Aidha, kuhusu maeneo ya wazi katika mji wa Chake Chake kwa matumizi ya mapumziko na wananchi, Serikali kupitia Kamisheni ya Ardhi, ilitenga eneo kubwa kwa ajili ya shughuli hiyo ambalo lipo Tibirinzi uwanja wa watoto ambalo kwa sasa limeendelezwa, kwa kujengwa kiwanja cha kisasa cha kufurahisha watoto, kinachomilikiwa na *ZSSF*. Ndani ya Mpango Mpya wa matumizi ya ardhi ya Mji wa Chake Chake, wizara kwa kushirikiana na Manispaa ya Chake Chake imeanza kuchukua hatua ya kuona umuhimu wa kuongeza maeneo ya kupumzikia katika mji wa Chake Chake. Ahsante sana.

**Mhe. Suleiman Sarahani Said:** Nashukuru Mhe. Spika, na mimi lazima nimpongeze au niipongeze wizara, kwa majibu yao mazuri sana ambayo yamenitia moyo. Lakini nimwambie tu Mhe. Waziri kwamba sasa hivi kama ulivyosema Chake Chake ni mji mkuu namba mbili katika Zanzibar, na kwa mtizamo wangu maeneo ya wazi kwa mjini yamepotea zaidi ya lile eneo ambalo limebakia. Lakini niseme kwamba kwa sababu ya kutenga eneo ambalo, tunazungumza Kibirinzi uwanja wa watoto, lile litakuwa ni eneo kama anavyosema ni la *International*, lakini eneo letu ambalo watu wataweza

kujitumikia kama vile Forodhani, sioni katika mji wa Chake Chake zaidi ya pale.

(a) Sasa nilikuwa namuuliza waziri je, utatuahidi kwamba unaweza ukazifuta zile hati ambazo zimetolewa kwa ajili ya manufaa ya watu wa Chake Chake.

(b) Je, katika utaratibu mzima ambao uliniambia kwamba eneo lile ni la karibu na Ikulu, huoni umuhimu kwamba eneo lile lisijengwe ili lisipoteze haiba ya mandhari yake.

**Mhe. Naibu Waziri Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Ahsante Mhe. Spika. Kama nilivyokua nimesema katika jibu mama kwamba kuna mpango wa *master plan*, huo ndio utaonesha kuona kwamba kuna haja ya kujengwa ama la. Lakini ni kweli kwamba pale ni karibu ya Ikulu. Sasa tusubiri na mwisho wa *master* hii kuona ni nini kinafanyika.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza):** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kwa mara nyengine kuuliza swali la nyongeza kwa wizara hii. Katika majibu ya Mhe. Waziri, alisema kwamba wamefanya utaratibu wa kupima eneo hili na kutokuwapa watu binafsi, majibu sahihi kabisa aliyoyatoa. Lakini katika mchanganuo wake wa kupima hivyo viwanja akasema vimepimwa kwa ajili ya matumizi ya serikali, lakini kiwanja kimoja kapewa mtu binafsi, akarudi kule kule alikokukataa mwanzo. Kwa nini huyu mtu mmoja akaingia katika utaratibu wa kupewa kiwanja katika eneo hili ambalo lina ukaribu na maeneo ya Ikulu, kama ambavyo alivyozungumza mapema.

**Mhe. Naibu Waziri Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Ahsante Mhe. Spika. Ni kweli kama nilivyokua nimesema, mwanzoni lile eneo lilipimwa viwanja kwa ajili ya makaazi, baadae matumizi hayo yakabadilishwa na ikaonekana ipewe taasisi za serikali. Kwa bahati mbaya sana miongoni mwa waliopewa kuna mwananchi mmoja kapewa hati. Hatukuwa na haja ya kuficha ndio maana tukaweka wazi, lakini tunafanya namna pia ya kumuondoshea na yeye. Ahsante sana.

**Nam. 88**

**Kuimarisha Usafiri wa Baharini**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said** - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi kuendelea kutoa huduma za usafirishaji wa wananchi wake katika visiwa vya Unguja na Pemba, lakini sekta hii ya usafirishaji bado inaendelea na mfumo ule ule wa kusafirisha watu au wananchi kwa meli ambazo safari ya Unguja na Pemba huchukua siku nzima kutoka asubuhi mpaka jioni. Mpaka sasa sekta hii haijaonesha njia nyingine za haraka na za kisasa zaidi kusafirisha wananchi wake.

(a) Je, Shirika la Meli bado linatumia mfumo wa kutoa huduma na halijiendeshi kibiashara.
(b) Je, badala ya kutumia mfumo wa meli kubwa za kusafirisha wananchi, kuna mpango gani wa kununua boti kubwa za kisasa kwa ajili ya kuwapa unafuu wasafiri wake na kwenda na wakati wa kisasa na haraka zaidi.
(c) Shirika hili linajikita zaidi kusafirisha wananchi wake kwa njia ya bahari, kwanini Serikali haiwekezi kwenye ndege hasa kwa kuzingatia kuwa wakati mwengine bahari huwa imechafuka vibaya sana.

**Mhe. Waziri Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: (Kny: Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji) –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 88 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwanza naomba kupingana na kauli ya Mhe. Mwakilishi kwamba safari za Meli hususan za Serikali baina ya Unguja na Pemba zinachukua siku nzima yaani asubuhi mpaka jioni. Uhalisia ni kwamba meli ya MV. Mapinduzi II inasafiri kwa muda wa masaa yasiyozidi matano katika mwendo wa kawaida (*Economic Speed*) baina ya Unguja na Pemba na katika ratiba yake ya kawaida Meli inaondoka bandarini saa 2.00 asubuhi na saa 7.00 mchana inawasili bandari ya pili, aidha Malindi au Mkoani kutegemea safari husika.

(b) Shirika la Meli linazingatia masuala yote kwa pamoja kwa upande wa huduma, Shirika limezingatia hali ya kipato cha wananchi na baada ya

kubaini wananchi wengi wanaotumia usafiri huo ni wa kipato cha chini imepanga nauli zake kwa kuzingatia hali hiyo. Aidha, kwa upande wa biashara Shirika limejiwekea viwango tafauti katika usafirishaji wa mizigo kulingana na hali ya soko na mara nyingi Shirika linafikia makubaliano na wafanyabiashara mbali mbali kabla ya kutoa huduma inayotakiwa. Shughuli hizi za biashara zinatumika zaidi kwa meli ya MV. Maendeleo yenye uwezo mkubwa wa kuchukua mizigo (Tani 690).

(c) Mhe. Spika, suala la upatikanaji wa boti kubwa na za kisasa zenye mwendo kasi limezungumzwa katika ngazi ya shirika na wizara, hata hivyo utekelezaji wake utazingatia baada ya kukamilisha mpango ulioanza wa ununuzi wa meli ya Mafuta na nyengine meli ndogo ya abiria na mizigo zitakazo chukua nafasi za meli ya MT. Ukombozi na MV. Maendeleo ambazo hivi sasa zimechakaa. Hivyo naomba Mhe. Mwakilishi awe na subra.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Mhe. Spika, nashukuru sana kwa majibu yake mazuri. Lakini nataka niseme kwamba bila ya usafiri basi nchi haiwezi kupata maendeleo. Pemba kwa kweli iko nyuma sana katika hali ya *speed* ya usafiri. Mhe. Waziri amejibu hapa kwamba meli yake ina uwezo wa kwenda kwa masaa labda manne au matano.

Je, meli yake ina uwezo wa kwenda siku hiyo hiyo na kugeuza siku hiyo hiyo, ili safari hizi ziendane na wakati.

**Mhe. Waziri Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: (Kny: Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji):** Mhe. Spika, ukichukua muda wa siku kwa maana ya kutwa ina masaa 12. Unatumia masaa matano kwenda unapata na masaa matano ya kurudi. Lakini utaratibu unaotumika ni upi, utaratibu kwa maana kwamba unakusudia kutoa huduma, hukusudii kusumbua watu ni lazima upange ratiba kwa kuzingatia watu wanaotoka maeneo yote waweze kupata huduma hiyo ya usafiri. Malengo makubwa ya usafiri wa meli hii ya serikali ni kuwasaidia watu wa chini.

Kwa hivyo, hakuna tatizo kama utapanga *route* uondoke asubuhi saa moja, saa tano au saa sita utakuwa uko Pemba, na saa saba utaweza kuondoka na saa kumi na mbili utakuwa Unguja. Kinachozingatiwa ni kuona kwamba yule anayetaka kusafiri aweza kupata muda wa kujiandaa na yeye asisumbuke, kwa kutambua umuhimu huo ndio serikali ikapanga *route* hiyo kwa siku.

**Nam. 92**

**Msimamo wa Serikali Kuhusu Usafiri wa Bodaboda**

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani** - Aliuliza:-

Hivi sasa kumejitokeza vyombo vingi vya usafiri vya magurudumu mawili yaani boda boda kufanya shughuli za biashara ya kuchukua abiria kutoka sehemu moja kwenda nyengine

(a) Je, Serikali imeridhia kufanyika kwa shughuli hii ya kusafirisha abiria kwa vyombo hivyo.

(b) Kama imeridhia, Serikali inafaidika vipi juu ya maswala ya kulipa kodi kama vyombo hivyo vinafanya biashara.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: (Kny: Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 92 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe . Spika, kwa mujibu wa Sheria Nambari 7 ya mwaka 2003 yaani (*Road Transport Act*) kifungu cha 48 (2) vyombo vya maringi mawili vespa na pikipiki, vinaruhusiwa kwa biashara yaani "*Hire and Drive*", yaani kumkodisha mtu aendeshe mwenyewe. Kwa maana hiyo chombo chochote au mtu yeyote ambaye anatumia chombo cha maringi mawili kwa biashara isiokuwa hiyo, atakuwa amefanya kosa la kufanya biashara bila ya kuwa na leseni, na akitiwa hatiani atatozwa faini ya shillingi za Tanzania, zenye thamani sawa na dola 50 za Marekani au kifungo kisichopungua miezi sita au adhabu zote kwa pamoja.

(b) Mhe. Spika, serikali inafaidika na mapato kwa vile vyombo vinavyofanya biashara zilizotajwa katika sheria tu. Hivyo, serikali haifaidiki na kodi zinazotokana na biashara kama za bodaboda, kwa vile biashara hiyo haipo kisheria.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa muktadha au majibu ya haraka haraka ya Mhe. Waziri, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

haijaruhusu utumiaji wa bodaboda kumchukua abiria Zanzibar kwa mujibu wa sheria hii.

(a) Je, serikali inatoa tamko gani kuzuwia au kuendelea kufanya biashara, kwa sababu imekuwa biashara endelevu katika nchi hii.

(b) Mhe. Spika, serikali imejipangaje ili kuona vyombo hivi vinafanya shughuli nzima ya kuchukua abiria. Tunaona upande wa pili vinaongoza katika masuala mbali mbali ya uhalifu kama kupora, kuiba mabenki na sehemu nyengine vinapotumika vyombo vya matairi mawili. Je, serikali ya Zanzibar imejipangaje kuzuwia wimbi hilo.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: (Kny: Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji):** Mhe. Spika, tunachozungumzia hapa ni huduma na suala lililo-*base* lilikuwa linazungumzia sheria husika. Katika majibu mama tumeeleza kwamba sheria inakataza kuwepo na biashara ya hii ya bodaboda. Lakini lazima tukiri kwamba huduma hizi ni sehemu ambayo inasaidia jamii.

Kwa hivyo, busara inaelekeza kwamba ipo haja na ipo hoja ya serikali katika ngazi za Mkoa, pamoja na wizara husika tukae nao tuzungumze, tuweze kuona wao na sisi tunawezaje ku- *bargain* katika kuona kama tunaweza kuwa na haja ya kufanya mabadiliko ya sheria, ili tuweze ku- *accommodate*, kwa kutambua huduma anayoitoa ni muhimu katika kurahisisha masuala ya usafiri kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa hivyo kwa msingi huo tunaona ipo haja ya kukaa na wenzetu hawa, tuweze kuwa *accommodate* kuweza kuwasaidia wananchi wetu kuondokana na kadhia ya usafiri, hasa nyakati za usiku kwa maeneo ambayo yanakuwa tabu kupata *route* za magari.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Mhe. Spika, utaratibu. Nimeuliza maswali mawili, lakini kanijibu swali moja tu. Swali langu la pili niliuliza, je serikali imejipangaje kuzuwia hili suala la usafiri wa bodaboda, kwa sababu tume-*copy* upande wa pili, tumeona uhalifu mwingi sana unasababishwa na bodaboda. Kama kupora simu, kuiba mabenki na ujambazi, lakini sijapata jibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: (Kny: Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Spika, nilitegemea nasaha zako zingekuwa zinatuongoza sana Barazani,

kwa sababu wakati nilipokuwa namjibu hakunisikiliza. Nilisema najibu maswali yote mawili kwa pamoja, ndicho nilichokisema. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nilisema kwa maudhui kwamba kimsingi wa sheria, sheria inakataza. Lakini umuhimu wa kukaa nao, sisi kama kuna haja ya kurekebisha sheria umuhimu huo upo kwa kutambua uzito wa huduma wanayoitoa. Kama suala la kwamba kunatokea uhalifu, hili ni jambo la kawaida kwa maana kwamba kitu chochote kina *pros and cons.* Kama kuna masuala ya uhalifu maana yake ni jukumu letu serikali ku-*provide* ulinzi kwa maeneo ambayo wanatoa huduma, lakini hatuwezi kukatisha huduma kwa sababu tu kwamba kuna mtu kaporwa simu. Kikawaida kwenye gari watu wanaporwa simu, kwenye meli wanaporwa simu unapoteza.

Kwa hivyo, mimi ni imani yangu kwamba serikali tutakaa ili tuone umuhimu wa kulisaidia eneo hili, kuwasaidia vijana kupata ajira, kuwasaidia wananchi wetu kupata huduma za usafiri, lakini pia kama kuna tatizo la kiusalama ni jukumu letu serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote tunalinda ili wananchi wetu wapate huduma nzuri na kuwapunguzia kadhia katika maisha yao.

**Nam. 27**

**Uhaba wa Vyombo vya Usafiri Katika Benki ya Damu**

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani** - Aliuliza:-

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na kitengo cha damu salama katika shughuli za kukusanya damu kwa ajili ya wananchi wetu ili kuweza kunusuru maisha kwa jamii ya Wazanzibari kumekuwa na changamoto nyingi wanazozipata kwa muda mrefu. Baada ya gari lao kupata ajali na imekaa kipindi kirefu halijashughulikiwa.

(a) Je, ni lini Wizara yako itaanza kutengeneza gari hili ambalo hapo mwanzo lilikuwa linahitaji milioni ishirini za matengenezo.

(b) Wizara imejipanga vipi katika kuwatatulia tatizo hilo kwa wafanyakazi wa Benki ya Damu na kuondoa upungufu wa damu kwa kukosekana kwa gari hili ambalo ni muhimu kwa shughuli zao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya** - Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 27 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nitoe shukrani na pongezi za dhati kwa Mhe. Abdalla Maulid Diwani, kwa umakini wake na ufuatiliaji wake alionao katika kitengo hiki. Mhe. Spika, wizara imemtathmini na kuona juhudi zake, na imemuelewa kwamba analengo la kuwasaidia na kuhakikisha hawapati shida wakati wanapohitaji damu.

Mhe. Spika, wizara inafahamu umuhimu wa kuwepo usafiri kwa shughuli za ukusanyaji wa damu kwa ajili ya wananchi wetu. Hivyo, taratibu za matengenezo ya gari hilo zimeanza kwa kukamilisha taratibu zote za manunuzi. Wizara iko kwenye mchakato wa kukamilisha mipango ya bajeti ya Tsh 23,000,000/= kwa ajili ya matengenezo haya. Kwa kupitia bajeti ijayo ya mwaka 2017/2018, na wakati huo huo kuna mazungumzo yanaendelea baina ya ubalozi wa China kwa kupitia Serikali ya China, ambao ndio waliotufadhili gari hilo. Naomba itambulike kwamba kukosekana kwa gari hilo, sio kukosa kukusanya damu na kutoa huduma hiyo, lipo gari ambalo wizara inashirikiana nao katika ukusanyaji wa damu.

Mhe. Spika, kupitia Mpango wa Damu Salama wizara inafanya uhamasishaji wa uchangiaji wa damu kwa wananchi katika kila shehia kupitia Maafisa wa Afya wa Zoni. Maafisa hawa wamehamasishwa ili waweze kushirikiana na Mabwana Afya, kwa lengo la kushajihisha jamii katika kuchangia damu.

Mhe. Spika, tunatarajia siku ya Jumapili ya tarehe 5 Machi, 2017 mnamo saa 3:00 asubuhi tutakuwa kuna mkutano maalum kati ya Wizara ya Afya na viongozi wote wa Tawala za Mikoa, Serikali za Mikoa na vikosi kwa nia hiyo hiyo ya kufikisha uhamasishaji huo, hadi kufikia ngazi ya shehia kwa Unguja na Pemba, baada ya hapo tunatarajia kufanya vikao maalum kwenu Waheshimiwa Wawakilishi na Waheshimiwa Wabunge wa Jamuhuri ya Muungano, ili kuwashirikisha katika kampeni hiyo, hii ni kwa uhamasishaji na uchangiaji damu Zanzibar, itakayoitwa 'Changia Damu Uokowe Maisha'. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri na kuzunguka kwingi. Je, katika tathmini, sasa hivi ni zaidi ya miaka miwili gari lile limekuwa bovu, na ilikuwa tathmini ya milioni 23,000,000/- ni zaidi ya miaka miwili, kama tulivyosema kwamba gharama hazipungui bali zinazidi.

(a) Je, wizara yako iko tayari kushirikiana na mimi ninaye mfadhili ambaye ataweza kutengeneza gari lile chini ya milioni 23,000,000/-.

(b) Pamoja na uchangiaji wa damu ulivyokua, lakini vilijitokeza viambatanisho vya damu muda mrefu, hadi kupelekea baadhi ya wagonjwa wetu kupoteza maisha katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Je, tatizo hilo kwa upande huo sasa hivi limemalizika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante Mhe. Spika. Kwa heshima kubwa Mhe. Mjumbe tunakuambia kwamba wizara iko tayari kushirikiana na wewe, na ni kwa sababu na wewe umeanza kuonesha mashirikiano kwetu mapema. Kwa hivyo, tuko tayari tupange ni lini, ni wapi na ni wakati gani, ili tuanze kulishughulikia hili kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, kuhusu viambatisho ambavyo vimekuwa ni shida kidogo kupatikana au kuwepo katika hospitali zetu. Mhe. Spika, kwa sasa mapungufu makubwa ambayo tulikuwa tunakabiliana nayo yamepungua, yakiwemo viambatisho hivi. Kwa hivyo, hata kama yapo siwezi kukuambia havipo kwamba asilimia mia moja tuko *clear*. Lakini hata kama vipo, basi ni kasoro chache sana na wizara inaendelea kufuatilia ili kuhakikisha kadhia hiyo inamalizika. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Mohammed Saidi Mohammed:** Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri yenye kutia moyo na ya kupendeza, naomba kuuliza swali moja dogo sana ya nyongeza. Kwa kuwa banki ya damu tumekosa *reagent* nyingi za kufanyia, kama *syphilis, hepatitis* pamoja na HIV na tunaweza kuwapa watu vipimo wende nje. Je, ni sababu gani zinazosababisha vitu hivi kukosekana kwa mara moja na kupewa fomu za ku-*risk* watu wetu ili watie saini na kupata damu ile bila ya kuwa *screened*.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Naomba nishukuru na nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Mhe. Mjumbe kauliza kuhusiana na baadhi ya mapungufu ambayo hutokezea kwa baadhi ya wakati.

Mhe. Spika, kweli mapungufu haya yalitokezea kwa kipindi kama cha mwezi mmoja, lakini baada ya hapo Wizara ya Afya ilikwenda mbio kuhangaika. Mapungufu haya yaligawika sehemu mbili.
La kwanza wale *supplies* wetu ambao wanatupa vile vifaa walikuwa na wao hawana *stock*, kwa hivyo pale kidogo ilikuwa ndio kipindi kigumu kwetu sisi.

Lakini la pili, kulikuwa kuna ufadhili ambao uliondoshwa kwa ghafla na wenzetu Marekani *Center for Disease Control (CDC*), ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilichukua jukumu hilo moja kwa moja chini ya Wizara

ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na kupata muongozo mkuu wa Serikali na kuweza kununua vifaa hivyo.

Kwa hivyo naomba niseme sasa hivi katokeza mfadhili mwengine nae kusaidia ambaye anaitwa *Global Fund* mfuko wa kimataifa wa ulimwengu kwa hivyo viambatanishi vyote hivi tayari sasa hivi vimeshafika vya *syphilis* vya HIV na damu ni salama kama tunavyotamka kwamba damu yetu ni salama. Kwa hivyo naomba Waheshimiwa wengine wote wawakilishi watuvumilie kwa kipindi kile ambacho kina shida lakini sasa hivi kutakuwa hakuna shida na *stock* ya kutosha na Mungu akitujaalia tutaendelea kuagiza kila pale vifaa vinavyopungua ili tusipate matatizo kwa wananchi wetu kupewa damu salama.

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla**: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa ya kuzunguza suala moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza suala dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri kutokana na kuharibika kwa gari lile idadi ya chupa katika benki ya damu zimepungua na kutokana na utafiti ambao kuwa nimefanya Je, Mhe. Waziri unaweza kunipatia idadi ya chupa ambazo kuwa zipo hivi sasa katika sehemu ile ya damu, kutokana na kupungua hatuoni kuwa tunahatarisha maisha ya wananchi wetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Kwanza kuharibika kwa gari lile hakujaathiri sana upokeaji au upataji wa damu salama kutoka kwa wananchi, lakini kinachochangia zaidi kupungua kwa damu yetu sio gari lile hata kidogo, kwa sababu gari zipo na zinafanya kazi na wafanyakazi wanatoka kwa shifti kwenda kukusanya damu ni uhamasishaji. Tunaomba sana uhamasishaji wenu kwa wananchi ambao wamewapigia kura uwe mkubwa ili waweze kujitokeza katika masoko gari zetu zinatembea maskuli zinatembea katika taasisi mbali mbali ili kuhakikisha tunapata wananchi ambao wanataka wao wenyewe kuchangia damu kwa ajili ya wananchi wenzao.

Mhe. Spika, damu salama kwa kweli siwezi kukupa idadi ya chupa kwa sababu kwanza huwa hatuhifadhi kwenye chupa kama ulivyosema Mhe. Viwe Khamis Abdalla, tunahifadhi katika vyombo au sehemu maalum zikiwemo mipira ile ambayo mnaikuta inatundikiwa mgonjwa pamoja na sehemu nyengine maalum ambazo zinawekwa katika vifaa vya baridi, halafu kwa ajili ya ubaridi wenye *temperature* maalum kwa ajili ya matumizi. Kwa hivyo kile kiasi cha chupa ngapi siwezi kukwambia ni chupa ngapi kwa sababu hatuhifadhi katika chupa.

**Nam. 28**

**Taratibu za Kukabiliana na Maradhi Yasiyoambukizika**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said** - Aliuliza:

Serikali ina wajibu wa kuchunguza maradhi mbali mbali yanayojitokeza, lakini kwa sasa inaonekana imejikita zaidi katika maradhi ya *UKIMWI*, maradhi ya kipindupindu na malaria na kuacha kuchunguza maradhi mengine kama kisukari, moyo, *pressure*, uti wa mgongo, mafigo ambayo kwa sasa hapa Zanzibar inaonekana yamechukua nafasi kubwa na kusababisha vifo vya watu wengi.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuchunguza na kudhibiti maradhi hayo yasiyoambukiza.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kupata mashine au vifaa vinavyoweza kusaidia kutibu au kuondosha kabisa matatizo hayo.

(c) Na Serikali imejipanga vipi kuwa na wataalamu au madaktari bingwa wa maradhi hayo yanayosumbua watu kwa kiasi kikubwa.

**Mhe. Waziri wa Afya** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 28 lenye vifungu (a) (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nikiri kuwa Wizara ya Afya inatambua ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza linalotukabili, na naomba ifahamike kuwa ongezeko hilo si kwa Zanzibar tu bali ni duniani kote.

(a) Mhe. Spika, naomba nieleze hatua ambazo Wizara ya Afya imezichukua katika kipindi cha miaka minne iliyopita. Kwanza, tumeweza kuongeza idadi ya kliniki zinazotoa huduma za matibabu na uchunguzi wa magonjwa hayo kutoka 8 kwa mwaka 2012 hadi kufikia 49 mwaka 2016. Hii imelenga kusogeza huduma hizo karibu na wananchi. Pili, Wizara imenunua aina tisa (9) tofauti ya vifaa vya uchunguzi wa magonjwa hayo na kuvisambaza katika kliniki hizo.

Mhe. Spika, wafanyakazi wapatao 200 kutoka vituo vipya na vya zamani wamepatiwa mafunzo juu ya kugundua na kutibu magonjwa

hayo. Kwa sasa Wizara imejikita zaidi katika kuelimisha jamii juu ya kujikinga na magonjwa hayo pamoja na kujenga utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara.

(b) Mhe. Spika, naomba niweke bayana kuwa hakuna sababu za moja kwa moja zinazosababisha magonjwa yasiyoambukiza. Kupata magonjwa haya kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na vichochezi vikuu vinne ambayo sote tunaweza kuviepuka. (i) Kutofanya mazoezi, (ii) Kutozingatia mlo kamili "balanced diet" (iii) matumizi ya aina zote za tumbaku na (iv) matumizi ya pombe.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya ilifanya utafiti mwaka 2011 na kubaini kuwa wasiofanya mazoezi miongoni mwa wazanzibari ni asilimia 18 kati ya waliohojiwa; matumizi ya matunda na mboga mboga za asili ni asilimia 2; matumizi ya tumbaku ni asilimia 7.3 na matumizi ya pombe ni asilimia 1.7. kwa matokeo hayo, pamoja na kuwa Wizara ina wajibu mkubwa wa kuelimisha jamii, lakini jukumu kubwa zaidi la kujikinga litabakia kwa jamii ambayo inahitaji kubadilisha mfumo wa maisha ili kuepukana na magonjwa hayo.

(c) Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba ifahamike kwamba hakuna mashine wala kifaa chochote kinachoweza kukinga au kuondoa magonjwa haya; kitu pekee kitakachosaidia katika kupunguza kasi ya magonjwa haya ni juhudi zetu binafsi za kupambana na vile vichochezi vinne nilivyovitaja awali ambavyo kwa kiasi kikubwa vinapelekea kupata magonjwa haya.

Mhe. Spika, kwa upande wa vifaa vya uchunguzi ni kama nilivyotangulia kusema kwamba vifaa kadhaa vimenunuliwa na kusambazwa katika vituo vya afya. Pia wafanyakazi walikumbushwa juu ya matumizi ya vifaa hivi wakati wa mafunzo ya msasa yaliyofanyika Septemba mwaka 2016.

Mhe. Spika, Wizara imekuwa ikifuatilia kwa karibu suala la upatikanaji wa madaktari bingwa katika fani mbali mbali na hivi sasa tayari kuna madaktari kadhaa ambao wapo masomoni na wengine wapo tayari kwa kuajiriwa.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, baada ya majibu mazuri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye vifungu a na b.

Lakini Mheshimiwa amesema kwamba Wizara na ndio ilivyo ina jukumu la kuwalinda wananchi wake kiafya, Mhe. Spika, tabia haina dawa na haya ndio maisha yetu ya kila siku ambayo tunayatumia kwa hivyo haya lazima tunakwenda nayo, lakini sasa hivi asilimia 90% wagonjwa wote wanahama hapa na kwenda Dar es Salaam na wengine kufa huko huko kutokana na uhabara matibabu au madaktari bingwa.

a) Namuuliza Mhe. Waziri, Je, amejipangaje kupunguza wimbi la wananchi wake kwenda kutafuta matibabu kati ya Dar es Salaam na India.

b) Lakini la pili kwa kuwa hili janga limeshatufika haoni umuhimu wa kutafuta kikosi kazi cha Madaktari bingwa ili kutoa taaluma au kuangalia wagonjwa katika zahanati zote za Unguja na Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa suala lake la (a) lakini la (b) nitamuomba arudie kidogo.

a) Mhe. Spika, ndio maana Wizara na Serikali ikaonyesha juhudi kubwa na tunaomba msaada wenu wa kutaka kuifikisha hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kufikia kuwa Hospitali ya Rufaa, lengo na madhumuni ni kuwapunguzia mzigo mkubwa wananchi wetu na wagonjwa ambao tunawasafirisha kuwapeleka Muhimbili, kuwapeleka India, kuwapeleka Israel na sehemu nyengine yoyote nje ya Tanzania. Hospitali yetu itakapokuwa ya rufaa Mheshimiwa tatizo la wananchi wetu wagonjwa la kusafiri kwenda kutafuta matibabu nje ya Zanzibar litapungua au litaisha kabisa.

**Mhe. Spika:** Naomba umuulize tena hilo swali la pili.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Ahsante Mhe. Spika, nilikuwa namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba kwa kuwa hili limeshakuwa janga maana yake tunaliita janga kutokana na matatizo yanayotukabili, lakini lazima tukabiliane na janga kama mhimili mkuu wa wananchi Wizara ya Afya. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta kikosi kazi ambacho kitakuwa namadaktari binga kutembelea nchi nzima katika zahanati ili kutambua au kuwasaidia wananchi wake katika hali zote ambazo madaktari wale wanaweza wakaziona.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, nitajibu kwa jinsi nilivyolifahamu, kikosi kazi cha kwanza kitatoka ndani ya Wizara yetu kwa ajili ya kutembelea

sehemu zote kufanya utafiti na kuchunguza kasoro na matatizo wanayokabiliana nayo wananchi wetu. Sio rahisi kikosi kazi hicho kukitoa nje ya nchi halafu kikatembea katika nchi, kikosi kazi ambacho kitatoka nnje ya nchi kwa misaada yao wenyewe basi kile kitaingia katika hospitali zetu kuu na kutoa huduma kama ambavyo wanafanya sasa hivi.

Lakini tunakuhakikishia hili kwanza tunalichukua kama ni shauri kwa sababu hatunalo, kwa kweli ni jambo zuri tutawapanga madaktari wetu, tutawapanga baadhi ya manesi wetu ili kutembea katika Hospitali zetu zote na ikiwezekana kwa wananchi na ikiwezekana ikiwa ni rahisi zaidi basi kuingia hata kwa baadhi ya taasisi ili kuona wananchi wetu na wafanyakazi wetu na kutizama afya zao na kupata kujua linalokabili na kupata matibabu.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuongezee kidogo Mhe. Suleiman Sarahan na kuweka sawa kidogo baadhi ya takwimu, chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindui hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kuokoa takriban dola milioni tano sawa sawa na bilioni kumi kwa upereshen wa uti wa mgongo, ubongo pamoja na vichwa maji ambavyo hapo awali tulikuwa tunapeleka huko Dar es Salaam.

Lakini naomba nimfahamishe pia Mhe. Suleiman Sarahan ile asilimia 90% aliyotoa kwamba ndio wanaokwenda Dar es Salaam na kwengineko katika wagonjwa wetu wote tunaopokea hapa Zanzibar Wizara ya Afya ni asilimia 2.8 tu ndio wanakwenda kupata matibabu nje ya Zanzibar. Wengine wote asilimia 97.2% wanapatiwa matibabu yote hapa Zanzibar.

Lakini kwa swali lake (b) naomba niengozee majibu kumtolea takwimu chache tu za mwezi huu ambapo madaktari wetu bingwa wakishirikiana na kambi mbali za madaktari bingwa wa ulimwengu wameweza kuweka kambi zao hapa Zanzibar, kwanza kabisa ni *NED*, yaani *Neurosurgery Education Development* ya kutoka Spain wameweka kambi juzi na jana madaktari wa Spain wamesafiri tumewasindikiza wamefanya upereshen takriban 58 kisiwani Pemba za kinamama ambao wameathirika na maradhi mbali mbali na zote zimekuwa *very successful operation* wakishirikiana na madaktari wetu.

Lakini mbali ya hayo kutokana na maradhi yasiyoambukiza kuna kambi za macho zimefanyika katika wiki hizi mbili kumefanyika kambi mbili, moja ni ya *specksaver* na moja ni ya *sightsaver* wakishirikiana na Lions Club kijiji cha Uroa na eneo la Kiembesamaki, lakini hiyo ikiwa haitoshi Mheshimiwa kuna

pia kambi ya saratani hasa kwa kinamama saratani ya matiti na shingo ya kizazi iliendeshwa mnamo tarehe 26 Novemba, Mnazi Mmoja na akinamama zaidi ya 600 walijitokeza ilikuwa *very successful camp* kina mama zaidi ya 600 walijitokeza kwenda kupima. Kwa hivyo la muhimu hapa naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi kupitia Baraza lako pia naomba wananchi tunapotoa matangazo ya kambi hizi, ambapo wataalam wetu wanashirikiana na wataalam wa kimataifa ambao wanaomba sasa hivi wako wengi sana wanaomba kushirikiana na sisi basi tunaomba sana wananchi wajitokeze ili kupatiwa hizo huduma na tunaendelea kutoa bila ya malipo, vile vile ilipokuwa sera ya Chama cha Mapinduzi na sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba tunatoa huduma bila ya malipo, yaani matibabu bure.

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mauri sana ya Mhe. Waziri pia tuipongeze Serikali ka mipango yake madhubuti aliyosema naomba kuuliza suala dogo sana la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).
Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kuwa maradhi haya yasiyoambukiza yanakuja kwa kasi na yanatakiwa kukingwa.

(a) Je, Serikali imehamasishwa je wananchi ili kufanya mazoezi na mambo mengine ambayo yatakuwa yanaweza kutokea kama hayo.

(b) Ni madaktari wangapi wa *Cardiologist* na wengine *Internal Medicine* Serikali imewasomesha kwa kipindi hichi ili kukabiliana na wimbi hilo kubwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, Serikali na Wizara kwa ujumla inaendelea kuhamasisha wananchi katika njia mbali mbali juu ya jambo hili jema la kufanya mazoezi, elimu hii huwa inatolewa wakati wa *clinic* wanapokwenda wagonjwa na hasa akinamama na wajawazito wanapokwenda *clinic*. Lakini pia wagonjwa wa aina mbali mbali wa *pressure*, wa sukari wanapokwenda kwenye *clinic* zao basi kabla ya kupata matibabu kwanza huwa wanapata elimu ya afya na huwa wanakumbushwa na kuelemishwa mambo haya yote ya mlo, watumie mlo gani wafanye nini lakini pia wanasisitizwa sana kuhusu suala la mazoezi.

Kupitia nyinyi Waheshimiwa wetu tunaomba sana nyinyi mna watu mna wapiga kura mna jamii kwa hivyo tunaomba na nyinyi pia muhamasishe wapiga kura na wananchi wetu katika suala hili la mazoezi ni suala muhimu, lakini hata miongoni mwenu pia mimi nikiwa mwana mazoezi siwaoni katika vikundi vya mazoezi, naomba sana waheshimiwa tujitupe katika viwanja mbali

mbali na Baraza letu nakumbuka lilituba barua maalum ili tujitupe kwenye viwanja kwa ajili ya kufanya mazoezi.

Mhe. Spika, kuhusu swali la (b) kwa kweli nikiri kwamba sina takwimu kamili Mheshimiwa naomba unisaidie.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumjibu mtaalam bingwa Mhe.Mohammed Said Dimwa katika sekta hii ya afya hasa masuala ya maabara. Mhe. Spika, naomba nimjulishe Mhe. Mohammed Said pamoja na Baraza lako tukufu kwamba hivi sasa tuna Ma-*Cardiologist* wawili pale Mnazi Mmoja ambao pia kuna ma-*physician* wawili. Mkurugenzi wa Mnazimmoja mwenyewe pia ni *physician* ni Dkt. Ali Salum, lakini wakati huo huo tuna *Internal Medicine* wawili. Naomba nimshukuru tena sana Dkt. Ali Mohammed Shein hivi karibuni tulikwenda kuomba idhini ya kutumia fedha za ziada kwa ajili ya kuwapeleka vijana wetu 7 nchini Egypt nadhani na wengine mlikuwa mashahidi, kwa sababu hata ile *field* yake mwenyewe *biochemistry* imepata mtu safari hii.

Kwa hivyo tulipata idhini ya kupeleka vijana 7 na tunashukuru sana Chuo kikuu cha Alexandria pamoja na Mhe. Balozi Hamza ambae ndie aliyekuwa mahiri na mstari wa mbele kuleta nafasi hizi za masomo kwa vijana saba. Vijana 7 hao wakienda idadi yote jumla ya madaktari ambao watakuwa nje ya nchi kwa mara ya kwanza katika historia ya Zanzibar ni 124 wakiwa masomoni, kwa mara ya kwanza katika historia ya Zanzibar madakrati 124 wako nje ya Zanzibar masomoni, watakaporudi wote hawa basi eneo hili litakuwa halina tena upungufu wa aina yoyote.

**Mhe. Hamad Abdalla Rashid:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika majibu ya Mhe. Waziri amejibu kwamba kuna vifaa mbali mbali vimeletwa na vimejaa katika mahospitali na vituo vya afya.

a) Mimi kwanza ningependa kujua ni vifaa vya aina gani hivi.
b) Pamba vimepelekwa vingapi na katika vituo gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Jumla ya vifaa vilivyopelekwa ni vingapi siwezi kujibu nikiri sina takwimu,hapa ni pahali patakatifu pa kujibu neno au swali ambalo ni makini na lenye usahihi. Lakini vimepelekwa vifaa zikiwemo mashine za kupima presha, zikiwemo baadhi ya seti zetu za *Delivery* na mambo mengine tofauti, na vimepelekwa karibu katika vituo vyote ambavyo vilikuwa

na mahitaji, kuna vituo ambavyo havina mahitaji vina vifaa ambavyo vinatumika hakuna matatizo havikupelekwa.

Lakini vile vituo vyote ambavyo vina mahitaji basi tulihakikisha tunafikisha vifaa hivi bila ya matatizo.

**Mhe. Waziri wa Afya**: Namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kutumia utakatifu wa pahala hapa, naomba kuongeza katika majibu hayo Mhe. Hamad Gerei vifaa vilivyoletwa ambavyo vinahusiana na masuala haya yaliyoulizwa kwenye swali ni *glucomiter*, yeye anajua *glucomiter* ni ile ambayo unatobolewa hapa kutoa damu na kutiwa kwenye ile *strip* na kusomwa sukari yako iliyokuwa kwenye damu, sio chumvi, wengine wanafikiri na chumvi inasomwa hapa hapa ni sukari tu. Lakini pia mashine za *pressure* tumeletewa kwa wingi sana. Tumeletewa pia *wheighing scale* ambayo inatumika kwa kupima uzito wa mwili ili kuweza kufanya ile *calculation* ya *body mass index* yaani kuangalia uzito wako, urefu wako ambao unakwenda sambamba na hali yako ya kiafya halafu unapewa hesabu pale. Lakini pia tumepewa kile kipimo cha kupima urefu.

Mara ya mwisho tumepokea misaada kutoka sehemu mbali mbali, tumepokea misaada kutoka kwa wenzetu Wami, Saud Arabia, Lions Club wa Dar-es-Salaam, tumepokea misaada kutoka *Rotary Ilala Health Center*. Hivi ni vingi siwezi kutoa idadi yake kamili, lakini vipo vingi na vituo vyote naomba nimwambie, vituo vyote vimesambazwa ila baadhi ya wakati kinachotokewa *staff* huondoka nacho ndio maana tunachukua hatua tunakuwa wakali. *Staff* anapoondoka nacho kifaa kama kile cha *blood pressure mashine* pia zimeletwa nyingi *digital* unafunga hapa lakini unasoma tofauti na ile ya zamani ya kubonyeza. Kwa na sisi tunaendelea kutoa wito kwa *staff* wetu wote kwamba hivi vifaa vimeletwa kwa ajili ya vituo, vinatakiwa vibakie kwenye vituo. Ila vingapi vimesambazwa hilo jibu tutampatia Mheshimiwa kwa maandishi. Ahsante.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe maswali yamekwisha ingawa muda bado tunao kidogo nina tangazo la wageni, Waheshimiwa wageni waliopo ni wageni wa Mhe. Nassor Salum Ali (Jazirra) Mwakilishi wa Kikwajuni jumla yao ni (11) hawa ni Kamati ya mchezo wa Nage Mapinduzi Cup.

Wageni wenyewe ni:

1. Ndugu Haji Sultan Mtembe — Rais wa nage Zanzibar
2. Ndugu Kombo Juma Maalum — Mjumbe wa Kamati

3. Ndugu Mussa Kassim Mussa Mjumbe
4. Ndugu Abdulrahman Azzan Mjumbe

Ahsante karibuni sana Baraza la Wawakilishi. Katibu kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA KAMATI

### Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Mhe Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati yangu ya Mawasiliano na Ujenzi. Naomba kuwasilisha Ripoti au Muhtasari wa Ripoti ya Kamati hii ya Mawasiliano na Ujenzi katika wizara mbili (2) kupitia katika bajeti ya mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naona maji hapana, naomba maji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kuweza kukutana leo hii ili kuendelea na shughuli zetu za kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, napenda kukushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kuwasilisha ripoti hii,

Mhe. Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi imepewa majukumu ya kusimamia Wizara hizi zifuatazo:-

1. Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira; na
2. Wizara ya Ujenzi, Mawasilino na Usafirishaji.

Mhe. Spika, kama zilivyowasilisha Kamati nyengine za Baraza la Wawakilishi, Kamati ya Mawasilino na Ujenzi ilifanya kazi kwa muda wa wiki sita (Unguja na Pemba) kwa kukagua na kutembelea taasisi mbali mbali zilizo chini ya Wizara hii tunazozisimamia. Aidha, Kamati kwa kushirikina na Wizara husika, ilibahatika kutembelea Tanzania Bara ili kujifunza kwa vitendo na hatimae kuweza kuishauri Serikali ipasavyo. Kamati pia ilitembelea Bandari ya Tanga na Dar-es-Salaam, Songosongo, Kituo cha Umeme Rasi Kiromoni. Kamati pia ilipata nafasi ya kwenda Mombasa (Kenya) kwa ajili ya kujifunza masuala ya uwekezaji kwenye hifadhi ya mafuta na gesi yanayohifadhiwa na kusafirishwa nje ya nchi pamoja na miundombinu mingine inayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, pia, katika kuhakikisha kwamba maswali mbali mbali yanayogusa taasisi zinazosimamiwa na wizara hii, Kamati iliwakutanisha Viongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango, pamoja na Mfuko wa Barabara, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Viongozi wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ili kuweza kukwamua ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe Fuoni ambayo pale ilipokwama. Aidha, Kamati ilisafiri tena hadi Tanzania Bara kukutanana na viongozi wa Wizara ya Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Uongozi wa TANESCO ili kuzingatiana na kuweza kulitatua tatizo la deni la umeme la Zanzibar pamoja na madeni ya Shirika la Umeme inayodai Taasisi za Jamhuri Muungano Tanzania.

Vile vile, kamati yangu ilikutana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Muungano pamoja na uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti na Usafiri wa Baharini SUMATRA ili kuzungumzia changamoto zinazogusa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati (ZURA) pamoja na Mamlaka ya Usafiri wa Baharini ( ZMA).

**Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira**

Mhe. Spika, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ni Wizara mama katika mfumo wa utoaji wa huduma za kijamii kwa wananchi wa Zanzibar. Aidha, Wizara hii ina dhamana ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wa Zanzibar wanafaidika na huduma bora za maji, matumizi bora ya ardhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira pamoja na upatikanaji bora wa nishati unaosimamia uendelevu kwa maisha yao.

**Kamisheni ya Ardhi**

Mhe. Spika, Kamisheni ya Ardhi inaundwa na Idara ya Ardhi na Usajili (ikiwemo Mahakama ya Ardhi, Afisi ya Mrajis wa Ardhi na Bodi ya Uhaulishaji), pia Idara ya Upimaji na Ramani pamoja na Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Kamati yangu ilipata fursa ya kuzikagua taasisi zote hizo chini ya Kamisheni ya Ardhi na kugundua changamoto kadhaa zinazohitaji kufanyiwa kazi kama zinavyoonekana ndani ya ripoti hii ili kuweza kuleta ufanisi mzuri kwenye wizara.

Mhe. Spika, moja ni kukosekana kwa mfumo wa uhakika wa usajili wa ardhi, ambao kuchelewa kufanyiwa mapitio kwa sera ya ardhi, kuchelewa upimaji wa viwanja na utoaji wa hati baada ya kupimwa, kumepelekea kuwepo kwa migogoro sugu ya ardhi ambayo inachukua muda mwingi watendaji kuweza kuitatua. Aidha, changamoto nyengine zinazoikabili Kamisheni ya Ardhi ni

upungufu wa wataalamu hasa wenye utaalamu wa utawala, usimamizi na uthamini, usajili na utambuzi wa ardhi.

**Mhe. Spika**: Tafadhali kidogo nimpishe Mhe. Naibu Spika, halafu utaendelea. Mhe. Naibu Spika tafadhali

*(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)*

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa Mwenyekiti tuendelee.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Mhe. Naibu Spika, vilevile, kwa mujibu wa wataalamu wa sheria kuna changamoto nyingi kwenye sheria mbali mbali za ardhi ambazo zinahitaji marekebisho muhimu ili kuzipa nafasi nzuri taasisi zinazotoa ardhi na wale wanaopewa ardhi na hatimae kuepusha matatizo mengi ya kisheria hapo baadae.

Mhe. Naibu Spika**,** changamoto nyingine kubwa iliyopo na inayohitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka ni malimbikizo ya madeni ya Wazee wa Mahkama ya Ardhi *ma-accessor* wa Mahkama ya ardhi, kwani hadi hivi sasa hakuna bajeti yoyote iliyopangwa wala hakuna Fungu *(vote)* inayosimamia malipo yao. Matokeo yake wafanyakazi wa Mahkama ya Ardhi ndio wakati mwengine hutumia mishahara yao kuweza kuwasaidia Mahakimu wa Mahkama ya Ardhi kuweza kujihikimu wakati ambapo ma-*accessors* hao ndio ambao wanaowasaidia Mahakimu kuweza kutatua kuhukumu na kutatua kesi za migogogoro ya Ardhi, kwani bila ya wao hakuna kesi itakayoweza kuendeshwa. Kutokana na hali hiyo, kamati yangu inaitaka Wizara ya Fedha kwanza kuwalipa malimbikizo yao Wazee wa Mahakama ya Ardhi yaani ma-*accessors* wote lakini pia katika kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hili ni lazima kwenye bajeti ya mwaka huu wazee hao waweze kupangiwa fungu lao yaani *vote* ya ili kuweza kuondosha matatizo hayo.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu pia inaitaka Mahakama Kuu wanapoandaa programu za semina na mafunzo mbali mbali basi kuhakikisha kwamba Mahakimu hawa wa Mahakama ya Ardhi na wao pia wamekuwa wakiwaingiza katika programu hiyo kwani kwa hivi sasa wamekua kama mayatima hawapati mafunzo yoyote na semina zozote ambazo zinaandaliwa na Mahakama Kuu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Mawasilino na Ujenzi inaishauri Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kuwa na chanzo kimoja cha kitengo tu cha usajili ardhi katika taasisi zake zote zinazohusiana na masuala ya ardhi. Aidha,

kamati pia inaiomba Kamisheni ifanye utafiti maalumu kuangalia mahitaji ya wananchi wa kuweza kupata makaazi bora, ili kuondokana na migogoro mtambuka ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, wakati huo huo, kamati yangu haikuridhishwa kabisa na hali ya jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Ardhi hapo Vuga, hivyo tunaitaka serikali kupitia wizara kwa ujumla kuwapatia Mahkama ya Ardhi jengo jengine la kufanyia kazi ili kunusuru afya za wafanyakazi wake, kutokana na uchakavu wa jengo linalotumika hivi sasa. Pia Kamati yangu imegundua kua kuna baadhi ya wafanyakazi wanatumikia nafasi zaidi ya moja kwa wakati mmoja ili kuziba pengo wakati ambapo kuna maombi tayari yameshapelekwa Idara ya Utumishi wa Umma lakini bado ruhusa ya kuajiri haijatolewa. Hivyo, kamati yangu inaiomba Wizara na Serikali kulishughulikia tatizo hili ili kuweza kulipatia ufumbuzi unaofaa. Changamoto nyingine ni usafiri wa Mahakimu hasa katika kufuatilia kesi za migogoro mbali mbali ya Ardhi yaliyokuwepo hapa Zanzibar.

1. **Eneo la Uwekezaji Mangapwani**

Mhe. Naibu Spika, serikali imetoa tamko katika eneo la Mangapwani limetengwa kwa ajili ya uwekezaji mkubwa wa shughuli zote zinazohusiana na masuala ya Mafuta na Gesi Asilia, ikiwemo kuhamishia matangi ya Mafuta yaliopo Mtoni Unguja na kuyahamishia huko Mangapwani.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaupongeza sana mpango huo wa serikali lakini kasi ya utekelezaji wake hairidhishi hata kidogo, kwani serikali inafanya maamuzi ya matumizi ya eneo hilo lakini hadi leo bado hakuna mchoro wa kuonyesha eneo hilo litaanzia wapi na kufikia wapi. Pia eneo hilo tayari limeshamilikishwa kuna baadhi wawekezaji wazalendo na kuweka miradi yao bila ya maelekezo maalumu na matokeo yake kila mmoja anaangalia ni uwekezaji gani unafaa katika eneo hilo na hivi sasa karibu wawekezaji watatu kati ya wanne waliopatiwa hati za ukodishwaji *(lease)* katika maeneo hayo tayari wameshaanza kuwekeza miradi yao mikubwa na ya gharama kubwa jambo ambalo kusema kwamba serikali itaweza kuwaondoa itawatia hasara kubwa kwani kuna baadhi ya uwekezaji hao tayari wameshakamilika na bado mambo madogo tu kuweza shughuli zao za biashara.

**Ushauri wa Kamati**

Mhe. Naibu Spika, ushauri wa kamati ni kwamba eneo hilo serikali ilipime haraka kisheria na hao wawekezaji waliomo kwenye eneo hilo waingizwe

kwenye mpango mkuu wa serikali ili waweze kukamilisha miradi yao na serikali iweze kufaidika na ajira kwa vijana wetu pamoja na mapato yatakayopatikana kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, katika eneo hilo la Mangapwani ni vyema serikali yetu ikajenga bandari maalumu itakayoweza kutumika kwa ajili zinazofanana na eneo hilo ikiwemo kufunga Meli kubwa na ndogo za mafuta, ambapo wazo hilo lipo, lakini pia serikali iwekeze kwenye ujenzi wa matanki ya kuhifadhia mafuta pamoja na Gesi Asilia.

Pia, kamati yangu katika eneo hilo ilitembelea miradi mitatu ikiwemo kituo cha kupokelea gesi kutoka Tanzania Bara na kujazwa kwenye mitungi yake na kuuzwa kwenye soko la ndani jambo ambalo limeanza kupunguza matumizi ya makaa na ukataji ovyo wa miti hapa Zanzibar kwa kutumia gesi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, vilevile, tulitembelea mradi wa Chelezo ambao pia unamilikiwa na muwekezaji mzalendo mradi ambao kwa hapa Zanzibar utakuwa ndio mradi wa mwanzo kwa wawekezaji binafsi ukiacha ule wa Shirika la Bandari ambao upo hapa Malindi ambao utatoa ajira nyingi lakini pia katika uchumi mkubwa wa mafuta na gesi kwa vyombo vidogo vidogo vya baharini vitaweza kufanyiwa matengenezo madogo madogo hapo inapohitajika.

Mhe. Naibu Spika, mradi wa tatu ni uwekezaji mkubwa wa matenki ya hifadhi mafuta yatakayotumika nchini na yale ambayo hapo baadae yataweza kusafirishwa nje ya nchi kama wanavyofanya nchi jirani zinazolingana na sisi. Hata hivyo, kamati yangu inaishauri wizara kuendelea kuwapa mashirikiano wawekezaji waliopo hivi sasa ili kuweza kuwapa miongozo ya miradi yao ili kuleta tija kwa nchi yetu hapo baadae. Pia Kamati yangu imegundua miradi hiyo iliyokwishaanza kuwekezwa haina madhara yoyote kwa uwekezaji unaotaka kufanywa na Serikali.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu ilipofanya ziara huko Mombasa nchini Kenya tumejifunza mambo mengi ikiwemo usalama wa uhifadhi wa matenki ya mafuta kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Kutokana na ziara hiyo tumejifunza kuwa mambo yote hayo ikiwemo serikali kujenga Bomba la kupakilia na kushushia mafuta ambalo wawekezaji wataweza kulitumia na kulipia ada maalum Serikalini, itaweza kuengeza pato kwa Serikali vile vile hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu pia ilifika katika eneo la uwekezaji Nungwi ambalo hadi hivi sasa muwekezaji mmoja Kampuni ya "*Spice Islander"* anashindwa kufanya shughuli zake za uwekezaji kutokana na mgogoro wa

maamuzi ya utumishi wa umiliki wa eneo hilo. Katika kulipatia ufumbuzi suala hili, Kamati yangu imeshangazwa sana na kusikitishwa sana na maamuzi ya serikali kupitia Waziri aliekuwepo hapo mwanzo kwa kumpa hati ya miliki ya kawaida *(Right of Occupancy)* mwananchi wakati eneo hilo ni la uwekezaji ambalo tayari hapo mwanzo limekwisha kutolewa *lease* kisheria.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inamshauri Mheshimiwa Waziri kwakuwa hati hii ya *(Right of Occupancy)* iweze kufutwa na kuweza kupishwa uwekezaji mkubwa wa hiyo Kampuni iliyokuwepo na huyo mwananchi kama anahitaji kupewa eneo kama hili aweze kupatiwa eneo nyengine ili mwekezaji aendelee na shughuli zake.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaipongeza sana serikali kupita Wizara hii ya Ardhi wa kuamua kuyafuta na kuyarejesha serikalini maeneo ya uwekezaji alopewa *"lease"* kwa muda mrefu ambao ameshindwa kuendeza na kuikosesha serikali mapato pamoja na ajira kwa vijana wetu. Hivyo, tunamtaka Mheshimiwa Waziri aitekeleze ile ahadi yake ambapo ilikua inamaliza muda wake mwezi wa Februari mwaka huu ili kutoa nafasi kwa wawekezaji wa kweli wanaotaka Ardhi kwa ajili ya kuwekeza waweze kwa utaratibu maalumu na kupewa *'lease'* na masharti yao wao na vile vile kwa masharti na wao wawekeze vyenginevyo na wao vile vile kama hakuweza kuendeleza ardhi hizo wanyanganywe. Lakini ikitokezea kuwa kuna muwekezaji baada ya eneo lake kufutwa ikiwa atakuja kuomba tena kwa masharti maalumu ya ujenzi basi na yeye aweze kupewa kipaumbele ili baada ya serikali kujiridhisha na kwamba kweli yuko tayari kuwekeza katika Mradi wake.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaishauri serikali kwa upande wa maeneo ya Ardhi waliyopewa wananchi wakawaida kwa ajili ya ujenzi wa makaazi serikali isifanye haraka ya kuyafuta maeneo hayo ili ipate muda wakuweza kuyahakiki na kuweza kuyajua umiliki wake lakini vile vile kuweza kuhamasisha wananchi kuweza kujenga maeneo hayo kwa sababu wengi wa wananchi wetu ni maskini na kipato chao ni kidogo kulingana na mishahara wanayolipwa Serikalini na katika taasisi binafsi. Kwa hivyo, kama tulivyokua malengo ya Mapinduzi matukufu ya 1964 kuweza kuwapatia wananchi makaazi bora ya kudumu wananchi wake basi si vyema na busara ikatumika ili na wao waweze kuwapa nafasi wananchi kuweza kuendeleza viwanja vyao na kuweza kujenga maakazi ya kudumu.

**Mamlaka ya Maji (ZAWA)**

Mhe. Naibu Spika, kamati imegundua kwamba pamoja na jitihada mbali mbali za serikali, na viongozi wa majimbo pamoja na wafadhili mbali mbali kulivalia

njuga suala la upatikanaji wa maji safi na salama bado kuna mapungufu makubwa ya kutokuwepo kwa uwiano kati ya maji yanayozalishwa na yale yanayohitajika. Hadi kamati inaandaa taarifa hii, hali ya uzalishaji wa maji ilikuwa ni asilimia 70.6 huku tukiwa na mapungufu ya uzalishaji karibu asilimia 29.4. Hapa nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuangalie vizuri jadweli na mchanganuo mzima wa uzalishaji wa maji na mahitaji kama inavyohitajika ndani ya ripoti yetu ili waweze kuishauri vizuri Serikali kuhusiana na upatikanaji wa huduma hii muhimu ya maji hapa nchini kwetu.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, kamati imebaini kuwa suala la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi bado ni changamoto kubwa isiyokuwa na ufumbuzi wa uhakika. Kamati yangu imesikitishwa sana na tabia ya wananchi kuvamia na kujenga karibu na vianzio vya maji jambo ambalo linachangia upungufu mkubwa wa upatikanaji wa maji kila kukicha wakati mahitaji ya maji yanaongezeka kila siku zikienda. Hasa kwa ujenzi na uwekezaji wa Mahoteli mbali mbali na ongezeko za nyumba za makaazi hapa visiwani kwetu kwa upande wa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, hivyo Kamati yangu inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka ikiwemo kuwabomolea majumba na vile vile kuwahamisha watu wote waliovamia vianzio vya maji ili kuweze kunusuru upatikanaji wa maji katika nchi yetu. Vyenginevyo Mhe. Spika tukiendelea kuwaruhusu watu kuendelea kujenga katika vyanzo vya maji tutakuja kufika pahapa hayo maji ya kunywa tutayakosa.

Mhe. Spika, vilevile, Kamati imebaini changamoto moja inayoikabili Mamlaka ya Maji kuwa na deni linalodaiwa Mamlaka hiyo na Shirika la Umeme pamoja na Madeni inayodai ZAWA kwa wateja wake kwamba yanarejesha nyuma sana kazi kikubwa ya utendaji wa Mamlaka hiyo. Ili kuweza kusaidia kupunguza ugumu wa ukusanyaji wa ada za maji na kuongeza mapato ya Mamlaka, Kamati yangu inaishauri Mamlaka ya Maji kuanzisha mradi maalumu wa uwekaji wa Mita katika kila nyumba ili kuwawezesha wananchi kulipia maji kupitia simu zao za mkononi kama inavyofanya katika ununuzi wa umeme, jambo hili litaweza kuongeza si tu ukusanyaji wa mapato lakini pia litasaidia kujua takwimu halisi ya watumiaji wa maji ma mahitaji ya maji katika maeneo yote ya Zanzibar. Ni wazi kuwa makusanyo yatakayopatikana yataiwezesha Mamlaka kuweza kuyatumia mapato hayo kuweza kuimarisha miundombinu ya maji ikiwemo ununuzi wa mabomba mapya.

Mhe. Spika, kamati yangu imeshuhudia kiwango cha maji kinachozalishwa kwa sasa ni kidogo kutokana na sababu hizo hapo nilizozielezea hapo juu na

hadi Kamati inaandaa Ripoti hii ZAWA ilikua inadaiwa deni la umeme Tsh. 15,999,062,028.38 yanayotokana na vituo vya uzalishaji wa maji na Shirika la Umeme na Tsh. 1,962,426,428.44 yanayotokana na wasambazaji *(Suppliers).* Aidha, ZAWA ilikua ikidai wateja wake jumla ya Tsh. 8,378,846,275.

Mhe. Spika, pia, Kamati yangu inaishauri Serikali katika kuongeza upatikanaji wa maji kuharakisha kuviunga na kivitia umeme visima vyote vilivyochimbwa na mradi wa Ras al Khaimah kwani visima vipo vingi lakini karibu asilimia 60 bado havijaungwa umeme, kwa hivyo kupitia fedha za ufadhili kutoka Serikali ya India, Kamati yangu inashauri Serikali kuweza kutumiwa fedha hizo kwa ajili kuweza kukamilisha uungaji wa umeme katika visima hivyo ili kupunguza tatizo la maji.

Mhe. Spika, kamati yangu inaiomba ZAWA ifanye uhakiki wa kutosha na kukagua upotevu wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu yake na baadae kutoa ripoti kwa wadau wote ikiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili kuweza kujua ukubwa wa tatizo hilo na ili tuweze kutoa ushauri.

## SHIRIKA LA UMEME, ZANZIBAR (ZECO)

Mhe. Spika, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) pamoja na mafanikio makubwa inayoyapata kwa kuwasambazia Umeme wananchi mijini na vijijini lakini linakabiliwa na changamoto kubwa hasa ya kutokulipwa asilimia ya fedha zao za huduma zinazokusanywa na Serikali huku ikikabidhiwa majukumu makubwa ya kusambaza umeme kote nchini. Pia taasisi nyingine za Serikali SMT na SMZ pia taasisi za Serikali SMT nyingi hazilipi bili zake za malimbikizo ya umeme kama inavyotakiwa, lakini vile vile pia kuna changamoto nyengine pia madeni ya watu binafsi ambayo Shirika wanaendelea kuitatatua.

Hata hivyo, Kamati yangu imebaini kwamba ongezeko la madeni kwa taasisi za Serikali, Shirika kuendelea kutumia mfuko wake kwa kazi kuendelea kusambaza umeme vijijini, na deni kubwa la ununuzi wa umeme kutoka TANESCO ni miongoni mwa Changamoto kubwa kwa Shirika hili.

Mhe. Spika, katika kujaribu kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo, Kamati yangu inaitaka Serikali kuanzia Bajeti ya mwaka huu hapa Mhe. Spika naomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais pamoja na mawaziri wote wanisikilize.

Mhe. Spika, kamati yangu katika kuweze kutatua au kulipatia ufunguzi changamoto hizo Kamati yangu inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuanzia bajeti ya mwaka huu kuanzisha utaratibu wa kuwalipa moja kwa moja ZECO yaani Shirika la Umeme kupitia vifungu vyote vya Wizara za Serikali ili kulikomboa Shirika kuepukana na madeni makubwa ambayo inabeba mzigo mkubwa.

Mhe. Spika, kamati yangu bado inaitaka Serikali kuu kuingilia kati suala la deni la umeme inayodaiwa na TANESCO kila mwezi kwani sio sahihi ZECO kuweza kulipishwa *"Utility service charge"* ambapo wakati Zanzibar umeme unasambazwa na ZECO na sio umeme unasambazwa na TANESCO kama ilivyo kwa wateja walioko Tanzania Bara. Lakini pia sio haki kwa TANESCO Kuilipisha ZECO bei ya umeme sawa sawa na wateja wengine binafsi wakati ZECO kila siku wanatumia gharama zao za kusambaza umeme hapa Zanzibar.

Pia Kamati yangu ilikwenda hadi Tanzania Bara kusaidia kurekebisha hali hiyo lakini bado suala hili linaonekana ni zito kwa upande wa Shirika peke yake bila ya Serikali Kuu kuingilia kati kuweza kupata ufumbuzi wake kwzani bado umekuwa mgumu, kwani suala hili linagusa uchumi wa Zanzibar moja kwa moja kwa hivyo pia linahitaji maamuzi magumu ya kisiasa kutokana na maumbile ya Muungano wetu.

Aidha, Kamati inaendelea kuishauri ZECO iongeze ulinzi katika Vituo vyake vyote vya Uzalishaji Maji na Usambazaji umeme hususan katika maeneo ya Fumba, Mtoni pamoja na Rasi Kiromoni.

**Mradi wa Nishati Mbadala**

Mhe. Spika, kamati yangu inaishauri Serikali kupitia mpango wa mradi wa kutafuta Nishati mbadala ni vyema kuharakisha mchakato huu na kuweza kupata umeme mbadala wa uhakika.

Kamati yangu haijafurahishwa na kiwango kidogo sana kinachopatiwa Idara hii katika bajeti ambapo inasababisha uhaba wa vitendea kazi na hupelekea watumishi wakati mwengine watendaji wa Serikali au watendaji wa taasisi hii kuweza kutumia *'Computer'* zao kwa ajili ya kufanya kazi za Serikali.

Ukiacha ufinyu wa Bajeti, hata mazingira yao (wafanyakazi) wanayofanyia kazi bado katika eneo hili sio mazuri. Ufinyu wa nafasi yao katika ofisi iliyopo hivi sasa hivi haileti haiba na kazi zao za kitaalamu kama inavyohitaji. Kamati

yangu inaiomba Serikali katika ujenzi wa jengo jipya la Wizara kuzingatia kuwapatia nafasi ndani ndani ya jengo hilo Idara hii ya Nishati ili waweze kufanya kazi zao kwa utulivu.

Mhe. Spika, kamati yangu ilipokea taarifa na kukagua maeneo yaliyotolewa iliyojengwa minara ambayo ni Makunduchi, Mbuyu Tende na Bambi kwa Unguja na Mwambe, Micheweni kwa ajili ya Pemba pamoja na Kiuyu-Maziwa Ngombe.

Hata hivyo, Kamati yangu bado haijaridhishwa sana na kasi ya mradi huo wa kufanya utafiti wa umeme mbadala kwa hiyo tunaiomba Idara iweze kuzidisha kasi ili tuweze kupata uvumbuzi wa kupata umeme mbadala.

**Mafuta na Gesi Asilia**

Mhe. Spika, kamati inaipongeza Wizara hasa kupitia Mhe. Waziri kwa kuleta Mswada wa Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar ikiwa na lengo la kuanza shughuli za utafutaji, usimamizi na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar. Aidha, Sheria hiyo imepitishwa na Baraza la tukufu tarehe 27/10/2016 na kuwekwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mnamo tarehe 15/11/2016 pale Ikulu Zanzibar.

Mhe. Spika, kamati inataarifa kwamba tayari Wizara imeshawasilisha Mpango kazi wa suala hilo Baraza la Mapinduzi (BLM) ambapo hatua za kuazishwa kwa Kampuni ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) na Mamlaka ya Usimamizi wa Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) zimo katika hatua ya uteuzi wa Viongozi.

Kamati yangu inawaomba wadau wote Duniani wenye nia na dhati kuja kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya kuingia mikataba na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa upande wa Serikali kupitia Mamlaka itakayoundwa kuanza na kutoa elimu kwa wananchi wetu ili kujiandaa na kupokea uchumi huo mpya pia kujiandaa na kukabiliana na changamoto nyingi wakati wa utafiti na uchimbaji wa rasilimali hizo za mafuta na gesi, kwani katika baadhi ya nchi nyingine kumejitokeza misuguano baina ya Serikali na wananchi wake wakati harakati za maandalizi kama Sheria inavyoeleza kuwa kabla ya kuanza uzalishaji wa rasilimali hiyo ni lazima tathmini ya mazingira ifanyike ili kujua ni athari gani

zitakazojitokeza wakati wa zoezi hilo na wananchi waweza lakini vile vile na wananchi wataweza kulindwa katika kiasi gani pale athari itakapotokezea.

Vile vile, Kamati yangu inapongeza uanzishwaji wa Kamati ya Makatibu Wakuu wa Wizara zetu mbili ya Serkali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinazoshughulikia Nishati ya Mafuta na Gesi. Kamati hii tunategemea itaweza kufanya kazi zake vizuri kwa uadilifu mkubwa kwa kufuata nia njema ya Muungano wetu kuzingatia mipaka ya asili lakini vile vile nia njema ya viongozi wetu waasisi wa Muungano wetu, ili kuleta mafanikio kwa nchi yetu na Serikali zetu zote mbili. Pia tunategemea kwenye Kamati hiyo SMT na SMZ wataweza kutoa msaada mkubwa wa kitaalamu kwani wao wenzetu kupitia TPDC wameshaanza Uzalishaji rasilimali ya Gesi kwa muda mrefu kwa hivyo wameshakumbana na changamoto nyingi za kitaalamu na kisheria katika uingizaji wa mikataba na pia uzalishaji pamoja na uendeshaji wa shughuli zenyewe.

Mhe. Spika, pamoja ha hatua hizo nzuri, bado Zanzibar inakabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa wataalamu katika sekta Mafuta na Gesi Asilia kwa hivyo tunaiomba Serikali yetu kusomesha vijana wengi ili kuja kushiriki kitaalamu katika harakati katika uchumi huo mkubwa wa Mafuta na Gesi Asilia.

Mhesimiwa Spika, kamati yangu inaitaka Serikali kupitia Bajeti inayokuja kutenga fedha za kutosha kwenye Mamlaka itakayoundwa ili kuweza kuwa na ofisi za kisasa pamoja na wataalamu wa kutosha. Vile vile, Serikali kuwaajiri vijana wasomi katika fani ya Mafuta na Gesi Asilia ambao baadhi yao tayari wameshamaliza masomo na wapo hapo Zanzibar wanasubiri kupatiwa ajira. Ni vyema kwa Serikali kuwaandalia mazingira mazuri ya kuwaajiri wale walioko vyuoni lakini vile vile wakimaliza nao kuwaajiri kujiendeleza na baadae kuweza kupata wataalamu wetu wa ndani kwani sekta hii kama hatukujipanga kuwa na wataalamu wetu wa ndani basi itakua ni hasara kwetu. Pamoja na hayo, kutokana na unyeti wa shughuli hizo ni vyema wataalamu hao kuweza kuwapatia maslahi mazuri ili kuweza kuwadhibiti na kuweza kutumia juhudi zao katika kushughulikia masuala la rasilimali ya mafuta hapa Zanzibar.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati, Zanzibar (ZURA)**

Mhe. Spika, wakati Kamati yangu inapokea taarifa ya ZURA, imegundua kwamba kutokuwepo kwa mfumo huru wa uingizaji wa mafuta, uchakachuaji na magendo ya mafuta kunasababibisha nishati hii kuwa ghali. Aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa mpango wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati (ZURA) na Sheria nyengine zikiwemo zinazodhibitiwa

kama vile ile ya Shirika la Umeme pamoja na Maji. Aidha, Kamati imebaini kuwa tozo inayotozwa kwa mafuta yanayopakiwa kutoka Dar es salaam kuja Zanzibar ni kubwa mno ambapo badala ya kutozwa Dola tatu kwa Tani lakini sisi hapa Zanzibar tunatozwa Dola kumi tofauti na wanavyotozwa nchi za jirani ambazo nchi kama Kenya, Uganda na Kongo wanatozwa dola tatu wakati Zanzibar sisi tunatozwa dola kumi. Suala hili ni kubwa sana linasababisha kuongezeka kwa bei ya mafuta na kumuumiza mtumiaji. Kamati yangu imeweza kushirikiana na Mamlaka ya ZURA kwenda hadi Tanzania Bara ambapo tumeahidiwa kuwa suala hili litasawazishwa hivi karibuni kabla ya Mwezi wa April. Namuomba Mheshimiwa Waziri muhusika na yeye akija kuchangia ripoti ya Kamati yetu atueleze suala hili limefikia kama wizara ya Jamhuri ya Muungano kama wameshaanza kulifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka kubadilisha Mfumo wa uagizaji wa mafuta nchini kwa kutumia mfumo wa Uagiziaji wa pamoja. Aidha, Kamati yangu inaiomba Wizara kuzifanyia mapitio Sheria zote za sekta zinazodhibitiwa na Mamlaka hii ili ziendane sambamba na majukumu ya ZURA ili kuepusha mgongano wa kisheria. Vilevile, Kamati yangu inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kuwa na Taasisi moja tu inayoshughulikia masuala ya uchakachuaji na ukusanyaji wa mapato ya mafuta, ili kuweza kudhibiti mapato hayo yatokanayo na rasilimali hiyo.

Mhe. Spika, kamati pia inaipongeza Mamlaka ya ZURA kwa kudhibiti mapato yao na pia iendelee na mpango wake wa kutaka kujenga jengo lao pamoja na jengo la Wizara na taasisi zake ili ziweze kufanya kazi zao vizuri. Pia Kamati inaitaka ZURA kuendelea na mpango wao wa *program* yake ya utafiti wa ujenzi wa Bandari maalumu ya kuteremshia na kupakilia mafuta huko Mangapwani kwani suala hilo ni zuri kwani hata wenzetu ukiangalia tulipokwenda Jamhuri ya Watu wa Kenya tumegundua Serikali na wao wameshiriki katika uwekezaji wa miundombinu ya Mafuta na Gesi kwa hiyo si vibaya na ZURA na wao kuweza kushiriki katika mradi huo.

**Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira na Idara ya Mazingira**

Mhe. Spika, kamati yangu inapongeza kazi kubwa na ngumu zinazofanywa na Mamlaka hizi mbili za kuzuia na kudhibiti uchafuzi wa Mazingira vile vile kuvilinda vizazi vya leo na kesho na kuweza kuishi katika mazingira mazuri. Lakini kamati yangu imesikitishwa sana na hali iloyoikuta katika Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA) pamoja na Idara ya Mazingira ambapo Wakurugenzi wawili wanatumia chumba kimoja cha Ofisi moja, hali

inayopelekea kukosekana kwa uhuru na faragha ya utendaji wa kazi. Kamati yangu inaitaka Serikali kuweza kuwapatia wakurugenzi hao kila mmoja na ofisi yake ili wawe na faragha katika kufanyia shughuli zao, lakini pia jengo hilo halina nafasi ya kutosha na kupelekea wafanyakazi kufanyakazi kwa kujibana na katika mazingira magumu.

Aidha, Kamati yangu haifurahishwi na tabia ya utupaji ovyo wa taka pamoja na maji machafu ya kwenye makaro pale katika eneo la maruhubi pia maji yanayotapishwa kwenye vyoo na makaro kutupwa pale maruhubi suala hili linapaswa kusitishwa mara moja na kutafutwa eneo jingine nje ya mji ambalo litajengwa kitaalamu ili kuweza kulinda Mazingira na maisha ya watu wote kwa ujumla.

## WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

Mhe. Spika, baada ya kumaliza muhtasari wa Ripoti yetu kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, sasa naomba uniruhusu niendelee na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ambayo imepewa jukumu kuu la kusimamia Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar.

Mhe. Spika, kabla ya kuichambua ripoti ya Wizara hii, naomba kwa sekunde chache tuangalie utekelezaji wa baadhi ya miradi pamoja na changamoto zake zilizojitokeza katika miradi ifuatayo:-

1. Jengo Jipya la Abiria (Terminal II).
2. Ununuzi wa MV Mapinduzi II.
3. Mradi wa Mkongo wa Taifa na baadae kukatwa wakati wa utanuzi wa Barabara.
4. Ujenzi wa Matengenezo ya Barabara ya Fuoni.
5. Mradi wa mataengenezo ya Jumba la treni, Darajani ‘Corridor’

Mhe. Spika, hayo baadhi tu ya Miradi inayosimamiwa na Wizara hii na nafikiri utekelezaji na changamoto zilizojitokeza iwe fundisho tosha wakati tunapotaka kuingia katika miradi mikubwa kama hii.

## SEKTA YA UTAWALA

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ndio dira na kioo cha usimamizi na ufanisi wa mipango ya Wizara hii muhimu katika nchi yetu. Hata hivyo, Kamati yangu imegundua kwamba kuna mapungufu machache tumeyagundua katika Idara ambapo katika kusimamia baadhi ya taasisi zake zilizo chini yake. Hivyo basi, Kamati yangu inaishauri Idara hii kuangalia mapungufu hayo tuliyoyaona na

kama ushauri tullivyoutoa kamati kuhakikisha kwamba miradi yote inayofanywa na idara zote zilioko chini ya wizara hii basi Idara hii lazima ishiriki kikamilifu ili baadaye kuja kukumbia ili migongano wakati wa utekelezaji wa mradi hii.

Mhe. Spika, moja katika changamoto ni kukosekana kwa mawasiliano mazuri baina ya Idara ya Mawasiliano, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Mkongo wa Taifa ambapo kuna maeneo uliopitishwa Mkongo huo kila barabara zitakapoweza kutanuliwa basi inabidi Mkongo huo uweze kuathirika kwa kukatwa. Jambo hili ambalo litaigharimu Serikali mamilioni mengi ya shilingi kama ilivyotokea huko kwenye barabara ya Fuoni na pia hali hii tunaitegemea itakuwepo vile vile katika barabara inayotarajiwa kujengwa Kihinani - Mahonda hadi Mkwajuni pamoja na barabara nyingine. Kamati yangu inaishauri Idara hii kuhakikisha kwamba inasimamia kwa karibu zaidi miradi yote mikubwa ya Wizara hii ili kuweza kuokoa fedha za umma huko baadaye.

Mhe. Spika, kamati yangu imegundua kuwa Wizara hii ina Bodi karibu tano ndani ya wizara hii na zimeteuliwa kwa mujibu wa sheria lakini kwa bahati mbaya hazina bajeti mmalum iliyopangiwa kuendesha bodi hizo na vile vile kuweza kushindwa kufanya kazi zake kama ilivyokusudiwa ikiwemo Bodi ya *Condominium*, Bodi ya Usafiri na Leseni, Bodi ya Wasanifu na Wakadiriaji wa Majengo, Bodi ya Udhibiti wa Kodi za Nyumba pamoja na Bodi ya Wakandarasi. Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa katika Bajeti ya mwaka huu, Bodi hizi zote zilizomo kwenye Wizara hii zinatengewa fedha kwa ajili ya kufanya shughuli zao kama Sheria inavyoelekeza. Lakini pia Kamati yangu inaitaka Idara hii kutokurejea tena kasoro iliyojitokeza kupanga na kufanya mradi wowote bila ya kupitia Idara ya Mipango na Sera kama nilivyoeleza hapo mwanzo.

**SHIRIKA LA NYUMBA**

Mhe. Spika, kamati ilipokea taarifa ya Shirika la Nyumba na kutembelea baadhi ya Nyumba za Maendeleo za Kilimani, Mtemani, Madungu pamoja na Kengeja. Kamati haikuridhika kabisa na hali ya usafi, mfumo wa maji taka na uchakavu wa Nyumba hizo.

Hata hivyo, Kamati inatoa shukurani maalumu kwa Afisa Mdhamini wa Shirika hili la nyumba kule Pemba kwa jitihada zake za kuanza majaribio (*Pilot Project*) ya kuziokoa nyumba hizi katika jengo lile la Madungu na Mtemani. Kwa kweli "*Pilot Project*" yake kuipitia kufanya baadhi ya

marekebisho katika mfumo wa maji machafu katika nyumba hizo ni ya kupigiwa mfano na gharama yake tumeona ni nafuu tunaiomba serikali kupitia wizara kuweza kuwapa nguvu ili kuweza kufanya shughuli ile na kuikamilisha.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaiomba wizara kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba kuongeza bajeti na kuwa bega kwa bega na Mdhamini wa Majengo kule Pemba ili kuhakikisha kwamba mradi ule wa usafi kuweza kurekebisha mifumo ya maji taka ili iweze kukamilika kama ilivyokusidiwa lakini vile vile kuyarejesha majumba katika hali yake ya kawaida. Aidha, kamati kutokana na jinsi nyumba za maendeleo zinavyoendelea kuchakaa na kuzingatia wananchi wanaoishi ndani ya nyumba hizo hawana uwezo wa kuzikarabati na kuzinusuru nyumba hizo ni pamoja na kunusuru maisha ya wakaazi wake, basi ni vyema nyumba hizo zirejeshwe serikalini kupitia Shirika la Nyumba na kuwafungisha mikataba maalum wakaazi wote wanaoishi humo kwa ajili ya kulinda usalama wa maisha yao. Vile vile, kamati inalitaka Shirika la Nyumba kufanya uhakiki na kuzitambua nyumba zake zote na kuziorodhesha katika daftari la Mali za Shirika (*Fixed Assert Register*). Na pia kuangalia zile ambazo wanaweza kuziendeleza na zilizokua hawaziwezi kuziendeleza basi kuziuza ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya kuweza kutengeneza nyengine ambazo zinazowezekana.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na uchakavu mkubwa wa nyumba za maendeleo ambazo ziko katika Mikoa yetu ya Unguja na Pemba na miongoni mwa nyumba hizo nyingi walipewa wananchi na wameshindwa kuzikarabati. Na kutokana na aina ya majengo ambayo ni ya Ghorofa ambayo kwa hivi sasa kama serikali yetu, haikuchukua hatua za haraka basi kwa baadhi ya nyumba hizo zinaweza kuhatarisha maisha ya watu wanaoishi katika nyumba hizo. Kamati yangu inaitaka serikali kufanya marekebisho ya sheria ili nyumba zote hizo zirejeshwe serikalini ili serikali iweze kufanya utaratibu maalumu kwa ajili ya watu wanaoishi humo kuweza kupangishwa kwa ada maalumu na kwa malipo na kutoa ada kwa huduma zinazotolewa na serikali katika nyumba hizo. Lakini vile vile serikali iweze kurekebisha mifumo ya maji na ukarabati wa miundombinu na ada hizo ziweze kusaidia katika kuboresha mahitaji haya.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa inaonekana kwa wananchi wengi kutokana na kipato chao kuwa hakitoshi kujenga nyumba za makaazi bora pamoja na kumudu gharama nyingine za maisha basi ni vyema serikali yetu ikahamasisha kuanzisha '*MORTGAGE BANKING'* ambapo itaweza kuwachukulia dhamana wananchi na kuwapokea kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zao hizo za makaazi.

Mhe. Naibu Spika, wakati huo huo kamati yangu inalishauri Shirika la Nyumba kutafuta aidha wabia au taasisi za kifedha kuweza kushirikiana nazo ili kuweza kuwawezesha wananchi kuweza kuwakopesha nyumba na kuwajengea nyumba kwa njia ya mkopo nafuu kama wanavyofanya wenzetu Tanzania Bara na nchi nyengine ikiwemo Ethiopia. Pia kuzijengea uwezo Taasisi za Umma na kuwakodisha au kuwauzia majengo ambayo yataweza kurejesha gharama kwa haraka. Lakini pia kutafuta makampuni ya nje ya nchi kuja kuwekeza katika sekta hii ya nyumba ili kuweza kuboresha makaazi yetu (*really assert*).

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inasikitika kwa kuona Bodi ya Shirika la Nyumba inashindwa kusimamia malipo ya nyumba kama sheria inavyoelezea na tunaitaka bodi hiyo kufanya kazi yake kama sheria inavyoeleza au Mwenyekiti na bodi yake waweze kujiuzulu mara moja.

**Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe**

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu imegundua kuwepo kwa ukosefu wa wataalamu katika fani ya usimamizi wa majengo ya kale (kihistoria) na kutokuwepo kwa ushirikishwaji wa wataalamu wa ndani pale inapotokea Miradi ya Ujenzi katika maeneo ya Mji Mkongwe na hayo ni miongoni mwa changamoto ziliopo katika mamlaka hii. Aidha, changamoto nyengine ni kuchelewa kwa ukarabati wa nyumba ya kihistoria ya *Beit El Jaib*. Kama ilivyoshauriwa na Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa Wizara ya Elimu hapo katika kipindi cha nyuma kuweza kulikarabati jengo hilo mapema wakati matokeo yake wizara ilidharau ushauri huo na kupelekea jengo hilo kuporomoka na kitia hasara kubwa serikali wakati jengo hilo ndio kivutio kikubwa cha utalii wanaokuja kuja kuangalia Mji Mkongwe hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kamati imebaini kwamba serikali kupitia baadhi ya miradi inayopangwa na inayofanyika ndani ya Hifadhi ya Mamlaka ya Mji Mkongwe huandaliwa bila ya kuishirikisha mamlaka hiyo na matokeo yake wakati wa kutaka kuitekeleza miradi hiyo inakua haikidhi vigezo na masharti ya Mji Mkongwe. Matokeo yake husababisha hasara na usumbufu mkubwa kwa wawekezaji kama ilivyo hivi sasa kwenye mradi wa Darajani '*Corridor'* pamoja na ule wa uendelezaji wa Hoteli ya Bwawani ambapo hivi sasa jengo la hoteli hiyo ya Bwawani limeshaaanza kubomolewa limetolewa madirisha na limebakia matundu matupu. Kutokana hali hiyo hatujui hatma ya ujenzi wa mradi wa Hoteli ya Bwawani labda Mhe Waziri akija hapa aje atwambie ni ipi hatma ya mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Bwawani. Kwani huko mitaani kumekua na taarifa ambazo hazina uhakika kuwa aliyepewa mradi huo kwa sasa hana nia tena ya kuendeleza mradi kama ilivyokuwa nia yake hapo

mwanzo. Kama hivyo ni kweli je ni hatua gani zitachukuliwa baada ya jengo lile kubomolewa na mradi bado haujaanza kufanyika.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli huu ni udhaifu mkubwa ambao umejitokeza ndani ya serikali yetu kuweza kufanya maamuzi ambayo ni kinyume cha sheria za masharti ya uhifadhi wa Mji Mkongwe. Kwa hiyo, kamati yangu inashauri kwa wizara zote kabla ya kuamua kufanya mipango ya matumizi ya katika maeneo ya Hifadhi ya Mji Mkongwe basi lazima kwanza ipelekwe kwenye Kamati ya Wataalamu wa Mamlaka ya Mji Mkongwe ili kutoa miongozo ya kisheria inayofaa. Kamati yangu inaiomba serikali pamoja na wizara husika kuwatumia ipasavyo wataalamu wetu hawa wa Mamlaka ya Mji Mkongwe wa ndani hususan pale inapotokezea miradi mikubwa ya ujenzi katika maeneno ya Hifadhi ya Mji Mkongwe ili kuepusha hasara kwa wawekezaji.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu vile vile inamtaka Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe kwenda kuzungumza na *UNESCO* ili kuweza kukwamua mpango wa ukarabati wa jengo la Beit El Ajaib ili kuweza kujengwa na watalii wetu waweze kuja kuangalia kivutio hicho cha kihistoria pamoja na kufanya tafiti zao. Kamati yangu inaishukuru Serikali ya Oman kwa kuwa hivi sasa wao wapo tayari kutoa fedha zote za kuweza kukarabati jengo hilo. Aidha, kamati yangu inawaomba wajumbe kuipongeza sana Serikali ya Oman kwa kuonyesha moyo huo wa udugu na imani kwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu pia inazitaka taasisi zote zinazomiliki majengo katika maeneo yote ya Mji Mkongwe kufuata ushauri wa kitaalamu kutoka Mamlaka ya Mji Mkongwe pamoja na kuitekeleza miongozo hiyo hasa katika ukarabati majengo yao ili kuweza kuepusha kupata hasara ya kuanguka kwa majengo hayo jambo ambalo linaweza kupelekea kupoteza rasilimali lakini vile vile pamoja na maisha ya watu.

**IDARA YA USAFIRI NA LESENI**

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa faida iliyopatikana wakati kamati yangu ikifanya kazi zake ni hatua za dharura na haraka iliyochukuliwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji za kuihami Ofisi ya Idara ya Usafiri na Leseni, pale Mwanakwerekwe baada ya kamati yangu kutembelea na kubaini mazingira mabaya ya kazi katika ofisi hiyo. Kamati yangu inampongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Mawasiliano na Usafirishaji mara tu baada ya kamati kupita na yeye alipita na kutoa karipio kali na alikwenda mwenyewe na kuzungumza na watendaji wake wa idara hiyo na tayari kamati yangu imeridhika na baadhi ya marekebisho ambayo wameyafanya. Na ninawaomba

Makatibu wengine waweze kuiga mfano wa Katibu Mkuu huyu. Kamati yangu haijaridhika kabisa na mazingira ya kazi na uchakavu wa mitambo ya Karakana zetu zilizokuwepo Unguja na Pemba iliyopo Tibirinzi, Pemba na Chumbuni Unguja ni miongoni mwa mambo yanayorejesha nyuma utendaji kazi wa idara hii. Kamati yangu inaitaka serikali kuanzisha Shirika la Karakana ya Serikali ili liweze kujiendesha kibiashara kwani kazi za kufanya zipo za kutosha na wataweza kuliendesha shirika hilo, pia kuboresha wasimamizi na utawala katika shirika hilo.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu katika hatua nyengine inaishauri wzara kupitia idara zake ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kwa vyombo vya moto vya barabarani pamoja na madereva, ili kuisaidia serikali kupunguza idadi ya ajali za barabarani. Kamati yangu pia inaiomba kufikiriwa kuanzisha utaratibu wa ulipaji wa faini za papo kwa papo kwa kulitumia Jeshi la Polisi kama wakala kwa kutekeleza suala hilo kama inavyofanyika kwa wenzetu Tanzania Bara.

Aidha, kamati yangu inaitaka serikali pamoja na wizara husika kupitia idara hii kuangalia uwezekano wa kukataza usafiri wa bodaboda ama kutoa leseni ya kuwatambua madereva wa bodaboda hizo kwani kumekua na mlolongo wa malalamiko kuhusiana na usafiri huo hivi sasa wakati wa usiku. Kwani hivi sasa kumeanzishwa usafiri huo kienyeji na hakuna sheria wala muongozo wowote uliotoka serikalini kuhusu suala hili, hili sio la kulifanyia mzaha hata kidogo kwani wajibu wa serikali ni kulinda usalama wa wananchi wake muda wote na popote pale walipo. Kamati yangu inaishauri serikali ikiwa usafiri huu utapata baraka za serikali basi wasajiliwe na wamiliki wa vyombo hivyo wajulikane na wao wawe ndio dhamana kwa lolote litakalotokezea wakati itakapotokezea tatizo katika usafiri huo. Pia kamati yangu inaitaka wizara kulitia lami eneo la ndani ya Karakana Kuu iliyopo Chumbuni kwani siku za mvua hujaa maji pale kwenye eneo ambalo gari hufanyiwa mazoezi wakati wa upasishaji magari.

**IDARA YA UENDELEZAJI NA UTUNZAJI WA BARABARA (UUB)**

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu pia inaipongeza Idara na Wizara kwa ujumla kutokana na juhudi kubwa za kuimarisha miundombinu ya barabara Unguja na Pemba. Kamati ilitembelea miradi mbali mbali ya barabara kuweza kushuhudia wafanyakazi wa UUB wakifanya kazi zao usiku na mchana na kuhakikisha kwamba miradi yao waliyoikusudia inakamilika.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu haijaridhika kwa kuona uchakavu mkubwa na uhaba wa zana za kufanyia kazi za idara hii na kupelekea idara kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi zake zaidi ya moja kwa wakati mmoja na kuwa na ugumu wa kukamilisha mradi husika kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaitaka serikali kuipatia vifaa vipya na vya kisasa idara hii ili kuweza kujenga barabara zetu katika kiwango kikubwa na kuweza kuishi muda mrefu, kwani kwa hivi sasa kwa kutumia zana chakavu walizonazo husababisha barabara wanazozijenga hivi sasa kupitia idara hii kukosa kiwango cha kimataifa kama inavyotakiwa. Hivyo, ni vyema idara hii ikipatiwa zana za kisasa Unguja na Pemba na sio kama ilivyozoeleka hivi sasa wakati mwingine vifaa kuhamishiwa Pemba na wakati Unguja kuna kazi zinakwama.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu pia inaitaka Bodi ya Mfuko wa Barabara kuacha urasimu usio na msingi wakati wa ujenzi wa barabara kwani husababisha ucheleweshaji kwa ukamilishaji wa ujenzi wa barabara kama ilivyopangwa na hivyo, kupelekea kazi nyengine kukawia kukamilika kwa wakati. Aidha, kamati yangu inaitaka idara hii kuwasiliana na Afisi ya Rais Ikulu ili kuweza kufuatilia ahadi zote za Mhe. Rais majimboni na kuzitekeleza ili kuondoa malalamiko ya muda mrefu kuhusu utekelezaji wa ahadi za Rais katika ukamilishaji wa barabara mbali mbali katika majimbo yetu ya Unguja na Pemba. Lakini vile vile kwa upande wa Pemba ahadi hizo zimekuwa zikitekelezwa kwa haraka sana tofauti na Unguja labda waziri akija aje kutuambia hii inasababishwa na nini, kwamba ahadi za Rais katika ukamilishaji wa ujenzi wa barabara Pemba zinatekelezwa kwa haraka kuliko zile za Unguja kuna tatizo gani.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia inaitaka idara iwasiliane na Manispaa na Halmashauri mbali mbali za Unguja na Pemba ili kuhakikisha kwamba suala la usafi wa barabara linakuwa endelevu. Pia barabara ya Fuoni iwekwe taa za barabarani pamoja kuweka watu maalumu kwa ajili ya kuifanyia usafi barabara hiyo, kwani miongoni mwa barabara zilizojengwa kwa kiwango bora na cha juu hapa Zanzibar imo hii barabara ya Fuoni, lakini cha kusikitisha hivi sasa barabara ile imeshaanza kuchakaa, kujaa michanga pembezoni na hakuna utaratibu wa usafishaji wa barabara hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu haijaridhika kabisa na ukiukwaji wa ukamilishwaji wa ujenzi wa barabara ya Wete–Chake Chake ambapo imo katika mpango wa mradi wa ujenzi wa barabara tatu za Pemba Wete–Chake Chake, Wete-Konde na Wete-Gando ambazo mbili tayari zimeshakamilika kwa

zaidi ya miaka tisa hivi sasa. Lakini bado ile ya Wete–Chake Chake haijakamilika hadi leo. Mwanzo tuliambiwa kuwa mkataba wake ulikuwa umeandikwa kwa kiarabu na bado ulikuwa haujatafsiriwa kwa zaidi ya miaka tisa. Kwa hivyo, kamati yangu imeambiwa hivi sasa wizara iko mbioni katika kuhakikisha kwamba mkataba huo unatafsiriwa kwa Kiingereza ili barabara hiyo iweze kukamilika.

Aidha, kamati yangu pia inaitaka serikali kupitia Idara ya UUB kuwalipa fidia wananchi walioko pembezoni mwa barabara hiyo ya Wete–Chake Chake ili waanze kuondosha majengo yao pamoja na vipando vyao, kwani fedha hizo karibu bilioni 1,700,000,000 tayari tulizitenga kwenye bajeti hii tuliyokuwa nayo hivi sasa na kuendelea kuchelewa kuwalipa fidia wananchi fedha hizo inapelekea kuongezeka kwa gharama za vifaa vya ujenzi huko baadae.

**SHIRIKA LA BANDARI, ZANZIBAR**

Mhe. Naibu Spika, wakati wa kazi za kamati, kamati ilibahatika kuzitembelea bandari zote zilizopo Unguja na Pemba. Aidha, licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika shirika hili, bado kumekuwa na changamoto zinazopelekea kutofikiwa kwa ufanisi wa malengo yanayokusudiwa na shirika hili. Miongoni mwa changamoto hizo ni ufinyu wa eneo la kuhifadhia makontena katika bandarini ya Malindi Zanzibar na Mkoani Pemba. Kamati yangu inaishauri Shirika la Bandari kuanza mara moja ya ujenzi wa *yard* ya kuekea makontena pale eneo la Maruhubi ambalo tayari shirika wameshapata hati, kwa sababu eneo la Bwawani hatuwezi kujua wakati wowote mwekezaji akitaka kulichukua tutakua hatuna eneo la kuekea makontena.

Mhe. Naibu Spika, Changamoto nyingine ni Madeni sugu kwa taasisi mbali mbali zikiwemo za Serikali pamoja na kuchelewa kwa malipo ya huduma zinazotolewa kwa baadhi ya Makampuni na Mashirika ya Meli yakiwemo Shirika la Meli la Zanzibar pamoja na *Azam Marine* na hiyo ni sehemu ya changamoto za shirika. Tunaiomba Shirika kuweza kufuatilia madeni hayo ili kuweza kupata fedha za uhakika. Pia, kumekuwa na malalamiko ya Ukosefu wa *X-ray Machine* pale bandarini kwa ajili ya upekuzi wa mizigo pale bandari pande zote za Unguja na Pemba. Suala hili tunaomba Shirika la Bandari kwa kushirikiana na *TRA* kuweza kuharakisha upatikanaji kwa mashine hizo hasa katika harakati sasa hivi za serikali zetu zote mbili kumbambane na uhalifu lakini vile vile pamoja na madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika**,** kuhusu ujenzi wa Bandari ya Wete Pemba tunapongeza wazo la serikali kushirikiana, kuwashirikisha wawekezaji binafsi katika kujenga bandari hiyo, lakini Kamati yangu inaitaka serikali kuhakikisha kwamba yeyote atakaetaka kuwekeza kwenye ujenzi huo lazima udhibiti wa matumizi ya bandari hiyo yasimamiwe na Shirika la Bandari na pia iwe huru kuweza kutumia bandari hiyo vyombo vyote pamoja na abiria kuweza kutumia bandari hiyo sio kuiachia Kampuni moja tu iweze kutumia bandari hiyo.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyingine ni ukosefu wa upatikanaji wa hati miliki ya maeneo mengi ya Shirika la Bandari, ikiwemo minara ambapo Shirika tayari limekwisha kufanya malipo ya kupimiwa maeneo hayo sasa kwa kuwa Mawaziri wote leo wapo hapa watuambie basi ni maeneo gani Waziri wa Ardhi yupo Waziri wa Mawasiliano yupo watwambie ni lini maeneo ya Shirika la Bandari yatakwenda kupimwa ili yaweze kupatiwa hati miliki.

**SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA, ZANZIBAR**

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Meli na Uwakala linakabiliwa na uchakavu mkubwa wa meli zake za MV. Maendeleo na MV. Ukombozi ambazo hivi sasa zina umri wa zaidi ya miaka 30 tangu ziliponunuliwa zikiwa mpya mwaka 1984. Kamati yangu imebaini kwamba hali hii inapelekea gharama kubwa za uendeshaji na kuweza kuzihudumia meli hizo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu wakati inatayarisha ripoti yake hii, ambayo mnayo Waheshimiwa Wajumbe, pia ilibahatika kutembelea kwenye Chelezo cha *African Marine* na *SECy7O* kule Mombasa, Kenya ambapo kwa miaka mingi Meli zetu za Serikali na za watu binafsi zimekua zikipelekwa huko kwa ajili ya matengenezo lakini vile vile kupata maelezo mengi kuhusu kazi zao lakini pia Meli zetu ambazo zinazopelekwa huko kwa ajili ya kutengenezwa na upakiaji wa mafuta.

Mhe. Naibu Spika**,** Kamati yangu inakuja na ushauri mwengine wa kuwa Meli yetu ya MV. Maendeleo kwa hivi sasa kwanza isiuzwe na ifanyiwe marekebisho makubwa ikiwemo kuwekw wa ” *Engine*” mpya pamoja na vifaa vyengine kwa sababu kwa maelezo ya wataalamu tulowapata katika Chelezo hicho ikiwa itafanyiwa matengenezo makubwa basi inao uwezo wa kuendelea kufanya kazi tena kwa miaka mingine zaidi 30, kwani inaweza kubeba abiria, pamoja na mizigo tani 600 ikilinganishwa na Meli yetu mpya ya MV. Mapinduzi II ambayo ni mpya lakini ina uwezo wa kubeba tani 200 tu.

Ambapo kwa hivi sasa meli ya MV. Maendeleo pamoja ni ukongwe lakini ndio inazalisha faida kubwa katika Shirika la Meli hapa Zanzibar kulinganishwa na hiyo meli ya Mapinduzi II.

**Mhe. Naibu Spika,** Katika ziara hiyo wataalam walitueleza kwamba walipelekewa wazo na Shirika kuhusu namna gani ifanyike ili Meli yetu ya MV. Mapinduzi II iweze kufanyakazi zake vizuri kwa kutoa huduma za kubeba abiria pamoja na biashara ikiwemo magari kwa upande wa bandari zetu za nguja, Pemba na Dar es Salaam.

Kamati yangu ilitaka kujua kama meli hiyo inaweza kufanyiwa marekebisho ili kuweza kufunga Gati na kuteremsha abiria, mizigo pamoja na magari wakati wote. Jawabu tuliyopewa ni kwamba jambo hilo haliwezekani labda yanunuliwe au yatengenezwe Ma-*Barge* au Matishali ya kuweza kuwekwa na kuteremshia magari halafu baadae yapelekwe kwenye bandari jambo ambalo kamati yetu imeona itagharimu gharama kubwa serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu pia inaishauri serikali kuwa imekusudia kununua meli nyingine mpya ya abiria na mizigo ambayo itaendana na mahitaji muhimu ya kutoa huduma za kibiashara pamoja na abiria. Ni vyema kuangalia uwezekano wa kununua meli ambayo itaweza kupakia na kufunga gati wakati wowote lakini pia itakayoweza kubeba na kuteremsha abiria pamoja na magari kwenye bandari zetu zote kama ilivyo meli ya *Sea Link 'One'* na *Sea Link 'Two'* ambapo inaweza kubeba abiria pamoja na magari katika bandari zetu zote za Tanzania.

**MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (*ZMA*)**

Mhe. Naibu Spika, wakati kamati yangu ikipokea taarifa ya Mamlaka hii imebaini kwamba pamoja na mafanikio makubwa iliyoyapata kuna changamoto kubwa imejitokeza katika usajili wa Meli za Kigeni ambazo zimesajiliwa hapa Zanzibar ambazo zinaipatoa mapato makubwa mamlaka hii, kupitia wakala wetu waliokuweko nje ya nchi. Kwa kuwa hadi hivi sasa Jamhuri ya Muungano Wa Tanzania haijaridhia Mkataba wa "*Panama Convention*" ambapo nchi wanachama wakisharidhia mkataba huo ndipo meli wanazosajiliwa na nchi zao ndio hupata vibali na ruhusa ya kupeperusha bendera na kuweza kuruhusiwa kufunga gati bandarini kote duniani. Sasa kwa kuwa Tanzania hadi hivi sasa haijaridhia mkataba huo, meli zote tunazozisajili kwa jina la Zanzibar hukosa vibali vya kuweza kufunga gati katika Bandari mbali mbali Duniani jambo ambalo kuna baadhi ya meli tayari zimeshaanza kujitoa katika mkataba na mamlaka yetu na meli za nje.

Tatizo jingine linalojitokeza kutokana na kutokuridhia mkataba huo na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa *Panama Convention* ni kwamba kuna vijana wetu wengi ambao wameshateremshwa kwenye meli mbali mbali duniani kwani Tanzania haijaridhia mkataba huo, ambapo karibu vijana 1800 hivi sasa wameshateremshwa kwenye meli na tayari wamesharudi nyumbani na hawana kazi za kufanya ambapo mzigo huo sasa unakuwa ni mzigo wa serikali kwamba vijana hawana ajira.

Mhe. Naibu Spika, pia kwa kuwa Zanzibar tumeanzisha Chuo cha Ubaharia na kina vifaa vya kisasa vya kutosha na tayari kimeshaanza kutoa mafunzo ya ubaharia hapa hapa Zanzibar, Chuo hiki ni ukombozi kwa vijana wetu wengi ambao wana ndoto za kuwa mabaharia hapo baadae na kuweza kufanya kazi kwenye Meli za Kimataifa, ambapo hivi sasa tayari wameshaanza kutoa mafunzo katika Chuo cha '*DANOUNCE'* na wengi tayari wameshaanza kupatiwa ajira za mbali mbali na mikataba ya meli mbali mbali Duniani. Katika chuo hicho kijana akifaulu vizuri chuo chenyewe kinamtafutia ajira baharia huyo katika meli mbali mbali duniani, wakati mmiliki wa chuo hicho ana mikataba na kampuni mbali mbali za meli duniani kuweza kuwapatia ajira vijana hawa. Pamoja na mafanikio hayo, chuo hicho kina changamoto ya kutotambuliwa kwa vyeti vyake hadi hapo *SUMATRA* itakapopeleka mkataba wa chuo hicho *IMO* ili uweze kuambatanishwa na ule wa *SUMATRA* na kuweza kutambuliwa duniani ili chuo chetu kiweze kuambulika. Kwa hiyo, katika suala hili, kamati yetu inaitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuzungumza na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuweza kupeleka mkataba huo *IMO* kiweze kutambulika chuo hicho duniani na vijana wetu waweze kutambuliwa vyeti vyao lakini vile vile waweze kupatiwa ajira mbali mbali duniani, ambapo mmiliki wa chuo hicho ametuahidi ana uwezo wa kuwapatia vijana ajira zaidi ya vijana 1000 kwa mwaka.

**MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE, ZANZIBAR**

Pamoja na maelezo yote yanayotolewa na serikali katika vipindi tofauti kuhusu kukamilika kwa jengo la *Terminal II* hapa Zanzibar, Kamati yangu bado inasikitika kuona bado hakuna maendeleo yoyote ya kukamilishwa mradi huo. Kwa kuwa serikali imeshatumia fedha nyingi sana za kujenga jengo hilo na kuangalia namna gani jengo hilo litaweza kutumika. Kamati yangu inaitaka serikali kuja kutoa kauli sahihi hapa Barazani ili kutwambia nini tatizo na serikali ina mpango gani wa kuewza kukamilisha jengo hilo la *Terminal II* hapo Amani Abeid Karume Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyingine inayotokana katika mamlaka hii ya Viwanja vya Ndege ni kukosekana kwa '*Transformer'* katika Kiwanja cha Ndege cha Pemba ambapo kwa hivi sasa kiwanja kinatumia '*Transormer'* ambayo inatumiwa na wananchi wengine jambo ambalo ni hatari na sio salama kwa watumiaji pamoja na ndege zinazotua katika uwanja huo.

Pia kuna changamoto nyengine katika mamlaka hiyo kukosekana kwa kifaa maalum cha kuongozea ndege (*ILS*) hasa wakati wa ukungu au wakati wa mvua kubwa kifaa hicho ambacho kinaweza kumsaidia rubani kuweza kutua bila ya usumbufu. Kifaa hichi ni muhimu kwani ni moja katika vigezo makampuni makubwa ya ndeege zinazotaka kuleta ndege zao hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, vile vile changamoto nyingine kwa mamlaka hiyo ya Viwanja vya Ndege ni kukosekana kwa *'X-ray Machine'* katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar ya kukagulia mizigo, jambo ambalo mashirika mengi ya ndege hayatui Zanzibar kwa sababu yanakosa kupakia mizigo ambapo bila ya *X-ray machine* kunakuwa hakuna usalama wa kuewza kuhakikisha kwamba mizigo hiyo iko salama. Kwa hiyo, tunaitaka serikali kuhakikisha kwamba inapatikana *X-ray machine* hiyo ili kuweza kuondoa usumbufu huo.

Mhe. Naibu Spika, ili kuondoa na kutokuwepo kwa changamoto hizo, Kamati yangu inaitaka serikali kuiachia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuweza kukusanya mapato yake kama yalivyo Mashirika mengine ili waweze kuyatumia na fedha nyengine za kuendesha kazi zao. Vile vile waweze kulipa gawio serikalini ili kuweza kuongeza ufanisi wa kazi zao. Kwani hivi sasa viwanja au viwanja vina mahitaji mengi na muhimu lakini vinashindwa kujitosheleza kwa wakati kwa sababu ya ukosefu wa fedha, ambapo tunaamini kama Mamlaka ingelikuwa na uwezo wake wenyewe wa kukusanya fedha na kuweza kutumia mambo haya mengi yangeweza kufanywa na wao wenyewe.

**IDARA YA MAWASILIANO**

Mhe. Naibu Spika, wakati wa Mkongo wa Taifa kwenye baadhi ya maeneo hasa katika ujenzi wa barabara yanarudisha nyuma uwezo wa kuendeleza Mkongo huo na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Kamati inaiomba serikali kuendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ili kuweza kuwa na uwezo mkubwa na wa kasi wa kubeba habari picha na habari *data* ili kufikia wananchi kwa maendeleo endelevu na dunia kwa ujumla. Kamati pia inaiomba serikali na wizara kwa ujumla kuwashirikisha wadau wote kabla ya kuanza

kutekeleza miradi inayojipangia hususan katika masuala mazima ya mawasiliano.

**KAMPUNI ZA SIMU ZA MIKONONI**

Mhe. Naibu Spika, wakati wa kazi za kamati, Kamati pia ilitembelea baadhi ya Mashirika na Makampuni ya Simu za Mikononi pamoja na Shirika la Posta la Zanzibar. Kamati imegundua kwamba, baadhi ya makampuni yanalalamikia urasimu mkubwa wa kupatiwa vibali vya ujenzi na utandikaji wa miundombinu yao ili kuweza kuwafikia wateja wao sehemu zote hapa nchini. Kamati inaomba Makampuni ya Simu kuunganishwa kwa haraka kwa Mkongo wa Taifa ili kupata njia mbadala ambayo itabeba mzigo mkubwa wa mawasiliano.

**SHIRIKA LA POSTA NA SIMU, ZANZIBAR**

Mhe. Naibu Spika, kamati pia ilipata fursa ya kulitembelea Shirika la Posta na Simu na kuweza kubaini muingiliano wa matumizi ya sheria za Zanzibar na za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mfano, Sheria ya Uvuvi wa Baharini na ile Sheria ya Uuzaji wa Baadhi ya Mazao ya Bahari ambapo Sheria ya Zanzibar inaruhusu usafirishaji wa majongoo ya baharini wakati ile ya Jamhuri ya Muungano hairuhusu usafirishaji wa majongoo hayo.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na changamoto hiyo, imekuwa kuna matatizo makubwa ya kutotambulika kwa baadhi ya vibali vya taasisi za Zanzibar wakati wa mizigo ambayo inapelekwa kupitia njia ya posta ikifika kule Tanzania Bara vibali vile vya Zanzibar vinakuwa havikubaliki kutokana na sababu hizo za mgongano wa kisheria. Vile vile husababisha mizigo ya Zanzibar kuzuiliwa inapofika uwanja wa ndege wa Dar es Salaam na wakidai watendaji wa taasisi za Zanzibar na Bara kuwa Zanzibar haitambuliki kimataifa na kutaka vibali hivyo kuchukuliwa katika taasisi ziliopo Tanzania Bara jambo ambalo kinyume cha utaratibu kwa sababu taasisi hizo sio za Muungano.

Kamati inaiomba serikali ifanye juhudi za kuhakikisha kwamba inaweka utaratibu wa kutatua kero ya kutotambulika kwa vibali vinavyotolewa na Taasisi za Zanzibar kwa wakuu wa taasisi hizo ambazo si za Muungano pamoja na kuweka utaratibu unaoeleweka ili wananchi waweze kupata huduma za kiposta bila ya kuwa na usumbuvu wowote.

**HITIMISHO**

Mhe. Naibu Spika, kabla sijakamilisha Muhtasari wa Ripoti hii ya Kamati ya Mawasilino na Ujenzi naomba niendelee kuwashukuru watendaji wote wa wizara zetu zote mbili ikiwemo Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kupitia kwa Mhe. Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wake. Lakini vile vile Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kupitia Waiziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wao wote kwa mashirikiano yao makubwa waliyoweza kutupatia wakati wote tukiwa katiak shughuli zetu. Vile vile upatikanaji wa fedha za *OC* pamoja na vitendea kazi na usafiri pamoja na malipo ya ziada ya *overtime* ambavyo vimekuwa vikirejesha nyuma shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache sasa nitaomba niwataje Wajumbe wangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ambao ndio walionipa nguvu za kuweza kusimama hapa kwa niaba yao nikaweza kuwasilisha ripoti hii.

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Suleiman Sarhan Said - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Ali Kombo - Mjumbe
4. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Mjumbe
5. Mhe. Khadija Omar Kibano - Mjumbe
6. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali - Mjumbe
7. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe
8. Mhe. Nassor Salim Ali - Mjumbe
9. Mhe. Said Omar Said - Mjumbe

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa naendelea tena kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa niaba ya Spika kwa kuweza kuikabidhi kamati yako hii kusimamia wizara zetu hizi zote mbili na tunakuahidi kwamba mashirikiano tuliyoyapata katika wizara hii tunaendelea kuyaimarisha siku za mbele.

Lakini la mwisho kabisa hili ni langu mwenyewe. Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Shaurimoyo...

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mwenyekiti ripoti yako kwanza imevunja rikodi, imechukua muda mrefu sana.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Dakika moja tu.

**Mhe. Naibu Spika:** Nisikilize basi Mheshimiwa na mimi, wewe umesoma nimekuachia na mimi nisikilize. Umechukua muda sasa nakuomba nikupe dakika tano tu, utumie umalize hayo ambayo unataka kuyazungmza kwa sababu na wajumbe na wao wanataka kuchangia. Ahsante nimekuruhusu Mheshimiwa.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Mhe. Naibu Spika, nakuahidi sitotumia dakika tano kwa sababu ripoti yangu nimeisoma kwa muda mrefu. Kwanza natoa shukurani za dhati kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuja kusimama mbele yao. Nawaahidi kuendelea kutoa mashirikiano makubwa kwenye jimbo langu na ninaamini si muda mrefu haya mambo mengi ambayo tuliyoyazungumza kwenye kamati, hasa changamoto za barabara zetu katika jimbo letu la Shaurimoyo, tunaamini Mhe. Waziri ananisikia ataweza kuzitekeleza. Lakini vile vile Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yupo kuna ahadi ya Mhe. Rais katika jimbo la Shaurimoyo ya ukamilishaji wa barabara yetu ile, tunaamini salamu zetu hizi ataweza kutufikishia.

La mwisho kabisa naomba kutoa shukurani kwa ofisi yako ya Spika kwa kuweza kunishirikisha katika ziara ya Mhe. Spika nchini Iran ambapo tulipata mualiko wa Mhe. Spika wa Iran. Kwa kweli tumepokelewa vizuri heshima tuliyoipata tulipokuwa Iran na heshima aliyopewa Mhe. Spika kwa kweli sijapata kuiona. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Naibu Spika, ofisi yako hii iweze kuwapa fursa nyingi Waheshimiwa Wajumbe wasafiri na Mhe. Spika ili waone huduma za Mhe. Spika anavyohudumiwa na Spika anavyotakiwa awe. Naamini yale ambayo niliyojifunza mimi naamini na wajumbe wenzangu wakiweza kuyapata basi tutaweza kuboresha sana masuala mazima ya utawala wa Baraza na kwa sababu bila ya kuwa na utawala wa Baraza hayo yote ambayo tunayoyasema kuweza kupatikana kwa kweli itakuwa ni changamoto.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru katika ziara ile tumeweza kupata mashirikiano makubwa na naomba ofisi yako kama tulivyopewa huduma na ofisi ya Spika wa Iran basi na nyinyi ofisi yetu muweze kumualika Spika wa Iran ili waje tuweze kushirikiana nao. Kwa sababu kwa muda mfupi tuliokaanao tumehisi kuna baadhi ya mambo mengi ambayo ofisi yetu na ofisi ya Spika wa Iran tukaweza kushirikiana kuna mambo makubwa mengi ambayo tunaweza kusaidiwa. Kwa sababu wenzetu wana teknolojia kubwa ya kisasa lakini vile vile wana uwezo ambao tunaweza kufaidika na msaada wao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache naomba kukushukuru. Naomba kutoa hoja ahsante.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa ripoti yako uliyoitoa. Waheshimiwa Wajumbe sasa tunakaribia kuanza michango na nilikuwa nina ombi kwenu. Kwa sababu ya muda tulionao na muda ambao kanuni inatutaka tuutumie kwa kila mmoja wetu hautatosha kutuwezesha wengi wetu kupata muda wa kuchangia. Mpaka sasa hivi nina wachangiaji 25 na mnaelewa kwamba ripoti hii inabidi tuimalize leo. Sasa ningewaomba sana mkubaliane na mimi nitamwita Mwanasheria Mkuu tutengue kanuni ya muda wa dakika 15 na badala yake tutumie dakika 10 ili angalau kila mmoja wetu apate nafasi ya kuchangia.

Baada ya kusema hivyo ningemuoma Mwanasheria Mkuu atutengulie kanuni ya dakika kwa ajili ya kuweza kuendelea.

**Muongozo**

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa ruhusa yako. Kutokana na umuhimu wa ripoti hii na jinsi gani inavyowagusa wananchi wetu na imebeba mambo mengi, na hasa jinsi mwenyekiti alivyoyazungumza leo na yale ambayo yanatukabili sisi kesho, ambayo kwenye orodha ya kazi zetu za shughuli za Baraza kwa wiki ambayo ratiba yetu imetupa kuna hoja binafsi ya Mhe. Mohamed Said Mohamed. Sasa nilikuwa nakuomba labda kama utazingatia hayo na ripoti hii ili muda wetu ambao Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tupate muda muwafaka, kwa sababu wiki nzima tumekuwa tunakwenda sasa hivi *marathon*. Jana ripoti muhimu ya *PAC* tumepata dakika 10, 10 haitoshi kabisa. Sasa mimi naomba sana Mheshimiwa tuzingatie baina ya leo na kesho na ikibidi kama mara moja uliwahi kusema hapa zege isilale, basi hata kama kuondoka saa sita za usiku kwa niaba ya wananchi wetu sisi tuko tayari.*(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika,** Mhe. Mjumbe unajua tatizo lililokuwepo labda nyinyi wenyewe au baadhi yenu hamlielewi hilo, napojaribu kuchangia wengi wenu mnayarudia hayo kwa hayo. Wezetu Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wana ripoti kubwa sana, ripoti mbili au tatu zinajadiliwa kwa siku moja kwa muda huu huu ambao tunautumia sisi. Lakini sasa sisi tumekuwa wengi wana utashi wa kutaka kumaliza kila kitu, lazima yeye azungumzie kila kitu na wengine wapate nafasi wazungumze. Hilo ndio tatizo.

Kuna baadhi wanataka kila kitu wakizungumze wao, chukua *point* zako mbili au tatu uzizungumze ambazo wewe ambazo unazihisi ni muhimu nyengine waanchieni wengine hapa yote unayoyafahamu wewe kama unaona wewe muda wako haukutoshi mwambie mwenzio kile kitu ambacho unahisi wewe anaweza kukisema muda kama haukutoshi.

Lakini haiwezekani hivi tukaendelea kila mmoja akachangia kwa dakika 15 ratiba yetu haisemi hivyo. Sisi tunakwenda kwa ratiba na mnatupa shida sisi na nyinyi mnafahamu sina haja kuelezea kwanini tunakuwa na ratiba tuna siku maalum ya kufanya shughuli zetu za Baraza hatuwezi kuongeza siku na hayo ambayo unayasema wewe kwamba hoja binafsi zina umuhimu wake vile vile.

Kwa hiyo, mimi ningemuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu atengue kanuni tuone tupige kura. Tupige kura na naomba sana Waheshimiwa mshaanza kugeuka kutizama kuwatisha wengine hapana, kila mtu apige kura kwa kujiamini naomba sana. Dakika kumi zinatutosha naomba kila mtu apige kura kwa kujiamini. Ahsante Mhe. Mwanasheria Mkuu.(*Makofi*)

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa maelezo ambayo umeyatoa na kama ambavyo umeniomba nisimame ili niweze kutenga kando kanuni ya muda ya kusema na kuchangia ambayo ni kanuni ya 58 fasili ya 6 ambayo ndio inaongoza muda wa kusema na kuchangia ndani ya Baraza.

Mhe. Naibu Spika, kanuni 58 fasili ya 6 inatoa dakika 15 kwa kila Mjumbe kuchangia na kusema ndani ya mijadala ya kawaida na kama ulivyosema wachangiaji wako wengi na tunataka fursa kutoa kwa kila Mjumbe ambaye ameleta jina lake kuchangia.

Hivyo, kwa heshima naomba kutoa hoja ya kutenga kando kanuni ya 58 fasili 6 ili Baraza likubaliane na hoja ya kutenga kando muda wa kusema na kuchangia baada ya dakika 15 iwe ni dakika 10. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba kuwauliza, wale wanaokubaliana na hoja wanyoshe mikono mmeona wenyewe eenh! wale waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa karibu.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu kuwa mchangiaji wa mwanzo baada ya Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nitazitumia kwa heshima kabisa dakika zako kumi ili na wenzangu wapate taratibu za kuchangia kama tulivyojipangia.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa kamati hii yeye na Wajumbe wote pamoja na Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu wetu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa wizara hizi kwa kazi nzuri waliofanya na taarifa hii iliyokuja ambayo ina changamoto ambazo zinataka kufanyiwa kazi juu ya kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nitazungumzia kwa ufupi kabisa mambo mawili katika Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ili baadae niende katika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Kwanza, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi zake nzuri pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu wa Wizara, Naibu Katibu Mkuu na wengineo. Kubwa ninalotaka kulisema hapa tunalolizungumza hapa Mheshimiwa kwa maslahi ya wananchi wetu na kuwaondolea kero katika maeneo yetu. Wizara hii ndio wizara mama naweza kusema kwa huduma za jamii katika nchi yetu bila ya maji huwezi kuishi. Lakini halkadhalika maji hayapatikani bila ya umeme.

Kwa hivyo, taasisi hizi mbili nazipongeza kwa kuhakikisha kwamba mambo mawili yanapatikana yanakwenda sambamba. Kwa mfano juzi palipotokea mdharba umeme ulikatika sehemu za Tomondo Uzi baada ya kukatika umeme ule maji yalipotea yakawa hayapatikani. Lakini kwa ujasiri wao Shirika la Umeme nawapongeza kwa dhati kabisa kwa juhudi zao za dhati wanazozifanya usiku na mchana bila ya kuchoka, wenzetu hawa mimi nilipiga simu kama saa 3 sa usiku tunatoka Barazani hapa alfajiri walifika kwa sababu usiku ulikuwa hauendeki na kuna sehemu kadhaa ambazo Taveta na kwengineko ulikatika umeme waliweza kuurejesha wakati huo huo usiku. Lakini kutokana na bahati mbaya walipofika Tomondo kulitokea na mzozano kidogo wenye minazi sijui hawataki ikatwe na nini lakini namshukuru Mkuu wa Mkoa na kupitia na hao *ZECO* kazi imekwenda vizuri na umeme umerudi ule bila ya matatizo.

Kwa hivyo, nawapongeza Shirika la Umeme pindi linapotokea tatizo hata saa saba za usiku ukiwapigia simu wanatekeleza kazi zao. Naomba hili Mheshimiwa mimi tabia yangu moja tu "nitasema kweli daima fitina kwangu mwiko". Mamlaka ya maji Mheshimiwa naomba wafate mambo kama haya ya Shirika la Umeme.

Maji tunayategemea ni kitu cha mwanzo kwa binaadamu lakini yanapokuwa hayapo basi pale unapopata ufumbuzi kuna hili tulifanye ili tupate maji kidogo huonekana kama kuna mzungumko. Mimi niwaombe sana Mamlaka ya Maji wawe na jitihada kama Shirika la Umeme wende sambamba. Kwa hivyo, niseme nampongeza waziri hili la makusudi.

Mamlaka ya Maji wasinielewe vibaya Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kijito Upele kwa sababu mimi kazi yangu kufatilia matatizo ya wananchi wangu sio wananchi wa Jimbo la Kijito Upele hata kwengineko ninapohisi kuna matatizo ya maji nina haki ya kuwaambia kwa usalama bila ya kuleta hapa kwenye Baraza. Kijito Upele kuna kituo kikubwa cha maji ambacho alikichimba sasa hivi Mbunge Mhe. Shamsi Vuai Nahodha kupitia na Mbunge wake wakati ule alikuwa Mhe. Juma Sereweji, maji yale yalinufaisha sana sehemu ya Pangawe kote yaani kutoka Taveta, Melinne Uzi na kwengineko watu walikuwa wanafaidika.

Bahati mbaya Mhe. Naibu Spika, lilitokea tatizo magari yote baada ya kwenda Msikiti Mabuluu yakahamia pale maji yakawa hayapatikani kabisa mimi nikatoa wazo mara moja mbili tatu bado. Lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri tulitoka hapa nikamwambia tunakwenda usiku kuangalia hapa pahala maji yanachukuliwa mpaka usiku wakiondoka hawayapeleki sehemu ya Melinne Uzi au Taveta na tuliyakuta magari.

Lakini nampongeza kwa ujasiri wake akasema leo hebu maji haya yafungwe msichukuwe tena maji hebu nendeni Msikiti Mabuluu kuanzia siku hiyo Mheshimiwa namshukuru Mwenyezi Mungu watu wale wote wanapata maji katika maeneo hayo, wanapata maji asubuhi mchana na jioni. Lakini natoa taarifa sio yakazuiliwe tena yale maji, maji wanayapata bila ya matatizo.

Kwa hivyo, nawashukuru ZAWA kwa kuruhusu yale maji kwenda kule na mimi naiomba Bodi ya Mmamlaka ya Maji wasifikirie nimeyazuia Shihata sina uwezo huo uweza wangu mimi kama Mwakilishi kutoa rai ili wananchi wetu wengi wafaidike kule kwenye biashara ya magari maji yanapatikana Mheshimiwa Waziri hongera wewe Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na watendaji wake.

Lakini naomba suala moja kubwa ili kuondoa tatizo ni vyema katika majimbo yetu tukapata mtu maalum wa kudumu linapotokea tatizo katika jimbo tumjue tunamuendea nani kwa sababu Mkurugenzi yuko afisini watendaji wengine hawana nafasi. Namuomba sana Mhe. Waziri tuwe na mtu maalum sio kwa jimbo langu mimi hata majimbo mengine au kuwe na *zone* maalum, likitokea

Jimbo la Kijito Upeke kuna matatizo namkamata fundi fulani twende waturuhusu hilo maji yana matatizo.

Lakini hili jengine nitalisema kwa ufupi Mhe. Naibu Spika, baada ya haya na nina visima kama vinne katika Jimbo la Kijito Upele *Ras Al-Khaimah* visima viwili na vyenvginevyo Mbunge na Mwakilishi Mheshimiwa Shihata na Mbunge Shamsi tumevichimba kusaidia Mamlaka yetu haya ya Maji. Kisima cha Magirisi kipo kikubwa sana kama tutapatiwa *pump* leo na ukavutwa umeme tu basi tatizo la maji katika Jimbo letu upande wa Tomondo upande wa Kijito Upele, upande wa Kwarara yataondoka.

Naiomba Mamlaka ya Maji kupitia wizara tuwe tufanye ziara mimi na wao niko tayari tukimaliza Baraza wakati wowote twende tukaangalie hayo mazingira na mimi na Mbunge tutachangia huduma nyengine nzito ili kuhakikisha kwamba maji tunayapata wananchi wetu kuwaondolea shida. Lakini kisima cha Kwarara kizuri, Kijito Upele kipo kisima vile vile haya yote kuondoa tatizo kama kutafanyiwa kazi najua sasa hivi bado lakini tutakwenda mbio.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nakuja Wizara ya Ujenzi nimshukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu wake pamoja na watendaji wa *UUB* kwa kazi nzuri ambayo wanasimamia na wanaifanya inaonekana. Mhe. Naibu Spika, tulililia sana barabara hii ya Kwarara hii mpaka Skuli mpya Kwarara. Lakini namshukuru Katibu Mkuu alikuwa hakai Naibu Waziri hakai, Naibu Katibu Mkuu hakai, Mkurugenzi na watendaji wake wote walikuwa bega kwa bega tunafanya kazi pamoja.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru barabara imepatikana watu wanafurahia hilo suala. Kwa hivyo, naowambea vile vitendea kazi vichakavu na mambo mengineyo serikali ifanye bidii iwapatie wenzetu wanafanya kazi nzuri na ukizungatia kwamba kama watapata vifaa basi *UUB* wanafanyakazi nzuri hasa kuliko hizo taasisi nyengine za nje. Tuwape uwezo wafanyekazi zao na zinaonekana kazi. Kwa mfano sasa hivi wanamaliza barabara ya Cheju huko kunakolimwa mpunga wanakwenda vizuri, kwa hivyo, tuwasaidie sana.

Jengine Shirika la Bandari nawaapongeza Mheshimiwa wanafanyakazi nzuri na wanaendelea na jitihida zao *Alhamdulillah* pamoja na mazungumzo ya hapa na pale lakini bado tuwasaidie katika changamoto zao ili wapate nafasi nzuri ya kutekeleza.

Jengine ni Shirika la Meli na Uwakala halkladhalika nawapongeza ndugu yangu Mkurugenzi Salum nae anakwenda vizuri lakini pia tumpe uwezo wa kupatikana meli mpya azidishe kazi zake kwa juhudi ya maendeleo ya nchi yetu.

Jengine Idara ya Usafiri wa Leseni. Mhe. Naibu Spika, limezungumzwa neno moja nataka kuliweka sawa kidogo. Idara ya Usafiri na leseni wanafanya kazi nzuri mimi nashukuru *route* yangu ilikuwa kutoka Kwarara mpaka njia nne sasa inafika skuli mpaka Madina wameruhusu iende. Kwa hivyo, wananchi ambao waliokuwa hawajapata usafiri karibu miaka 40 au mingapi sasa hivi wanapata usafiri. Kwa hivyo, mimi nawapongeza kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Lakini suala Boda boda lilizungumzwa Mheshimiwa, mimi naiomba serikali ikae kupitia vyombo vinavyohusika wawafikirie hawa vijana kama wako kwelini kufanyakazi kwa kuwasaidia wananchi utafutwe utaratibu mzuri wajulikane kazi zao wathibitishwe pawe na picha zao na usalama wao ueleweke.

Lakini Mheshimiwa nasema tu kwamba vijana wanasaidia watu maana tusiseme tuko mjini wengine huko daladala haziendi. Kwa hivyo, wanasaidia na hivi kule mimi kule siwatetei kwa ubaya nawatetea kwa kusaidia watu. Mimi ninao katika Jimbo langu la Kijito Upele wanakaa pale msikitini njia ya Kwarara wanasaidia watu sijapata lalamiko kama kamnyanganya mtu au kafanya nini. Nawaomba sana watafute utaratibu unaofaa ili kuwasaidia wananchi wetu.

La mwisho kabla hujanipigia kengele Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mhe. Naibu Spika, mimi nawashukuru wenzetu wanafanya kazi zao nzuri. Lakini unajua kama ukiwa kiongozi wananchi kama wana matatizo watasema na pa kusema na mimi pa kutolea maelezo hapa na wenyewe watakuwa wanasikia sikusema pengine pempeni. Kuna utaratibu wa wafanyakazi wanafanyakazi *shift* ya asubuhi mchana na usiku. Lakini usafiri ni jambo la mwazo ambao nalitegemea, kwa hiyo kuna utaratibu wa kukodiwa mabasi. Lakini kuna malalamiko kwa baadhi ya wafanyakazi mfano wakaaa Bububu wanakaa Mfenesini basi linakwenda lakini wakati mwengine huwa .....

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa umebakiza dakika mbili.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante Mheshimiwa huwa hawafiki kule kunakohusika wanaweza kufika *Amani round about* wakawateremsha

wakasema madhali watu wawili chukuweni daladala nendeni zenuni huo si utaratibu.

Naomba sana Mamlaka ya Uwanja ya Uwanja wa Ndege wawaangalie hawa madereva wanaokodi katika mabasi yao kuwapeleka wafanyakazi wao kwa sababu wafanyakazi wanalalamika huduma ambayo waipate wanaikosa.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi baada ya hayo machache naiomba serikali iwape nyenzo wenzetu hawa, iwape kila, uwezo wafanye kazi zao kwa maslahi ya pato la nchi yetu na kufaidika wananchi wetu katika maeneo yetu ya Majimbo. Nashukuru Mhe. Naibu Spika, naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi kuchangia Ripoti ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakikishi.

Kwanza niwashukuru sana wenye kamati hii pamoja na kuwatuwasilishia ripoti ambayo inaonesha Mwenyekiti, alikaa pake yake bila kushirikiana na wenziwe maana yake mengi aliotueleza pale hayakuwemo kwenye kitabu hichi alikuwa na kurasa zaidi ya thalathini naa huku kuna ishirini naa mwenzetu kapiga mbele zaidi. Kwa hiyo, inaonesha namna umahiri wake peke yake anaweza akafanya kazi. Wakati nayasema hayo Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja maana kila siku muda unazidi kubanwa tu kila siku ukacha itafika *time* tutachangia dakika tano humu ni vizuri.

Niende kwenye Sekta ya Ardhi, Sekta ya Ardhi ukurasa wa 4 pamoja na kauli za Mhe. Waziri kufuta ardhi imesomwa pale ripoti kuna maeneo mengine sana ambayo makubwa yamezungushiwa makuta *East coast* na *West coast* nafikiri yale Mhe. Waziri angefanya haraka iwezekanavyo hiyo kauli basi angetekeleza kwa yale bila ya kuogopa wala kuwa na ghofu kuliko kutoa kauli ile kujenga ghofu kwa Wazanzibari au wananchi wakwezi na wakulima wa nchi hii kwenye kitapo cha chini.

Maeneo mengi yenye makuta na yenye mlimbikano wa ardhi ni sehemu za pwani ambapo watu wetu waliokuwa wanakwenda kubarizi kule kupata upepo, sasa hivi hawapati kwa sababu makuta yale ambayo yamefika miaka kumi, kumi na mbili, miaka minane watu wametegeza pesa ili mtu anapata pesa kuta lile anakuja kuliuza wakati serikali imetoa kwa pesa ya chini. Basi nafasi ile Mhe. Waziri angeitumia zaidi kuyafuta yale makuta haraka iwezekanavyo na sisi tungekuwa pamoja naye moja kwa moja.

Lakini kwa kauli aliyosema kwamba kufuta viwanja ambavyo vya wakwezi na wakulima viwanja vya Mombasa, Mpendae kweli hivyo hawatendi haki au hawatendei haki wananchi wetu, ingekuwa kufuta Mhe. Waziri angefuta yale makuta kwanza kuanzia Pongwe yamejaa makuta kule zaidi ya meli tatu, meli nne mtu ana kuta tu kalipiga kuta zaidi ya miaka kumi limekaa halina chochote, watu wanataka kuja kuekeza wakosa nafasi zile watu wamezikamata nini lengo lake.

Kwa hivyo, atakapokuja kufanya majumuisho yake Mhe. Waziri atwambie nini tatizo ya yale makuta na nafikiri mtu anapopewa kiwanja au kibali anapewa na muda wa kuendeleza sio kupiga ukuta kuendeleza kwa ule mradi aliouombea miradi imeombewa lakini mpaka leo yamekaa tu pale yamekaa yanatega maslahi mbele.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Mamlaka ya Maji pamoja na manufaa waliokuwa nayo kupatiwa maji wananchi wale. Lakini bado kuna malalamiko wote humu Wawakilishi ni mashahidi kwamba kulalamikia kwa upatikanaji wa maji wa nchi hii umekuwa tatizo, katika vitabu kuna asilimia 87 mjini na siku zote mimi napingana nayo na hii nitapingana nayo mpaka nitatoka katika Baraza la Wawakilishi sikubali kwamba upatikanaji wa maji mjini ni asilimia 87 kwenye maandishi yako hivyo lakini uhalisia haujafika hata asilimia 50. Sijui ina maana gani kutwambia au ndio miundo mbinu ya maji yanayozalishwa hatutaki miundombinu tunataka maji yafikwe kwa walengwa kama sithubutu ya Waheshimiwa Wawakilishi kuchimba visima vyao kuwasaidia watu basi nafikiri Unguja hii ingenuka kwa uchafu maji ni tatizo sugu, maji tatizo na sisi Wawakilishi tunapata hivyo vipesa vya maendeleo vyote asilimia 90 tunakimbiza katika huduma za maji.

Hakuna huduma yoyote mtu akizipata basi anafikiria akanchimbe kisima, nikawasaidie watu maji kulikoni na miradi mingi sana ya maendeleo basi ipo katika Idara ya Maji, kuna mradi ya *JAICA* Japan umetengenezwa kule Welezo mpaka leo hakuna, usambazaji wa maji mjini hivi sasa kuna pesa dola milioni tisini na mbili hizo vile vile maji lakini maji bado imekuwa ni tatizo. Lakini maji hayo hayo ikiwa kesho Waziri au Rais anakwenda sehemu husika sehemu isiyotoka maji zaidi ya miaka miwili siku hiyo maji yanatoka kulikoni.

Nafikiri kunatakiwa dhamira maalum Mhe. Waziri na watu wa Idara ya Maji watwambie tatizo nini si hilo tu imefika *time* hata miundombinu ya maji yenyewe iko katika mitaro ya maji machafu, mimi mwenyewe katika ujenzi wa mtaro wa Kijangwani nilifika kumwambia Mkurugenzi kwamba pale pana bomba la *Asbestos* na pana kiungio na ndani ya kiungio pana chemba ya maji

machafu mtakuja kutuulia watu wetu bure na maji yale yanatumika kwa wananchi wa Kwahani na Miembeni nimekwenda kupeleka lalamiko hilo lakini sikusikilizwa imekuwa kama mtu uliyepiga muziki tu mtu kacheza baada ya kucheza kaondoka. Nakuomba sana Mhe. Waziri hili suala ulichukuwe, kuna kiungo kwenye chemba ya maji machafu ni hatari kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala la Shirika la Umeme. Pamoja na masuala mazuri sana wanayotusaidia kutung'arishia nchi yetu, lakini bado malalamiko yapo. Ni shahidi kwako mheshimiwa nilishakuambia kwa muda mrefu sana. Mimi kilio changu kwenye Shirika la Umeme ipo katika miundombinu yetu. Viwanja vya Mnazi Mmoja ni viwanja vya mpira, kuna nguzo zaidi ya miaka miwili na nusu zimekaa pale zinafanya nini zile nguzo. Hapo nyuma zilikuwa nguzo zile zinawekwa kwa ajili ya shughuli ya skukuu, ikimalizika skukuu zinang'olewa, lakini leo hii zaidi ya miaka miwili na nusu nguzo zile zipo katika viwanja vile, ni hatari kwa vijana wetu, vile viwanja kazi yake ni kuchezea mpira. Au labda tuambiwe kwamba zimebadilishwa badala ya kuchezwa mpira wa miguu sasa hivi unachezewa *racked* tutakubaliana, lakini zile nguzo pale sio pahala pale, suala hili nitasema na nitaendelea kusema.

Mhe. Naibu Spika, nilifika mpaka Shirika la Umeme, na waziri wa habari kwenda kumlalamikia nguzo zile. Kwa bahati nzuri mmeondosha nguzo moja tu katikati ya uwanja wa *black fighter* nguzo nyengine mmeziacha, kulikoni, nani aseme. Tunasema kwamba zile nguzo sio mahala pake, ifike wakati zile nguzo pale ziondoshwe, mkakunje waya wenu muondoshe nguzo zenu, wakati viwanja vinataka kutumika mwende mkachomeka kwa sababu hiyo ndio kazi ya Shirika la Umeme kusambaza umeme, lakini leo hii zile nguzo zimekaa zaidi ya miaka mitano, zaidi ya miaka miwili na nuzu. Kwa kweli hamtutendei haki, tunaosema mnatuchukua, lakini mwisho wa siku itabidi zile nguzo pale sio mahala pale ziondoke.

Nakwenda kwenye suala jengine kuhusu nguzo hizo hizo. Mimi kwa bahati nzuri Shirika la Umeme kidogo nalitembelea kidogo nalijua. Kuna malalamiko mbali ya kufanyakazi tu, hata kuna taasisi nyengine. Hapa nitaomba Mhe. Naibu Spika, nikukabidhi vidhibiti vyangu, nina risiti ambayo wamepokea zaidi milioni 26, 800,000/- kwa uchimbaji wa mashimo, sijui mashimo haya miezi mingapi au muda gani, ninayo moja hii na nyengine ninayo hapa ya kulipana mishahara hewa ambayo watu hawajafika viwango vya elimu ile, lakini watu wanalipana mishahara ambayo haiko sawa shirika la umeme.

Mhe. Naibu Spika, tukumbuke Baraza hili hili liliwahi kumzungumza huko nyuma Katibu Mkuu wa wizara moja na akafika kuwajibishwa kwa kumlipa mshahara mtu ambaye sio kiwango chake, hivi vyote nitakuomba Mhe. Naibu Spika, uvichukuwe hivi vielelezo niko tayari kuvizungumza ninavyo mkononi, tatazo liko wapi. Haiwezekani kwamba baadhi ya watu wafanye mashirika mali yao. Hapa ndio ukweli tunajenga nchi yetu

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, inaletwa kwa katibu halafu baadae ndio unapewa wewe mheshimiwa.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Sawa Mhe. Naibu Spika. Naomba uipokee na naomba kazi ifanyike katika hilo. Sitokuwa tayari kwamba baadhi ya watu wawe mabwana katika nchi hii.

Nikiendelea mbele nakwenda katika *UUB*. Niipongeze sana *UUB*, pamoja na kufanyakazi ya utengenezaji wa barabara zetu vizuri. Lakini masikitiko yangu barabara zile haziendi katika makusudio yaliyokusudiwa. Nitatoa mfano wa barabara ya Uwanja wa Amani nyuma. Barabara ile unapofika muda wa saa moja tu au saa 12:00 inakuwa *parking* za magari, watu wanashuka upande huu wa pili wa barabara sio lengo, watu watumie barabara ile kuingilia Uwanja wa Amani na kutoka. Kama Mhe. Naibu Waziri hujui hilo suala basi hata leo kaangalie sio mahala pake. Zile barabara zimejengwa kwa ajili ya kutumia watu kupita na magari yao sio kulaza magari yao. Nitakuomba sana Mhe. Naibu Waziri, nikotayari kwenda na wewe hata muda huu kwamba utakuta kweli pale pamefanywa *garage* au pamefanywa *parking* za magari, basi jambo hilo pia hatulioni. Tunakuja kukaa hapa na kusema mambo mengine ambayo tunaposema tunakuwa tunaweka hitilafu kwa watu.

Kwa hivyo, nitakuomba sana Mhe. Naibu Spika, suala la *UUB*, ujenzi wa barabara hususan matumizi ya barabara yatumike kwa makusudi yaliyokusudiwa, barabara zipitike kila wakati, sio barabara zipitike mchana ikifika jioni watu wanafanya *parking* za magari na kufanya ma- *garage*.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Shirika la Bandari. Shirika hili mimi nilipongeze sana kwa ufanyaji kazi wake sana. Tumepiga hatua sana japo kulikuwa kuna malalamiko, lakini nashukuru kwamba Shirika la Bandari linafanyakazi vizuri sana tena. Limeweza kununua vifaa mbali mbali, limekuwa sasa hivi tatizo la bandari la ucheleweshwaji wa mizigo limeondoka. Lakini kama ripoti ilivyosema kwamba kuna tatizo la uwekaji wa makontena matupu. Tukumbuke Baraza hili hili lililopita tulipiga kelele na tukaruhusiwa kwamba tuweke, lakini ile miezi sita imekwisha pale. Namshukuru sana Mhe.

Waziri kwa maamuzi yake ya Kimapinduzi, kuamua kwamba watu waweke pale yeye ndiye atakayejibu maswali yale, mpaka leo watu wanaweka makontena yale. Ni lazima patafutwe *centre* maalum ambayo itakuwa inamilikiwa na serikali, ili makontena yale yaweze kukaa sehemu ile. Tusikae leo na kesho hali ya kuwa kwamba mwenye eneo lake akalitaka ikatupa tena matatizo.

Nitakuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja suala la sehemu ya kuwekea makontena matupu ya bandarini, tuwasaidie wenzetu wana nia ya dhati kabisa ya kutufanyia kazi za kweli, bandari sasa hivi imekuwa afadhali, kontena lako ndani ya saa 24 lazima utakuwa umepata unapoitaka, tofauti na nyuma, nyuma ilikuwa siku tatu, nne, au tano. Sasa hivi ndani ya masaa 24 kontena imeshuka unaitaka unaipata, niupongeze sana uongozi wa Shirika la Bandari.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, niende katika Shirika la Meli, pamoja na uchakavu wa meli zilizokuwepo na kumpa tabu Mhe. Mkurugenzi wa Shirika la Meli, nimpongeze anafanyakazi katika kipindi kigumu sana, tumemtengenezea meli ya MV. Mapinduzi II ambayo ni meli nzuri, lakini kwa uendeshaji wake tumempa mzigo mkubwa ambapo yeye mwenyewe pengine kama anasema chini chini au kama hasemi kutokana na uendeshaji wa meli ile. Uendeshaji wa meli ile unasemekana kwamba hauingizi kitu. Meli yenyewe naambiwa kuwa inapakia tani 4 sijui, gari haiwezi kupakia meli ile, utegemee biashara ya ndizi na makaa kutoka Pemba na abiria, tutafanyakazi vipi tunampa mzigo ni lazima tutafute njia nyengine mbadala ya kuona ile meli inamuingizia pesa, ili kuweza kukidhi haja na hata kuweza kununua meli nyengine. Lakini kwa meli ya MV. Mapinduzi II, ni kweli ni mzigo kwa watu wa Shirika la Meli, mimi niwapongeze tu katika ufanyaji wao wa kazi, wanafanyakazi vizuri japokuwa wanachangamoto hizo. Imezungumzwa kwamba meli nyengine zile mbovu mnatangaza kuziuza, lakini najua bado mpaka leo tarehe ya kuuza meli ile bado, lakini tuna hamu sana tusikie kwamba meli zile zinauzwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuleta meli nyengine.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Viwanja vya Ndege. Nipongeze kwenye miaka mitano au miaka 10 ilivyokuwa sio Uwanja wa Ndege sasa hivi, imekuwa kweli *Zanzibar International Airport Karume* inaelekea elekea, nimpongeze sana Mkurugenzi pale ndugu Said Iddi Lubugani kwa kazi nzuri aliyofanya katika viwanja vile vya ndege, angalau unajisikia kwamba unakwenda kweli Uwanja wa Ndege wa Zanzibar, hongera zake katika hilo.

Vile vile apewe jitihada, yale malalamiko aliyokuwanayo juu ya fedha nyingi kuingia katika mfuko wa serikali basi aongezewe kidogo, hizi pesa zipunguzwe

angalau kidogo awe nazo kwa kuweza kuongeza miundombinu mengine pale na kuimarisha uwanja wa ndege wetu. Kwa kweli anafanyakazi ngumu sana na nzito na kila mtu shahidi kwa viwanja vile kwamba vimepata mabadiliko makubwa sana.

Mwisho niende katika suala zima la mawasiliano.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe umebakiza dakika moja.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Ahsante sana, naomba nimalize. Mawasiliano naipongeza, lakini ina malalamiko. Sasa hivi mitandao ya kijamii Mhe. Naibu Spika, imekuwa changamoto, na wizara ipo. Tunakuta kila siku ya Mungu kuna mitandao mbali mbali kuna *Mzalendo Network* leo hii anathubutu kuandika mambo ambayo hayastahiki kuandikwa. Anathubutu kuandika aliyekuwa Rais wa Zanzibar Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein ni makosa na hakuna hatua yoyote ambayo inachukuliwa. Huku wao wanaandika Rais halisi mteuliwa wa Zanzibar, mpendwa na watu Maalim Seif. Jamani tunaogopa nini kama hii nchi yetu na sheria zipo tunashindwa kuchukua hatua kwa nini, tunasubiri nini jamani. Viongozi mawaziri mko nyie mbele, kila siku ya Mungu ukiangalia *Mzalendo Network* unakuta mambo hayo. Hata juzi wakati Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar alivyokuja kulihutubia Baraza la Wawakilishi. Baada ya dakika tano tu kumaliza kuhutubia imekuja *speech* ambayo sio ya kweli.

Je, mpaka leo mnashindwa kukanusha, hata ile kukanusha inashindikana, kuchukua hatua inashindikana. Ina maana wanasema kwamba Rais kasema uongo. Kwa sababu baadae siku ya pili ikatolewa hotuba ya Rais aliyoizungumza, mwanzo wametoa wale jamaa hotuba ya uongo ya kugombanisha watu. Hii nchi bado ina amani, utulivu na usalama. Lakini kwa taarifa kama zile cha kiuchochezi, itaiweka Zanzibar pahala pabaya. Nitawaomba sana waheshimiwa tujaribu kuwa wakali katika hicho. Ahsante sana, japo muda mdogo naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Mjumbe, sasa mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Bahati Khamis Kombo, baada ya hapo atachangia Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, na atafuata Mhe. Mohammedraza Hassanali.

**Mhe. Bahati Khamis Kombo:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa na mimi nafasi ya kuweza kuchangia machache katika ripoti hii. Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nichukuwe fursa hii ya kuwapongeza Mhe. Naibu Waziri

wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, pamoja na watendaji wake wote. *(Makofi)*

Pia nimpongeze Mhe. Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasilano na Usafirishaji pamoja na watendaji wao wote, kwa mashirikiano makubwa waliotupa wakati tulipokuwepo katika kamati. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja katika kuchangia machache. Mhe. Naibu Spika, nimepata tabu sana tokea ripoti zetu tulipoanza kuwasilisha mpaka hii leo kwa jambo moja kubwa. Katika ripoti zetu zote Mhe. Naibu Spika, zina ukosefu wa wataalamu. Lakini hii ripoti yetu sisi pia ina ukosefu wa wataalamu na wenye utaalamu wa utawala. Mhe. Naibu Spika, jambo hili kwa kweli halitotufikisha pazuri katika serikali iwapo hatutokuwa na wataalamu na pia wataalamu wa utawala. Ofisi zetu hazitokwenda vizuri kwa sababu hazina wasimamizi wenye taaluma nzuri. Kwa hivyo, nikuombe Mhe. Naibu Spika, jambo hili liangaliwe kwa kina ili liweze kuondoka kwa haraka sana katika ofisi zetu.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika jengo la Ofisi Kuu ya Mahakama ya Ardhi iliyopo Vuga. Pamoja na uhaba wa vyoo, lakini ofisi hii Mhe. Naibu Spika, haifai na haifai hasa kwa wafanyakazi wanaofanyakazi mule. Ofisi ile tumeikagua kwa kweli hairidhishi hata kidogo. Tumepata taarifa ya kwamba kuna wananchi ambao wanakuja pale wakati wa kusikiliza kesi basi ni tatizo kubwa sana, vyoo hakuna wanakwenda kujisaidia katika vile vyoo ambavyo havitumiki tena. Wale wafanyakazi waliomo mule ni binadamu kama binadamu mwengine, wanahitaji kuwekewa mazingira mazuri ambayo kuwa wataweza kufanyakazi na wao kama binadamu mwengine. Mhe. Naibu Spika, ningeomba jengo lile liondolewe pale kwa haraka sana, na pia jengo lile wale waliomo mule baada ya kuondoka basi lifanyiwe ukarabati wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, kamati katika kutembea kwetu tumebaini kwamba wananchi wana muitikio mdogo wa kulipia uchangiaji wa huduma ya maji. Suala hili Mhe. Naibu Spika, ni kweli na kama halikupatiwa ufumbuzi mzuri, basi wataendelea kutokuchangia maji na kwa sababu zao maalum. Kwanza Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya wananchi maji hawapati inafikia miezi miwili au miezi mitatu hawapati maji, ni kweli hawatoweza kulipa mfereji mtupu wakati maji hawapati.

Mhe. Naibu Spika, nimsifu sana Mhe. Salama Aboud Talib Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa juhudi zake nzuri anazozichukua. Namuomba waziri Mhe. Salama Aboud kwa juhudi zako nzuri ulizonazo, uendelee kuwapa

taaluma wafanyakazi wako wanaopita wakichukua uchangiaji wa maji kuwapa taaluma nzuri wananchi na wasiwe wenye hasira, kwa sababu wananchi wana changamoto kubwa ya maji, bila ya kuwa na wao kwenda pale na kuwapoza wananchi, basi wataendelea kugombana siku zote. Mhe. Waziri nakuomba sana.

Nikiendelea Mhe. Naibu Spika, niende katika mawasiliano, Idara ya Usafirishaji na Leseni Mwanakwerekwe. Mhe. Naibu Spika, ofisi ile ni kubwa na ina kila aina ya mapato yanayochukuliwa pale, kama usafirishaji wa leseni uko pale, leseni, usafirishaji na kila tunavyojua lakini lile banda walilonalo halikidhi. Mhe. Naibu Spika, nathubutu kukuambia tena kwamba tulikwenda lakini hata chooni huwezi kufika na choo hicho tunaambiwa wanatumia wafanyakazi wale. Kwa kweli wafanyakazi wale hatuwatendei haki.

Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Naibu Spika, wangefanyiwa ukarabati wa kutosha katika jengo lile ili na wao wakaweza kukaa katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la ukosefu wa mitambo iliyoko Karakana na mitambo iliyoko Tibirinzi Pemba. Mhe. Naibu Spika, karakana zile ni za serikali na magari yetu ya serikali tunayapeleka katika karakana, lakini karakana zile tumeona kwamba hamna vifaa vya kutosha vya kutengenezea yale magari. Kwa hivyo, ningeiomba wizara zile karakana zipatiwe vifaa vya kutosha vya kufanyia kazi, ili na haya magari yetu tusiyapeleke nje ya karakana, karakana ile inatia hata faida kwa wananchi wa nje, pale wanapeleka gari zao, lakini wakiona pale hakuna vifaa vya kutosha basi hawawezi kupeleka gari zao, ina maana lile tulilokusudia hatulipati.

Mhe. Naibu Spika, kwa leo naomba nichangie hayo na kwa vile ni mjumbe wakamati basi nimeona nichangie machache tu. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Bahati Khamis kwa mchango wako mzuri kabisa. Anayefuata ni Mhe. Nadir Abdul-latif, baadae atafuata Mhe. Mohammedraza Hassanaali, na ajitayarishe Mhe. Asha Abdalla Mussa.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf:** Bismillah Rahman Rahim. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majukumu mazito aliyokuwa nayo yeye peke yake ndani ya wizara na watendaji wa chini.

Lakini la pili, nimpongeze sana Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuturuhusu sisi wawakilishi siku aliyokuja kwamba tuzungumze yale ambayo tuna uhakika nayo na yenye ushahidi, na hayo tutayafuata kama alivyotuagiza.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza kuchangia kwenye ripoti ya kamati ya mawasiliano na ujenzi. Nitaanza na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Jambo la kwanza nitakwenda moja kwa moja kwenye Mji Mkongwe, kusema kweli kuna watendaji wazuri hasa wakurugenzi na watendaji wengine ni watu ambao wako sawa kwa kiasi fulani, japokuwa binadamu hakuna aliyekamilika. Lakini kwenye masuala ya changamoto, wanalaumu kwamba hawashirikishwi hasa katika hizi *project* ambazo zinaendelea ndani ya Mji Mkongwe eneo lao na wao wako *under UNESCO*, kuna masharti na vitu vingi vinataka kuzingatiwa wakati wa kujenga katika eneo la Mji Mkongwe. Sasa sijui ni sababu gani ambazo kama wizara nyengine au serikali haiwashirikishi vizuri katika masuala hayo wakati wao wapo. Kama ingekuwa haina haja ya wao kuwepo basi bora waondoshwe tujuwe hawapo ili watu wanapotaka kufanya yao waendelee tu kufanya bila ya kuwashauri.

Vile vile ushauri wangu mwingine katika Mji Mkongwe ni kwamba yale majumba ambayo yanajengwa ya kisasa na wakati ule ni mji wa kihistoria, basi ningeomba sana kwamba wasiruhusu, hasa zile sehemu za *open space* nyingi ambazo zilizoporomoka, zilizokuwepo *natural* yake kwmaba ziko tupu, basi kuna baadhi ya watu wamejaribu kujenga katika maeneo yale na wamejaribu kujenga katika *new shape*, ambapo nyumba mtu akiiona tu anajua huu ni mjengo wa kisasa. Lakini mimi ningeshauri kwamba wawaruhusu, lakini wangejaribu kuwapa ramani angalau zifanane sana na yale majumba ya kihalisia yaliyokuwepo ndani ya Mji Mkongwe, ili ile hadhi yenyewe ya Mji Mkongwe isijeikaondoka, kwa sababu majumba leo yataoza, yataporomoka na watakuwa watu wanajenga wanavyotaka wao, mwisho ule Mji Mkongwe ndani ya miaka 50 au 100 mbele utaondoka.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye suala langu jengine la majenzi. Majenzi ndani ya wizara yake kuna watendaji ambao wanafanyakazi za utapeli ndani ya wizara hiyo ya mawasiliano. Katika hiki kipindi cha nyuma kuna watendaji wasiopungua watatu ndani ya wizara yake wamekuwa wanatapeli watu, wanawaendea na kuwaambia kuna nyumba za kilemba zinauzwa, wanakwenda kuwaonesha wanachukua milioni 17 au 18, halafu *at the same time* hao hao siku za mbele kidogo wanawafuata wale waliowauzia wanawaambia kuna mtu mwengine kwa bei kubwa tunakuletea. Matokeo yake akipelekwa yule mtu anavamiwa na polisi ambao wamewapanga wao wale watendaji na zile fedha

ndio zimeshakwenda na maji na mkataba wanauchukua. Suala hili lipo na Mhe. Naibu Waziri kama atalikataa nitamuomba ainuke anikanushe, nina uhakika nalo. Kwa hivyo, ningemuomba sana aje atujulishe kuwa suala hili atawachukulia hatua gani, na nyumba watarejeshewa lini hao waliodhulumiwa, kuna kesi kama mbili au tatu zipo ambazo ni za utapeli ndani ya wizara yake ambapo watendaji wake ambao wamefanya masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye suala la Uwanja wa Ndege ambalo nililizungumzia juzi, lakini kuna baadhi ya vitu nilikataliwa kwamba nilichosema hakina uhakika. Mimi nilizungumza kwmaba Uwanja wa Ndege sehemu ya *terminal* ili-*fail*, kazi ilikuwa sio nzuri, sehemu ya ku-*park* zile ndege mbele zili- *fail* zikatafutwa na sehemu nyengine nikakataliwa. Lakini mimi nina ushahidi huu hapa, picha zimo, *drawing* ya mwanzo inasema iko vyengine, ambapo ndege zilikuwa zi- *park* nne mbele ya uwanja wa ndege hizi hapa, zi-*park* nne kwa mbele. Sasa hivi wamebadilisha mchoro ambapo ndege mbili zita-*park* mbele ndogo, kwa sababu zile kubwa haziwezi kuingia na mbili zita-*park* kwa pembeni. Hii maana yake ni kwamba uwanja wa ndege ni *failier*. Hao ambao wanakataa mimi ninazo hizi hapa, na hata Mhe. Rais ametuhakikishia kwamba mambo tuliokuwa na uhakika nayo tuyazungumze. Lakini cha ajabu uwanja wa ndege ule watendaji wako hai hawajafa, na mimi ninachoshangaa zaidi ni kwamba Wizara ya Fedha na Mipango mtu aliyeiba dola 10 tu katika hoteli atafanyiwa kesi kubwa sana kaiba mapato. Lakini mabilioni kama haya mpaka leo watendaji waliosababisha hasara ndani ya nchi hawajachukuliwa hatua.

Mimi nitatoa mfano mdogo tu *Airport* ya Dar es Salaam Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano alikwenda kipindi cha nyuma akaambiwa *Airport* ile ni bilioni 560 mpaka kumalizika jambo lile kalilani *Management* nzima kaivunja na akaagiza lile suala lichunguzwe kwamba hajaridhika na ujenzi ule. Lakini hapo hapo tukenda kwenye Airport ya Dar es Salaam ina ukubwa wa *Squire meter* elfu 60 mpaka elfu 70 ina *capacity* ya kuchukua wageni milioni 6 kwa mwaka mpaka milioni 7 kwa mwaka. Lakini *at the same time* ina uwezo wa kuchukua wageni laki tano mpaka laki sita kwa mwezi lakini imetumika karibu dola milioni 240 kwa bilioni 560*T.Shilling* Mhe. Mwenyewe Rais hakuridhika na lilimkera sana kwamba jambo lile juu ya kwamba *Airport* ya Dar es Salaam kubwa mara tatu kwa mujibu wa *size* kuliko *Airport* ya Zanzibar.

Lakini twende kwenye *Airport* ya Zanzibar, *Airport* ya Zanzibar ina *capacity* ya kuchukua watu 1.3 *million* to 1.6 *million* ambayo wameongeza wao baadae itakuwa na ukubwa wa size between elfu 17 *square meter* mpaka elfu 21 *square meter* na imesha-*cost* mpaka sasa hivi dola milioni 128,747.89.51 kwa

Shilingi itakuwa karibu bilioni 285. Mheshimiwa cha kusikitisha kwamba *Airport* ya Dar es Salaam kubwa sana mara tatu kuliko ya Zanzibar na imeanza mwisho na inamaliza mwanzo, *Airport* ya Zanzibar umefanyika utumbo wamefeli katika masuala ya michoro, wamefeli kwenye masuala ya ku-*park* zile ndege zimefeli na isitoshe fedha zilizotumika wangesema wajenge *Airport* hii ya Zanzibar kama ya Dar es Salaam basi wangetumia dola milioni 375 karibu ya trilioni moja. Inamaanisha dhahiri kwamba *Airport* ya Zanzibar ina madudu, ilifeli na watu wamesababisha hasara lakini mpaka leo wanaangaliwa tu na hili tatizo ambalo halichukuliwi hatua kwa sababu mambo ya undugu undugu tunaoneana muhali.

Lakini suala hili mimi nitamuomba sana Waziri wa Fedha alifanyie kazi kama anavyochukua hatua watu walioiba kodi ndogo ndogo sikwambii hizi fedha kubwa zinazosababisha hasara wakati watu wapo wanacheka tu, miguu juu wameshafaidika na walichokipata wanacheka sasa hivi mimi naondoka *Airport* nimekuja na ushahidi kamili kwa sababu ninachoongea nina uhakika nacho.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Nadir kama una ushahidi unauleta mbele kwenye Afisi ya Katibu halafu anawasilisha.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Mimi ushahidi wangu kwamba *Airport* imeshatumika fedha nyingi hizi hapa Dola milioni 128 na *drawing* ya mwanzo na ya pili tofauti.

**Mhe. Naibu Spika:** Nakwambia anakuja msaidizi anaichukua hiyo *Document*.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Njoo uchukue lakini na mwenyewe nirejeshewe isije ika-*dissapear* maana yake mara inafichwa.

**Mhe. Naibu Spika:** Aaa hiyo itabakia huku.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Mara inafichwa siamini

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Nadir hiyo inabakia huku kama ni hivyo hatuhesabu kama ni ushahidi.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Mimi nitaileta lakini kopi yangu nibakiye nayo.

**Mhe. Naibu Spika:** Endelea.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Mhe. Naibu Spika, mimi naendelea kuchangia kwenye suala la Wizara ya Ardhi, Wizara ya Ardhi kipindi cha nyuma tulizungumza kwamba imetoka kauli ya kufuta ardhi na suala hili ambalo lina wananchi wanyonge ndani ya nchi hii kwani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inamuogopa nani kusema kwamba tunatoa tangazo kwa yoyote aliyekuwa na maeneo ya bahari au maeneo hayajafanyiwa kazi tunatoa kwa muda wa miaka mitatu tutaweza kuja kumnyang'anya.

Lakini tunapotoa kauli kwamba tutawafutia watu wote waliokuwa wamejenga *foundation* na fence hili suala haliingii akilini. Kwa sababu sheria inasema katika kifungu cha sheria cha ardhi kifungu 56 mwaka 1992 kinasema Wizara ya Ardhi inaweza kuchukua maeneo ya wananchi kwa *National interest* mambo ambayo ya kitaifa ya muhimu, na mambo hayo hawawezi tu Wizara kwenda kuchukua ardhi mpaka waende Mahakama ya ardhi wakathibitishe kile wanachotaka kukifanywa na wanatakiwa walipe *compassion* pamoja na kile kilichokuwemo kwa *value* ya wakati ule uliokuwepo.

Leo imetoka kauli imewaumiza watu vichwa imesikitisha watu wengine wamekufa kwa *pressure* huko duniani watu wameshahangaika miaka mingi, tunapotaka kuzungumza vitu vya kuelimisha kama watu wajenge tuzungumze tu kwamba watu tunawatoa muda fulani wajenge, lakini tusitumie njia kutaka kutisha watu halafu matokeo yake watu wameathirika vibaya na mpaka leo jambo hili limenyamaziwa kimya utaratibu gani uliofuatwa na wakati kuna sheria nyengine hiyo hiyo ya mwaka 1992 inasema mtu unatakiwa umpe miezi 18 utume barua.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa umebakisha dakika mbili.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Mimi siku zote nikiongea dakika zangu zinarushwa hazitimii na naangalia *this is to much*, mimi nilikuwa namaliza dakika kumi, saa 7.10 lakini sasa hivi unanambia dakika mbili.

Jengine ambalo ninalotaka kulizungumzia kwenye masuala ya barabara Wizara ya Mawasiliano barabara ziko chini ya kiwango, barabara zinazojengwa wanapewa watu ambao wanawataka wao na ukiangalia kwenye tenda unakuta watu 16 lakini atakuja kupeawa mtu mmoja ambae ambae wanamtaka wao kiwango kibovu, kiwango kiko chini ya tani 20 Zanzibar fedha inayojengwa ni zaidi ya bilioni na milioni 200 kwa *kilometer* wakati huko nchi za wenzetu wanajenga tani thalathini kwa shilingi milioni 850. Mhe. Rais juzi kazungumza kwamba wakijenga Serikali milioni 600 lakini akijenga mtu mwengine wafanyabiashara binafsi wanaopewa na watu wanaowataka bilioni moja na

milioni mia mbili. Hili suala ndio nazungumza tena ndani ya Serikali watendaji baadhi yao ndio watakaoua Serikali na sisi tupo hapa hatupigi kelele kwamba labda tunafaidika mimi Nadir na watu wangu, mimi napiga kelele kwa sababu Serikali yaondoshwe haya madudu yaliyokuwepo ili twende safi. Lakini ndio hivyo tena tunataka tunzungumze mambo mengi dakika tunaambiwa zimekwisha, mimi kutokana na mambo mengi ya humu ndani sijaridhika nayo mimi hoja siiungi mkono.

**Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohammedali:** Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa dhati kabisa kwanza kabisa nichukue nafsi hii kuishukuru Kamati hii ambayo inaongowa na *comrade* Mwenyekiti Mhe. Hamza ambae ni msikivu ana hekima na busara, lakini nishukuru Kamati nzima kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, laki ninishukuru na taasisi zote zilizotoa mashirikiano katika kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, sina tatizo na ripoti hii ninaikubali na kazi tuliyoifanya tumeifanya kwa uhakika, hatukuwa tumebahatisha kwa hivyo naipongeza wenzangu wote tuliofanya kazi hii basi ilikuwa ni kazi ya uhakika, haikuwa kazi ya majungu wala fitna wala mambo mengine ambayo kwa *interest* ya mtu. Mhe. Naibu Spika, mimi nishukuru Wizara zote Wizara mbili hizi lakini vile vile niwapongeze watendaji wakubwa, mimi nishukuru taasisi zote zilizokuwa chini ya Wizara hizo mbili ote, zinafanya kazi kwa uzalendo, zinafanya kazi kwa uchungu wa nchi. Lakini nafikiri kuna haja ya *Communication* mawasiliano ni jambo muhimu kwa Wizara hizi zikawa kila wakati zinafanya mawasiliano, kwa sababu kila moja inamuhitaji mwenzake.

Wizara ya Mawasiliano inajenga barabara inatia lami baada ya miezi mitatu inakuja Wizara ya maji inasema hapa kuna mradi wa maji matokeo yake ile barabara ambayo ilikwishakuwa tayari inabidi inyofolewe, na unajua Mhe. Naibu Spika, shati ikizaliwa kiwandani ukija ukishona ina maana tayari umeshainyofoa japo kwamba gharama zile zinafidiwa lakini matokeo yake barabara zetu huko tunakokwenda inakuwa ni chakavu na hasara kubwa ambayo tunapata, kwa hivi naomba *Communication* mbili hizi hizi ziwe na umuhimu kati ya ZAWA na ZECCO wakae pamoja unapopita mradi basi wawe na mawasiliano kati ya ZAWA na ZECCO kwamba bwana hapa tunapitisha lami je kuna waya inakuja, jamaa wa ZECCO au jamaa wa ZAWA wanawaambia jamaa wa ZECCO jamani tunafanya mawasiliano tunataka kupitisha lami Idara ya barabara kwa hivyo je kuna suala ambalo linataka kupitishwa waya au maji ili kukabiliana na gharama ambazo zinaweza kujitokeza ambazo hazina ulazima.

Mhe. Naibu Spika hili ni jambo muhimu lakini *communication*, lakini nishukuru taasisi zote hizi za bandari, Mji Mkongwe sehemu zote na Wizara zote ka kweli Mhe. Naibu Spika, vijana wetu hawa wana uzalendo mkubwa, lakini kubwa naona ni nyenzo na tuwe wa kweli, unajua tukiwa wa kweli basi mimi nafikiri mambo mengi. Kwa hivyo sisi kama viongozi kama watendaji tuwe wa kweli katika kutoa mawasiliano na kutoa *communication* kwa wananchi wetu waliotuchagua, waliotufikisha hapa tunaitekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Baraza hili linatekeleza ilani moja tu ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein.

Kwa hivyo changamoto zilizokuwepo ni mbili naomba muzichukue mimi sina masuala nina *confidence* na watendaji wote lakini changamoto mbili hizi ni muhimu sana Mhe. Naibu Spika, hili la kwanza tulipofanya ziara nakubaliana na Mwenyekiti wangu *comrade* Mhe. Hamza na Wajumbe tulipofanya ziara pale *Airport* Pemba Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akajitahidi sana na kelele hizi zilianza huku. Kuhusu taa kuwaka Pemba *alhamdullillahi* namshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na uongozi wake na Baraza lake la Mapinduzi kwa kuweza kufanikisha ZECCO ikachangia pesa nyingi sana na kama sikosei gharama yake zile za umeme ilikuwa haipungui Dola laki tano na mambo yote na Rais akasema ni lazima kwa hivyo tukenda tukafanya sherehe taa zikawaka na ndege zikatua.

Mhe. Naibu Spika, kama ripoti hii inavyosema *transformer* ambayo inayotumika uwanja wa Ndege wa Pemba *transformer* ile ni ya wananchi, sasa wananchi tunapozidisha mahitaji ya umeme kila siku *any time transformer* ile ni kazi ya Mungu ile ni mashine inaweza kuripuka na ikiripuka ina maana hakuna taa; kwa hivyo ndege hakuna zile pesa ambazo tume-*invest* mabilioni tumeshindwa Mhe. Naibu Spika, kutafuta *transformer* isiyopungua dola elfu 40. Mimi na Wajumbe wangu nikawaambia Mhe. Naibu Waziri hili jambo dogo Rais ameshajitahidi hebu tuwaambie kama una shida ya milioni 50 au 60 njoo uchukue kwangu kesho halafu baada ya mwezi unirejeshee tulikuwepo sote, tuambie nini tatizo kwa sababu ZECCO Leo umeme Mheshimiwa pale tusidanganye hamna umeme Pemba pale kuna kitu ambacho cha kubahatisha tu, kwa hivyo tumetumia mabilioni tunashindwa kutumia na *transformer* ikawa ya *Airport* pale ZECCO Wizara inahusika kwa ajili ya dola elfu 40 mpaka 50.

Mhe. Naibu Spika, lazima *we have to be serious* huyu Rais wetu amejitahidi sana kwa hivyo ninachotaka Mhe. Naibu Waziri kama hizo pesa hukuwa nazo mpaka kesho njoo uchukue kwangu leo ukatie hiyo *transformer* halafu unilipe sitaki riba. Kwa sababu ulitoa ahadi, na hii Mhe. Naibu Spika, nataka niiambie

nchi nzima kamati hii nzito kamati hii haina kutafuna tafuna maneno hasa nikiwemo na mimi. Kwa hivyo naomba kabisa tunapozungumza Mhe. Naibu Waziri ulitoa ahadi ukasema utakuja haina kumfikisha haja Rais, wala haina haja ya nini ukalimalize hili kwa wiki moja kwa niaba ya wananchi, kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi. *Otherwise* njoo utwambie mwambie Mwenyekiti wangu tu na huu ushahidi uliokuwepo hilo niliweke sawa kwa sababu ZECCO na mambo mengine tumeshafanya mengi haiwezekani Mhe. Naibu Spika, leo umeme hapana pale Pemba.

Kwa hivyo hili nimeona nitoe changamoto kwa Wizara inayohusika ambalo amelitolea ahadi mwenyewe Mhe. Waziri akatwambia sie, kwa hivyo sisi tuna uchungu na nchi tunaipenda nchi yetu, tunakipenda chama chetu cha Mapinduzi, huu ndio ukweli. Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi niwasaidie wajumbe wenzangu hili suala la *Terminal II* mpya Mhe. Naibu Spika, wakati uwanja wa Ndege ule unapanuliwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein alipoingia madarakani mwaka 2010 alipokuja *Airport* katika kipindi chake kile cha kwanza, mimi nilikuwepo kwa sababu ndio Mkurugenzi mtendaji wa kampuni ya *Airport* ya ZAT.

Mhe. Naibu Spika, *Airport* ile ilikuwa na mwangaza wa kupokea ndege katika dirisha la 737 sasa tunakwenda na wakati ina maanda ndege zote ilipojengwa ramani ya *Airport* ile ilikuwa ndege zote 767, *Air Bus* na ile 737 Mhe. Naibu Spika, umepitwa na wakati haziji sasa Zanzibar si nyingi. Kwa hivyo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akasema jamani kaeni jengo hili la kupeleka 737 haliwezekani kwa sababu ndege hizi sasa hivi tunakwenda na dunia ya kisasa, kwa hivyo Mhe. Rais wa Zanzibar unajua ni mkimya sana lakini ndiye aliyegundua kwamba taarifa ile kwamba 737 ndiyo inayokuwa pale. Sasa hawa ambao, unajua Mheshimiwa ukenda Marikiti kila mmoja karoa damu mchinja ng'ombe humuoni. Kwa hivyo lazima tuwe wakweli mambo yamevurugika watu walikuwa na *interest* zao, watu walikuwa na umimi umimi ndio nchi imefika hapa tulipofika.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nataka niwaambie Wajumbe wenzangu kwamba marekebisho yale ambayo amesimamia Rais na Wizara ya Fedha ni kuondosha tatizo la kulisogeza ili ndege zote ziweze kuwa *park* na hilo ndio limetu-*cost* sisi Zanzibar leo. Zanzibar tumefikia hapa kutokana na gharama ile kwa sababu mradi ule ulikuwa wa *World Bank*, na *World Bank* walifadhili *Airport* sasa kama wamefadhili ndege zote zitue mpaka *747* halafu unakuta kifaranga cha 737 kuwa *park*, kwa hivyo utaalam na wahusika ndio walioweza kufikisha hatua hii tuliyofika na wanajulikana wanafahamika. Kuna mseto dengu lakini

leo huwezi kwenda kumkamata Katibu Mkuu Mustafa Jumbe ukamkamata Balozi Karume, Mama Salma katika wizara yao ukaanza kuwaleta pamoja.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa umebakisha dakika moja.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mheshimiwa la mwisho nimalizie, pale Mwanyanya kulikuwa na tatizo la maji mpaka Kibweni mie maji nilikuwa sina kwa miaka ishirini, kwa hiviyo nashukuru ZAWA na Wizara kumbe sehemu ya Mwanyanya pale kuna maji ya kutosha. Sasa ZAWA ndio yetu lazima tuchangiane nikawaambia ZAWA mimi niko tayari kugharamia ikiwa milioni mia moja, mia mbili moja katika zaka kuwasaidia Wazanzibari. Kwa hivyo ZAWA wakatupokea tulipopokewa na ZAWA wakasema ule mradi uko chini ya kambi ya Jeshi ya Mwanyanya, basi tukatoka na ZAWA yaani Serikali na Ma- *engineers* tukenda kwenye kambi ya Jeshi iliyokuwepo hapo. Tulipokwenda hapo kuomba wakataka Serikali iombe ile sehemu ya kutoa maji Serikali, Wizara ilete ramani taratibu zote ZAWA wakafanya nashukuru sana na Wizara, ZAWA wakafanya kila kitu kikafanyika mashine ikapelekwa kwa sababu yale maji yalikuwa yanakwenda mpaka Kibweni ZAWA walinambia Raza ukikata maji hapa wananchi wataumia kwa hivyo ni mimi sikutaka kuchukua dhima kwa mungu fimbo ya mungu haina sauti.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa Muda wako umekwisha malizia.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Tukenda matokeo yake Mhe. Naibu wakataka ramani ya Mwanyanya jeshini pale tukapeleka wakataka barua itoke Mkurugenzi ni mteuliwa wa Rais Zanzibar ikapelekwa, mashine ya maji ikapelekwa matokeo yake Mheshimiwa yule kijana wa pale Jeshini anasema eti sikupata kibali Kibaha, aaa! ardhi ya Zanzibar Wazanzibari ardhi yetu unasema hujapata kibali kutoka Kibaha, Kibaha ndio Zanzibar sasa Mheshimiwa mimi nataka yule Mwanajeshi atuombe radhi Wazanzibari la kwanza. Pia ardhi ya Rais wa Zanzibar ndio mwenye Katiba ya nchi hii, Waziri wa Ulinzi, Waziri wa Mambo ya ndani hawana mamlaka ya kuzungumza mambo ya Zanzibar mwenye kuzungumza mambo ya Zanzibar ni Waziri yule pale.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mwenye kuzungumza mambo ya Zanzibar ni Waziri yule pale yeye ndio Waziri wa Ulinzi,Mohammed Aboud Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais hao ndio

viongozi, ule mradi haukupatikana wametuzuia mashine imekwenda ardhi wamesema hawawezi mpaka itoke Kibaha. Mheshimiwa nasikitika sana na hili sio jambo la kwanza jambo la pili lilitokea vile vile sherehe zetu za Mapinduzi wanajeshi wakasema mizinga isipigwe, Rais wa Zanzibar aingie mwisho sasa mambo kama haya tukiyawacha yanafanya mengi.

**Mhe. Naibu Spika:** Basi Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Naibu Spika, mimi naomba tuombwe radhi lakini nasema Mamlaka ya ardhi ya Zanzibar iko chini ya Rais wa Zanzibar chini ya Wazanzibari, na hii ramani Mheshimiwa nikuletee lakini haya hayakufanyika. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naunga mkono Wizara zote nazipongeza kwa mashirikiano mazuri *(Makofi)*

**Mhe. Asha Abdalla Mussa:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi kunipa nafasi hii ili nizungumze machache kupitia ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, mimi nimesimama hapa kwa ajili ya kutetea wanawake wenzangu wa Zanzibar nzima kupitia Wizara zote hizi mbili.

Mhe. Naibu Spika, kilichonisimamisha hapa suala zima la maji wanawake tunateketea sana kwa ajili ya suala zima la maji, na tunateketea kwa sababu vyanzo vya maji vipo lakini watu wanavivamia. Lakini pia maeneo ambayo wamesambaza maji kupitia mamlaka ya maji ZAWA kuna maeneo mengine huduma hizi hakuna, cha kusikitisha watu wa Mamlaka ya Maji unapotaka kuwasiliana nao kama sisi viongozi wakati mwengine huwapati hawapokei simu sasa sisi tunashindwa wakati mwengine hatujui tufanyeje. na tukiwafata tunakuwa hatupati fursa ya kuonana na hawa watendaji.

Lakini pia cha kusikitisha zaidi unaweza ukaambiwa kwamba hapa tatizo ni kitu fulani yaani pampu, lakini utanunua pampu na badala yake baada ya siku tatu au wiki moja maji hayatoki tena, hatujui sababu ni nini. Kwa hivyo hapa tunapatwa na wasi wasi kwamba laba utafiti wao unakuwa bado haujawa wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi baadhi ya vituo vingi vya Afya tatizo la maji limekuwa sugu. Wanawake wanapokwenda kujifungua wanalazimika kuchukua maji kwenye vidumu na kwenye ndoo kupeleka katika vituo vya Afya. Suala hili linatusikitisha sana Mhe. Naibu Spika, hususana katika kituo cha Afya cha Kitope, wananchi wanapata shida sana wanatoka wanakotoka wakifika pale wamechoka na maeneo wanayotoka maji hakuna, wawalazimika kwamba wanunue maji mengine waache nyumbani na mengine wabebe

wapeleke katika kituo cha Afya kwa ajili ya kumuhudumia mgonjwa. Namuomba sana Mhe. Waziri akae pamoja na watendaji wake kupitia Mamlaka ya Maji ZAWA ihakikishe kwamba wakaone, wakatizame tatizo ni nini ili na baadae lipatikane ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye suala jengine, kuna chemchem zetu ambazo tunazifahamu na chemchem ambayo nyengine ipo eneo la Kirombero baina ya Kirombero na eneo la Mchangani. Chemchem ile wakati maji yanapokuwa hayapatikani katika eneo la mchangani pamoja na eneo la Kirombero wananchi huwa wanakwenda kufata maji katika eneo la chemchem hiyo. Lakini mifugo pia wanakwenda kunyweshwa katika chemchem hiyo, kwa sasa kuna tatizo kubwa kumeibuka na ukulima huu wa matikiti. Hilo eneo kuna eneo la jeshi lakini eneo hilo wanajeshi wamekodisha kwa watu binafsi na sasa huyo mwananchi ambaye alokodishwa ameweka mashine zile pampu zinafika 9 kwa sasa hivi maji hakuna yamekauka katika chemchem ile. Kwa hivyo naiomba sana Mamlaka ya Maji ZAWA ikafanye ziara pamoja na mimi twende tukaone na tuhakikishe kwamba wanapewa taaluma nyengine na kuhakikisha wanaendeleza mradi wao wa matikiti.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Wizara ya Ujenzi naomba sana Mhe. Waziri wa Ujenzi watekeleze zile ahadi ambazo walizotoa viongozi wetu na Maraisi wetu ambao waliopita mwanzo na walioko sasa ili kuhakikisha ahadi zile zinatekelezwa. Kwa mfano, kwenye jimbo langu la Kiwengwa kuna barabara inayotoka Pangeni kuelekea Kitope, barabara ile ingewasaidia wananchi hususan kina mama wajawazito wanapotaka kwenda hospitaliya Kitobe kwenda kujifungua badala ya kupitia eneo la Kinyasini kuepuka madaraja mabovu yaliyopo Kitope wangeweza kupita *shortcut* katika njia ile kwa ajili ya kufika sehemu husika kwa haraka. Namuomba sana Mhe. Waziri wa Ujenzi ahakikishe kwamba ahadi ile inatekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye masuala mazima ya mazingira. Mazingira yetu sasa hivi yanaharibiwa sana, hususan katika maeneo wanayochimba mchanga. Kuna baadhi ya maeneo ambayo siyo rasmin wananchi wetu wanachimba mchanga lakini hawatizami hapa labda kuna nyumba au kuna nguzo ya umeme, lakini pia yanatuletea athari wakati wa mvua. Wakati wa mvua za masika, haifiki wiki unasikia kuna tukio limetokezea, watoto wetu wamezama katika maji. Kwa hivyo naomba sana Wizara husika ihakikishe kwamba ipitie katika maeneo yale na kuangalia vizuri kwa kina kabisa na kuhakikisha kwamba wanaweka mikakati ambayo inaweza kutatua na kuondosha kabisa kero hii ya uchimbaji wa mchanga kiholela.

Kwa haya machache Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba naunga mkono hoja hii, lakini pia naamini kwamba yakitekelezwa haya maoni ya ambayo waliyotoa Wajumbe wa Kamati hii naamini kwamba utekelezaji wake utakuwa mzuri na wananchi wetu wataweza kufaidika na Wizara hizi zote mbili. Ahsante sana nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Mussa Foum Mussa:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kupata nafasi hii ya kuchangia. Kwanza na mimi niipongeze Kamati ya Mawasiliano kwa hotuba yao nzuri ya yenye muelekeo wa mafanikio.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo na mimi nianze kuchangia na kuanza na Wizara hii ya Mawasiliano. Kwanza niipongeze kwa kutujengea barabara nzuri sana kutoka Mgagadu mpaka Kiwani na imemalizika vizuri. Kwa muda mkubwa sana tulikuwa tunapata shida kwa barabara ile lakini Mwenyezi Mungu amefanya rehema zake hivi sasa imemalizika na lilobaki ni kumsubiri Mhe. Rais na kupanga siku ya kwenda kuifungua.

Mhe. Naibu Spika, baada ya shukurani hizo vile vile niseme kwamba tuna tatizo katika barabara yetu ya Mwambe Mtambile. Tatizo lilokuwepo pale kwanza barabara ile ujenzi wake ulikuwa sio mzuri na kwa wakati huu barabara ile kiufupi inaendelea kumalizika. Kwa hivyo nadhani tungeliiomba Wizara ikaiona barabara ile na ikaifanyia matengenezo kabla ya kumalizika. Vile vile niseme kwamba katika ujenzi wa barabara ile kuna vipando vilivyoharibiwa vya wananchi na kwa muda mkubwa sana tokea ilipojengwa barabara ile mpaka hii leo bado wananchi wale hawajalipwa. Naiomba Wizara kwa makusudi ione huruma juu ya wananchi kwa sababu wameshakaa muda mkubwa wawalipe pesa zao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoka hapo niende suala la maji (ZAWA) kwanza niipongeze kwa jitihada yake kubwa inayochukua katika kuwapatia huduma hii wananchi wetu. Lakini mimi niseme vile vile katika jimbo langu la Kiwani nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwamba katika shehia zetu za Jimbo la Kiwani hakuna shehia ambayo kuwa haijapata maji isipokuwa kuna shehia mpya iliyoanzishwa hii ndio bado kuna tatizo la maji na shehia ya Chole. Hawa Chole walikuwa wamechukua maji kutoka Kengeja na Kengeja ndio sehemu inayotoa maji ya Shehia nyingi lakini Kengeja yenyewe ina matatizo ya maji kwa sababu visima vimechimbwa lakini mpaka hii leo bado na havijaanza kufanya kazi.

Sasa nadhani tungeliiomba ZAWA wakajitahidi na sisi wakatufanyia makusudi kwa sababu wananchi wetu wa Chole wametandikiwa mabomba kwa muda

mkubwa sana, lakini maji bado hawapati. Sasa tunaiomba Wizara ifanye jitihada tupate maji. Suala la shehia yetu ya Mtangani kama juzi nilivyouliza swali na Mhe. Waziri wakatueleza kwamba tuna mategemea makubwa bajeti inayokuja hili suala kutekelezwa, kwa hivyo tunaomba walitolee macho vizuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo niende kuzungumzia kidogo suala la ZECO. ZECO nayo tuipongeze kwa jitihada yake kubwa ya kutusambazia umeme. Lakini ZECO imekuwa na deni, inadaiwa na deni hili limekuwa kubwa la siku nyingi ingawaje na ZECO nayo inadai. Mimi ningeishauri serikali kwa vile deni limekuwa kubwa bilioni 63 i deni kubwa na la siku nyingi. Mimi ningelishauri Serikali yetu ya Zanzibar ikakaa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wakalizungumza suala hili, wakafika pahala hili deni wakasameheana wakaanza ukurasa mpya.

Mhe. Naibu Spika, deni ni la siku nyingi na inawezekana kila tukenda mbele linazidi. Ni vyema hili deni likatafutiwa ufumbuzi wa kusameheana kwa vile zote ni Serikali zetu hakuna jambo lisilozungumzika. Iko haja ya kukaa pamoja Serikali mbili likazungumzwa hili suala la deni, likasamehewa tukaanza ukurasa mpya tena hapo sasa pasiwekezwe madeni mengine yakaja yakatokea vile vile kama lilivyoanza hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya suala hilo niende katika ZURA naomba ninukuu kwenye suala hili nanukuu kwenye ukurasa wa 11 Changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) naomba niisome hii nambari 4.

"Tozo la ada ya Bandari ya Dar-es-Salaam kwa mafuta yanayokuja Zanzibar huwa kubwa tofauti na yale yanayokwenda nchi jirani ambayo hutozwa dola tatu kwa kila lita moja, wakati yanayokuja Zanzibar hutozwa Zanzibar dola kumi kwa kila lita moja"

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa nataka niulize kwamba yale mafuta yanayokwenda nchi jirani yanatozwa dola 3, lakini yanayokuja Zanzibar yanatozwa dola 10 kwa sababu gani na hii ni nchi moja. Tumeungana vizuri wa iwe ni bora wale tuliokuwa hatukuungana nao wao wanapata unafuu kuliko sisi tulioungana unafuu haupo. Hebu Mhe. Naibu Spika, hili suala naomba lizungumzwe namuomba Mhe. Waziri na yeye atakapokuwa anachangia suala hili hebu atupe maelezo kwa nini, kuna nini. Ili na sisi tupate tujue pengine kuna kitu cha msingi lakini hatukijui.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo vile vile niende kuzungumzia nyumba ya maendeleo iliyokuwepo Kengeja. Mhe. Naibu Spika, kamati imekwenda kuangalia nyumba hii na katika ripoti yao wameeleza kwamba nyumba hii ipo katika hali mbaya. Hii ni kweli nyumba ile ipo katika hali mbaya na bado wananchi wetu kuishi, mandhari yake sio mazuri. Sasa naiomba wizara husika ile nyumba iangaliwe vizuri na ipate matengenezo ya ziada kwa sababu ipo katika hali mbaya.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba na mimi vile vile niseme kwamba naiunga mkono hotuba hii ya Kamati ya Mawasiliano mia juu ya mia. Ahsante sana.

**Mhe. Masoud Abrahman Masoud:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema. Kwanza nimpongeze Mwenyekiti, wa Kamati hii ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kwa hotuba yake nzuri ambayo kaitoa mwenyewe anasema kwa muda mdogo lakini ni muda mrefu kidogo. Tumpongeze sana yeye pamoja na Kamati yake.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze moja kwa moja na Mamlaka ya Maji (ZAWA) mimi niseme tu kwa upande wangu nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri ambao wanaifanya ya kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata maji safi na salama. Kwa kweli maji ni kitu ambacho kila siku na kila binaadamu na viumbe vyengine vyote vinahitaji vipate maji. Jitihada kubwa inaonekana lakini kama walivyosema wenzangu bado tatizo hili ni kubwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye suala hili kwa lile eneo ambalo linanigusa la jimbo langu. Jimbo la Bububu ni pamoja na Shehia ya Dole pamoja na Mbuzini, Shehia ya Kizimbani pamoja na maeneo mbali mbali ya jimbo hilo. Eneo la Mbuzini kwa muda mrefu sasa upatikanaji wa maji umekuwa haupo kwa yale maji ya ZAWA isipokuwa wananchi wenyewe wamechimba visima vyao ambavyo wanatoa kwa ule wakati ambao wanaohisi wenyewe unafaa.

Nimuombe Mhe. Waziri kwa vile pale kipo kisima cha Ras el Khaimah, kasema visima 17 tayari vimeshafanya kazi kati ya visima 150 niombe kisima cha 18 kiwe hicho cha Mbuzini ili wananchi wangu wapate kufaidika. Naamini Waziri huyu ni msikivu, na bahati nzuri anatoka kwenye Jimbo langu la Bububu, kura yake alinipatia, kwa hivyo na wananchi wa jimbo la Bububu atawaunga mkono hasa eneo hilo la Mbuzini.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo eneo langu la Dole, upatikanaji wake wa maji umekuwa ni mdogo sana hasa eneo la Kiwambangoma. Niseme tu kuwa eneo lile yapo maji mengi ambayo yanatoka ya ZAWA eneo la Kianga, kuna *stop cook* ikifunguliwa eneo la Dole huwa wanapata maji. Nimuombe Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake tuwende angalau siku moja tufungue dakika 10 aone watu wa Dole watakavyofaidika kwa maji safi na salama.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende katika sekta ya Idara ya Usafiri na Leseni. Sekta hii ni nzuri na inatusaidia baadhi ya maeneo ilikuwa daladala hazifiki sasa hivi wameziruhusu zinafika. Niishukuru Idara hiyo waliniruhusu kutoa daladala Darajani kwenda mpaka Dole mtambo wa Redio, nimuombe sana Mkurugeni kwa heshima na taadhima bado wananchi wa eneo la Kizimbani wanapata tatizo la usafiri. Daladala hii inayotoka Darajani tuhakikishe inafika mpaka Mndu, watafaidika askari ambao wanafanya kazi Magereza, watafaidika wafanyakazi wa Idara ya Kilimo ambao wanakwenda Kizimbani, lakini pia watafaidika na wananchi wetu pale, kwa sababu kutoka Mtambo wa Redio Dole mpaka Mndu ndio Cente pale kuna soko letu nalo litapata kuimarika. Tusije kuwakatalia kufikisha pale Mndu, tuwaombe sana Mhe. Mkurugenzi aturuhusu ili daladala zifike mpaka pale Mndu.

Mhe. Naibu Spika, niende kwanye Idara ya Mipango Miji, bahati nzuri, idara hii ni idara ambayo ina kazi kubwa sana, lakini kwa muda mrefu tuna ombi letu la kuhakikishiwa tunapatiwa kituo kikubwa cha daladala eneo la Kwanyanya. Eneo lile kwa muda mrefu sasa hivi kila baada ya siku tatu huwa zinatokea ajali. Niombe sana Idara ya Mipango Miji japo ruhusa ya muda kiwekwe kituo cha daladala kilichokuwa sio cha kudumu lakini kihakikishwe pale kunakuwepo na kituo yaani Halmashauri watie kifusi angalau pale magari yawe yamepata kuweka *packing*. Kwa sababu sasa hivi watu wanapata ajali kila baada ya siku tatu kwenye eneo lile lakini kwa muda mrefu wanatwambia tuko katika mipango kituo kitawekwa lakini bado hilo halijafika kwa hiyo tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuambilie lini atatoa ruhusu ya kuwekwa kituo cha mle cha daladala.

Mhe. Naibu Spika, halmshauri ya Wilaya ya Magharibi 'A' sasa hivi imekuwa Manispaa mji wetu mkubwa uko katika maeneo ya Bububu niombe Mkurugezi wa Idara ya Miundombinu angalau kwenye eneo letu la mji wa Bububu kwenye *site* fulani pale zipatikane angalau njia za lami iwe na sisi tunasema Manispaa yetu iko Bububu na Bububu angalau kumepatikana japo barabara moja ya lami ambayo inaingia katika eneo letu.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende kwenye urajisi wa maeka Idara ya Ardhi, Mheshimiwa sasa hivi kumekuwa na tatizo ambalo sasa hivi limekuwa kubwa na kama Serikali watalichunguza vizuri basi Mhe. Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya lakini pia na Idara ya Ardhi ifanye kazi ya kulitafuta. Mhe. Sheikh Abeid Amani Karume Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema alifanya kazi ya mapinduzi mwaka 1964 kwa kuwakomboa wanyonge na akagawa heka tatu kwa kila mwananchi wakati ule aliyepata bahati hiyo, lakini kwa bahati mbaya sana Mhe. Naibu Spika, sasa hivi eka zile zilikuwa zinaitwa shamba sasa hivi tumegaiwa imekuwa maheka lakini imekuwa kinyume sasa hivi kuna watu Idara ya Ardhi wanazifanya tena kuwa mashamba natumai kiswahili changu kimefahamika. Zilikuwa shamba, zikawa heka, sasa hivi zinageuzwa tena zinakuwa mashamba zinarudi kule kule zilikotoka nia ya Serikali ziwe heka lakini sasa hivi zinageuzwa tena kuwa mashamba wale wanyonge akina Masoud sasa hivi wanazipiga mnada zinarudi kwao kwa hiyo, niombe Serikali kwenye hili walitambue itafikia wakati maheka watakuja kuyatafuta yatakuwa hayapo tena.

Nikondoka hapo niende Shirika la Umeme ZECO Mhe. Mwenyekiti nimpongeze Mkurugenzi pamoja na *team* yake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya Meneja Mkuu sio Mkurugenzi, Meneja Mkuu kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kuhakikisha wanatusaidia upatikanaji wa umeme katika maeneo yetu hasa maeneo ya vijijini, wenzetu walioko mjini sasa hivi hawahitaji nguzo za umeme lakini nimuombe tu yale maeneo ambayo bado umeme haujafika watusaidie ili kuhakikisha umeme unafikishwa vijijini humu.

Lakini mwenzangu hapa kazingumzia suala la madeni, madeni bilioni 63 ni nyingi sana na kila siku bado zinaongeza nimuombe Meneja Mkuu pamoja na wenzake wafanye utaratibu angalau kuziongeza zile mita za TUKUZA ili kupunguza hili deni kama mita za TUKUZA itakuwa tunafungiwa itakuwa deni haliongezeki kwa sababu ni sisi tuliomo humu na walioko nje ndio tuliokuwa hatulipi deni likafikia hiyo bilioni 63.

Mhe. Naibu Spika, deni hili naamini hapa linatajwa wanaodaiwa ni Shirika la Umeme lakini Taasisi zote za Serikali zinadaiwa katika hizo bilioni 63 kwa hivyo, niombe hao wanaodaiwa walipe na sisi tuliomo humu ndani tulipe na Taasisi za Serikali zilipe ili deni hili lipunguzike na baadaye ndo tukafanye mazungumzo na wenzetu ili deni liweze kusamehewa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi niunge mikono ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kwa asilimia tisini na tisa. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa mchangiaje anayofuata ni Mhe. Tatu Mohammed Ussi atafuatia Mhe. Omar Seif Abeid kama muda utakuwa unatosha.

**Mhe. Tatu Mohammed Ussi:** Ahsante Naibu Spika, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia wakati huu kusimama hapa ili na mimi niweze kuchangia, pili nikushukuru kwa kunipa nafasi kwa kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu moja kwa moja utakuja kwenye sekta ya mawasiliano kwenye suala zima la kampuni ya simu za mkononi. Mhe. Naibu Spika, Kampuni ya Mawasiliano ilibororesha mawasiliano kwa ajili ya wananchi wake ili kupata mawasiliano ya karibu na yalio bora zaidi, lakini cha kusikitisha Mhe. Naibu Spika, kampuni hii ya simu za mkononi hususan Kampuni ya simu za ZANTEL sasa hivi ina wananchi ambao baadhi yao kampuni hii wanaitumia vibaya kwa kuwatapeli wananchi na hususan wanaotapeliwa ni sisi wanawake.

Mhe. Naibu Spika, kampuni hii saa hivi inawapigia watu simu na kuwapa mambo ambayo hawanayo wanaweza kupiga simu wakakwambia kuna mtu wako kapata ajali na sasa hivi zinatakiwa pesa kwa hivyo kwa yule mtu ambaye ni mwepesi basi anakuwa pesa zile anazitoa. Lakini vile kuna matapeli wengine Mhe. Naibu Spika wanawapigia watu simu na kuwaambia kuwa sijui mimi ni mganga miye niko hivi kwa hivyo kuna matatizo unatakiwa utowe pesa, sasa kuna wengine wanakuwa hawatowi lakini kuna wengine Mhe. Naibu Spika wameshatapeliwa kutoka na simu hizi za mkononi na hata ukienda huko kwenye ofisi yao basi inakuwa ni vigumu kupata mashirikiano kuwa watakwambia ni namba fulani na namba utaipeleka lakini mashirikiano yanakuwa hayapatikani.

Mhe. Naibu Spika, miye nalisema hili kwa ushahidi kwa sababu wako wengi ambao wametapeliwa na kuna wengine wamepigiwa simu hata mimi mwenyewe binafsi nilipigiwa simu lakini kwa bahati hawakunipata lakini walinipigia simu mbili na baada ya kunipigia simu hiyo moja walipoona hawapati walibadisha namba nyengine. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naiomba wizara husika ilifuatilie wizara hii kwasababu kuna watu wengine ni masikini na wengine wanasema kuwa kuna watu wamepata ajali wakapeleka pesa lakini ukifuatilia inakuwa si kweli Kwa hivyo sasa ni kulitia aibu Shirika hili la simu nakutufanya simu za ZANTEL tusitumie Mhe. Naibu Spika, hili namuomba Mhe. Waziri anayehusika alifuatilie Shirika la Simu.

Lakini jengine Mhe.Naibu Spika nakuja kwenye Shirika la Meli ya Uwakala kwa Zanzibar na nitaingia kwenye sehemu ya uuzaji wa tiketi Mhe. Naibu Spika miye ninavyuojua kwamba meli zote zina kiwango chake cha kuchukua abiria na kuchukuliwa kwa abiria ina maana inategemea na tiketi zitakazouzwa lakini la kushangazwa Mhe. Naibu Spika kuna siku nyengine za kipindi cha meli hususan kipindi cha Disemba na kipindi cha Januari utakutia Shirika hili linauza tiketi zilizo nyingi ambazo husababisha abiria kuachwa pale bandarini.

Sasa Mhe. Naibu Spika, miye huwa najiuliza inakuwaje kuuzwa tiketi namna ile na watu wakachwa pale bandarini na ukienda pale pwani utakutia watu mtu mmoja ana tiketi 10 mikononi anauza, sasa huwa najiuliza zile tiketi huwa 10 mpaka 20 ndani ya mikono wanauza anakuwa anazipata wapi. Sasa Mhe. Naibu Spika hili naiomba wizara ilifatilie kwa sababu tatizo kubwa na linalonisikitisha mimi hutoka mtu nyumbani kwake asubuhi ana vitoto vichanga amekuja pale halafu akaambiwa kama wewe huingii melini, sasa hili ni tatizo na linatusumbua hususan sisi wanawake tunaosafiri na watoto. Kwa hivyo naiomba wizara husika iliangalie suala hili la uuzaji wa tiketi bado Shirika hawajaweza kulidhibiti hili. Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo ilikuwa nizungumzie suala zima la maji lakini kwa bahati wenzangu wameshalizunguza sina haja ya kuligusa lakini Mhe. Naibu Spika, suala la maji wameshalizungumza kwa hivyo sina haja ya kurudia

Jengine Mheshimiwa suala la nyumba Mhe. Mussa kagusia suala la nyumba za Kengeja lakini pia si Kengeja tu kamati iangalie na nyumba nyengine kama zile za pale Mkoani wakati mwengine kwa sababu na nyumba zile nazo zinahitaji matengenezo. Kwa hivyo baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, sitaki niende sana kwa sababu niwape wenzangu nafasi naounga mkono Ripoti ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa mchangiaje wetu wa mwisho una dakika kumi kamilifu Mhe. Omar Seif.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Mhe. Naibu Spika, dakika zimeshapunguza lakini haya twende *Bismillah*.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa ufupi lakini Mhe. Naibu Spika, mimi naanzia na *page* namba 5 *page* namba 5 iliyozungumza suala la usajili wa ardhi, kwamba kuna viwanja miongoni mwa viwanja vilivyosajiliwa kuna viwanja 94 vimesajiliwa kwa ajili ya mahoteli. Lakini nilitaka nijue katika hivi viwanja hii mikataba 20 iliyotolewa kwa ajili ya

viwanja vya uwekezaji mpaka sasa ni viwanja vingapi au ni wawekezaji wangapi ambao wamepewa hati za umiliki wa haya maoneo kwa ajili ya mahoteli ambayo wameyaendeleza na ni wangapi ambao hawajayaendeleza. Sambamba na hilo wenzangu wameelezea sana kadhia ya ardhi hususan kwa viwanja suala la viwanja mimi nafikiria kwa sababu sheria tuliitunga wenyewe na imepitishwa kwenye Baraza la Wawakilishi. Si vyema wala si busara ikawa sheria tunazozitunga tunazirejea kinyume kwa sababu kwenye hiyo hati au mkataba wa utumiaji wa ardhi wenyewe unaeleza nyuma ukiufungua muda ambao unamtaka mtu aliyepewa hati ya matumizi ya ardhi aweze kuitumia na kuiendeleza. *(Makofi)*

Jambo hili mimi nafikiria turudi kwenye sheria tuitizame sheria inasemaje lakini pia Mheshimiwa mimi nilikuwa naunga mkoni hoja za wenzangu kuhusu maeneo ya uwekezaji kwamba wawekezaji wanapokuja hapa kuwekeza, wanakuja kwa lengo maalum la kuwekeza lakini inaonekana baada ya kupewa ardhi wengine hawazitumii kwa lengo hilo ipasavyo wanachukua muda mwingi kuliendeleza, kwa hivyo Serikali inakosa mapato na wananchi pia halikadhalika.

Lakini pia kumetajwa Idara ya Mipango Mji kwa sababu kumekuwa na matatizo mengi katika matumizi bora ya maeneo ya wazi katika maeneo ya miji yetu, pia mimi nilitaja kujua jee kwanini au ni lini Idara hii Mpiango Mji itaweza kudhibiti matumizi holela au mabaya ya maeneo ya wazi katika mji yetu. Kwa sababu mji mingi imepimwa na inaonekana kuna watu wanakuwa hawataki kufuata sheria lakini pia si sheria tu waliokuwa wanaiopinga pale lakini usimamizi wenyewe unaonekana ni hafifu kwa sababu kabla ya kujenga kwenye hayo maeneo ya wazi au kuyatumia kunataratibu zinazotakiwa zifuatwe ikiwa pamoja na kupewa kibali na halmashauri, halmashauri wao lazima wanatakiwa wawe wanajua.

Mheshimiwa sasa hivi tumeshuhudia maeneo ya wazi kama matumizi ya *reserve* ya barabara yanatumika vibaya hata maeneo ya skuli sasa hivi utazikuta skuli nyingi zimezungushwa vibanda vinajenga mambo haya hayaleti twasira nzuri. Je, ni utaratibu gani unatumika kuyamiliki maeneo haya ili yasiendelee kutumika vibaya na yatumike kwa lile lengo tu tunalokusudiwa kwa sababu sehemu za biashara zinatakiwa zitengwe na zimetengwa zipo lakini cha kushangazwa ni kwamba watu wanaondoka kule walikotengewa katika biashara wanaingia katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mimi naishauri natoa ushauri wangu kwamba wizara ikishirikiana na Idara ya Maalum Tawala za Mikoa hawa watu wa Halmashauri na Manispaa waanze

utaratibu mahsusi wa kuwaondoa watu wote wanaotumia maeneo ya wazi ambao yametengwa kwa matumizi ya umma, pia nikiondoka hapo naenda nitaenda kwenye Idara ya barabara. Idara ya barabara nilikuwa nazungumza siku nyingi nimelizungumza jinsi ya matumizi mabaya ya barabara lakini sijui kwa nini lile lengo zima la kuwa na vituo vya barabarani imepotea ile dhana haipo ni kwamba sasa waendesha madaladala mtu anaamua kusimama anapotaka anashusha abiria na anachukua abiria pale pahali anapotaka bila ya kujali usalama wa barabarani. Jambo hili ni hatari linahatarisha si hatari tu kwa wenye magari pia kwa wapita njia ambao wengine wanatumia barabara ni vilema, vipofu, ambao hawaoni. Mimi nashauri kwamba

**Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis:** Mhe. Naibu Spika kwa utaratibu

**Mhe. Naibu Spika:** kuhusu utaratibu

**Utaratibu**

**Mhe. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis:** Nimuombe mjumbe atumie lugha ambazo zinakubalika na watu wenye ulemavu hakuna mtu mwenye ulemavu anayeitwa kipofu wala kilema *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa nafikiri umefahamu

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Nashukuru mheshimiwa kwa kunikumbusha naomba samahani kwa hilo..

Barabara za watu wote si za wenye magari tu kama alivyosimama Mheshimiwa akaniambia na nAshukuru nimesahau kwamba barabara zina watu wenye mahitaji maalum wengi wanaozitumia barabara. Sasa leo mwenye daladala anathamini shilingi mia tatu kulikoni kuthamini maisha ya mtu. Mimi natoa wito tena kwamba ule utaratibu wa kurejesha vituo uendelee kutumika ili kwa usalama wa watumiaji. Mimi Mheshimiwa nazungumizia hii nikitoa mfano barabara ya Bububu, barabara ya Bububu jinsi ilivyo lakini utakuta wenye madaladala pamoja na kuwa vituo vipo lakini wanaviacha vituo wanasimamisha magari na wanapakia abiria na kuteremsha mahala popote.Bila ya kuangalia barabara ile inatumika kiasi gani wingi wa magari uliopo msongomano uliopo lakini na wao ndio wanayongezea mzigo ile barabara lakini tuwaombe askari wa barabarani waendelee kwa kuwakamata na wakamate, naiomba ile sheria ya faini ya papo kwa papo ianze kutumika, itakapotumika mimi naamini kwamba mambo mengi yatakaa sawa juu ya usalama wa barabarani. Itaweza kutupunguzia tatizo hili na wenye madaladala

na wale madereva ambao si waangalaifu barabarani watachuka tahadhari lakini pia nachukua fursa hii kuipongeza Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa malizia una dakika moja

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Kwa kuanza kuweka *CCTV Camera* barabarani, jambo hili litatusaidia sana Mhe. Waziri na wizara yako hongera lakini zisije zikakulevya. Tufanyeni kazi kwa ajili ya usalama wa raia wetu, Mheshimiwa tuna mengi lakini mengine nitawasilisha kwa maandishi. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nimeombwa niwakumbushe leo baada ya kumaliza kikao tunatakiwa wajumbe wa Chama cha Mapinduzi kukutana juu kwa ajili ya uchaguzi wa mjumbe wa Tume ya Bajeti na vile vile Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano ametaka kukutana baada ya kikao hiki.

Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru nasitisha kikao hadi saa 11:00 jioni

*(Saa 7.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Jioni ya leo ninaanza na Mhe. Suleiman Sarahan Said atafutiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame na Mhe. Simai Mohamed Said ajiandae.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nashukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kutia nyama katika hii Kamati yetu ya Mawasiliano.

Mheshimiwa mimi nataka niseme kwamba Kamati yetu ya Mawasiliano katika sekta ya barabara, hili suala ni kwamba nafikiria sana chanzo cha kuwekwa mawasiliano hasa katika sekta ya barabara ni kumaliza tatizo la barabara zote za Zanzibar. Mhe. Spika, katika maelekezo tuliyokuwa tukienda na katika maelekezo ambayo yanajuulikana mawasiliano ina ukosefu wa vyombo vya kutendea kazi katika sekta ya barabara.

Mhe. Spika, chombo cha kutilia lami Unguja na Pemba kinabakia kuwa kimoja, ukikuta vyombo vyengine vyote ambavyo katika sekta wanaita *set* ni chombo kimoja kimoja. Sasa nguvu ambazo tunazo, watendaji wetu sasa hivi wana

elimu kubwa sana ya barabara wameshapata uzoefu wa kutosha, elimu ya kutosha na mifano ya kutosha wameshatuonesha, kwamba wanaweza kujenga barabara nzuri sasa hivi, lakini tatizo kubwa mheshimiwa ni vifaa. Ningeomba sana tukakata pua tuunge wajihi ili kuweza kuondoa tatizo la barabara katika visiwa hivi ni kuwakabidhi mawasiliano vifaa vipya na vya kisasa vya barabara.

Mhe. Spika, tumeshatembelea barabara nyingi ikiwemo ya Mgagadu/Kiwani tumeona jitihada za wenzetu hawa wanavyofanya lakini nusu wanafanyia mkono, nusu wanafanyia mashine iliyochoka. Nina uhakika pamoja na maneno maneno yanayosemwa kwamba hawana viwango vya barabara, lakini nina uhakika barabara haipimwi kwa mkono, barabara inapimwa kwa vifaa. Hii sekta Mheshimiwa ni sekta muhimu, ni sekta ambayo kwa kweli kila siku hata katika Ilani zetu, katika ahadi zetu suala la barabara ni la kwanza tunalolitolea ahadi. Muarubaini wake nakuhakikishia kwamba tukipata vitendea kazi vizuri basi suala hili linaweza kupungua kwa asilimia 70% ili tukaweza kunufaisha wananchi wetu. Lakini pia nina uhakika kama tuta-*save* pesa nyingi sana. Hii yote ingekuwa tuna vifaa hivi tusingekuwa tunaingia kwenye mikataba mibovu mengine ya barabara ambayo watu wanatuacha nayo njiani. Kwa hivyo, ningeshauri sana katika jambo moja ambalo nilikuwa naliona kwamba serikali itapiga hatua sana ni kuwapatia mawasiliano katika sekta ya barabara vifaa vyao vya kutendea kazi Unguja na Pemba. Hilo moja nilikuwa nichangie.(*Makofi*).

Mhe. Spika, la pili nakuja kwenye sekta ya maji. Mheshimiwa maji imetoka mbali sana, katika vichwa vya watu maji hakuna sekta ya kulipa, katika vichwa vya watu maji ni kitu ambacho hakikosekani lakini haya sio yalivyo hivi sasa, lazima tukubaliane na hali halisi inayojitokeza katika mazingira ya nchi yetu. Kila mmoja anafahamu vipi tulivyokuwa tunapata mvua katika nchi hii, sisi tulikuwa na miongo ya mvua na ya kilimo, leo miongo ile yote imepotea, miongo ile haiendani na kilimo tu inaendana na maji.

Mhe. Spika, maji kiutaalamu ukitaka kuyatizama hujui kwenye ardhi yanatoka vipi, lakini ile ni rehema yake Mwenyezi Mungu. Sasa tujue kwamba maji ikiwa mvua hazipo basi huko chini yanazidi kupotea, ukiachia vyanzo vya maji ambavyo Mheshimiwa hatujui gurudumu hili tumtwike nani, maana yake kila mmoja anakukuta mkono si la kwake. Mheshimiwa vyanzo vya maji tumevikagua watu wanajenga mpaka karibu, watu wanakata misitu mpaka karibu mwenyewe ni nani hajuulikani, watu wanakuja kuja tu mwenyewe nani hajulikani.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri sana mambo mengi haya sasa hivi kama hayajapata nguvu kwa nguvu basi hayendi. Mheshimiwa tungeshauri kwamba hizi Mamlaka zetu nyengine wakati mwengine tuzitilie nguvu kwa kuwasaidia kwa Vikosi, maeneo ambayo hayahitajiki kujengwa basi yakatolewa amri maalum kwamba maeneo haya hayaruhusiki. Lakini tunayatizama halafu tunakaa tunalalamika, sasa wakumlamu nani maji yale yakitoweka. Kwa hivyo, ningeshauri sana Mamlaka hii ya Maji ikasaidiwa nguvu pamoja na jitihada zake zote lakini tutachimba visima mpaka mwisho tuachimba ndani ya nyumba hayapatikani maji kutokana na kwamba matatizo ya maji tunazungumza katika sekta za watu kwamba unapojenga sana maji yanakimbia.

Mhe. Spika, Zanzibar haikuwa na historia hii ya kujengwa sana, Zanzibar ilikuwa tujenge padogo tulime pakubwa, tubakishe mito, mabonde na kila kitu. Lakini leo Zanzibar ina inajengwa mpaka ndani ya mito hivyo maji yanapotea. Mhe. Spika, maji si kitu cha mzaha tutakuja kuyatafuta maji kama tunavyotafuta mchanga sasa hivi, mwisho tutaagiza maji kutoka Bara. Kama hatukuweza kulinda mito yetu na vyanzo vyetu tukaviacha hatari inakuja. Kwa hivyo, hilo nilitakiwa nilitolee indhari ambayo ipo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi nataka niseme pia upande wa ardhi kidogo. Mheshimiwa upande wa ardhi kauli nyingi zinatoka za serikali, lakini ama ufuatiliaji wake, ama amri zile husahaulika na mwenye amri zile hakumbushi baadae tunaitia serikali katika matatizo ama ya kulipa, ama ya kumtafutia mtu hasara yule ambaye kishafanya mambo makubwa. Mheshimiwa kwa jicho langu nimekwenda Mangapwani ni pahala ambapo pametengwa kwa *reserve* ya mafuta ni pahala pekee labda palishatengwa na serikali kwamba pahala pale katika sekta ya mafuta na gesi ndio iwe mradi wake.

Mhe. Spika, lakini sijui nani sasa ame-*sign* kuwapa wengine mikataba, tumewaachia kuna watu wasiopungua wanne wenye maeneo makubwa wameshajinufaisha pale pahali, wameshajitandawaa kumuondoa ni kazi kweli kweli. Sijui ataondoka vipi maana yake ukisema umpigie thamani ya kuondoka hana nyumba, pana eneo hata sijui nikwambie kafanya nini, ukimwambia abakie ina maana ile dhana nzima ya serikali imeshapotea. Hawa waliotoa viwanja hivi ni nani na amri ilishatoka? Hivyo kweli ndio hatuwajui lakini tunafumbwa macho na mwengine akija atafanya vile vile. Kwa hivyo, inaonekana amri ya serikali haiheshimiwi tunaitia serikali hasara siku hadi siku. (*Makofi*).

Mhe. Spika, sasa hivi watu kila aina ni watu wa ujanja ujanja sote tunaishi kwa ujanja ujanja, lakini ujanja mwengine unachangiwa na watendaji. Mheshimiwa

mtu akigutuka na kitu tu anamwambia mtu pesi kafanye kitu fulani pale tutapata pesa. Mimi naona kama tungekuwa na mradi maalum wa kuipima hii Zanzibar na kuweka vitu vyake maalum, basi tungetangaza na sera kwamba sisi hatutolipa mtu yeyote tungeona mtu atajenga pale ambapo amekatazwa. Lakini sasa hii sera yetu ni kwamba tumpe fidia, mheshimiwa anaweka matufali mawili anataka milioni mia moja, tatizo linakuja hapo na serikali yetu ni serikali ya sheria. Sasa ningeshauri sana watendaji tusiitie serikali katika matatizo makubwa inakuwa hatufiki tunatenga barabara ukitizama tunasubiri kuwalipa wanaodai vifaa vyao au nyumba zao kwenye barabara hiyo barabara inavyojengwa hiyo thamani yake tunalipwa mara kumi ndio utengeneze barabara. Kwa hivyo, pesa zile zinazolipa majumba ya watu tungeweza kutengeneza barabara nyengine mbili au tatu kuliko vile. Lakini Mhe. Spika, haya yanafanyika. Lakini ningeishauri serikali basi yaliyopitwa si ndwele tugange yajayo hasara kama hizi tuondokane nazo pahala tunapataka tupapime kabisa na tuweke mstari mwekundu. Lakini sasa tunakaa wee! tunakuja kama kushtukiza, si pesa kidogo zinazopotea mahospitali humu hali ni ngumu zinatakiwa pesa zinakwenda kupotea kwa watu bure kwenye wajanja wajanja…

**Mhe. Spika:** Muda mheshimiwa malizia.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Ahsante mheshimiwa.

Mhe. Spika, pamoja na yote mimi nataka niseme kwamba bado naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein ambapo kwa kweli lazima tukubaliane kwamba hatua tuliyopo kama tunakwenda kwenye mia basi tuko kwenye sabini. Kwa hivyo, tukijikaza watendaji na wananchi wote kwa pamoja basi tutafika tunakokwenda Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Nashukuru sana Mhe. Spika.(*Makofi*).

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa sasa ninamwita Mhe. Hidaya Ali Makame atafutiwa na Mhe. Simai Mohamed Said na Mhe. Mwantatu ajiandae.

**Mhe. Hidaya Ali Makame:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi kuweza kuchangia katika Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Spika, kwanza na mimi nianze kwa kukushukuru wewe kunipatia nafasi hii, lakini niwapongeze pia Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati

kwa kazi yao nzuri ambayo wameifanya na kuweza kutuwasilishia leo ripoti yao hii yenye mvuto na changamoto nyingi ndani yake.

Mhe. Spika, kwa kuanza na mimi moja kwa moja nianze kwenye Ofisi ya Wizara ya Maji, Nishati na Ardhi. Mhe. Spika, moja kwa moja kwenye ofisi hii nitaangalia suala kubwa linalohusu ardhi. Mhe. Spika, wana Kamati wameweka changamoto nyingi ambazo zimeikabili hii Mamlaka ya Ardhi, lakini pia imekabiliwa Mamlaka ya Maji pia nayo ina changamoto nyingi ambazo wana Kamati wameziorodhesha hapa. Katika changamoto hizi wametwambia kwamba kuna changamoto ambayo imeikumba hii Mamlaka ya Ardhi kwenye suala la vianzio vya maji.

Mhe. Spika, vianzio vya maji kweli kwa sasa ni changamoto kubwa katika nchi yetu, tumeona kwamba vianzio hivi vya maji vimekabiliwa na mzigo mkubwa wa wajengaji nyumba ambazo hazina mpangilio maalum. Nyumba hizi zinajengwa kwenye vianzio vya maji bila ya mtu kutizama, bila ya mtu kupima ile sehemu lakini bila ya kufuata ushauri na maelekezo yanayotakiwa kwa ufasaha.

Mhe. Spika, lakini tukiangalia kwa undani zaidi suala hili niweze kusema kwamba baadhi ya wahusika wanaweza wakachangia kwa asilimia moja wapo. Kwa sababu kama unakwenda kununua kiwanja sehemu basi huwezi kuuziwa kiwanja kama Halmashauri haijafika pale, kama Kamati ya Sheha haijafika pale lakini na baadhi ya Wajumbe wakubwa kutoka kwenye Halmashauri wote wahusike ndio ndipo ukipate kiwanja kile na hatimiliki zote na uweze kujenga mpaka umalize nyumba ile. Kwa hivyo, tunaona moja kwa moja kwamba Halmashauri inahusika na ubovu huu wa kuharibu vianzio vya maji kwa kujenga nyumba holela ambazo hazina mpangilio maalum. Lakini pia kuharibu ile miundombinu ambayo inapatikana pale kwenye vianzio vya maji zikiwemo chemchem lakini na mabonde yanayosababisha kupatikana maji safi na salama. Kwa sababu tunafahamu kwamba maji safi na salama yanapatikana kwenye chemchem, na mabonde ambayo tunalima mipunga na vitu vyengine.

Mhe. Spika, kwenye Kamati hii pia wameeleza kwamba kuongezeka kwa ujenzi wa nyumba usiofuata taratibu za mipango miji. Mhe. Spika, ndio hapo hapo ninaposema kwamba hawa wahusika wa Halmashauri wawe imara na wawe makini juu ya kufuatilia suala hili la taratibu za ujenzi, pia na taratibu za ukataji wa miti. Kwa sababu mtu anapotaka kujenga ni lazima apate mawa, apate miti lakini apate mchanga na vitu hivi vyote tunajua kwamba ndivyo vinavyosababisha mmong'onyoko wa ardhi lakini pia ndivyo vinavyosababisha kukausha hizi ardhi. Kwa sababu pahali ukishapaweka nyumba hata kama pana

kianzio cha maji basi kile kianzio kinakufa na baadae panabakia jangwa na kusababisha kwamba kile kianzio cha maji kipotee lakini pia na mmong'onyoko wa ardhi utokee pale pale.

Mhe. Spika, pia niende kwenye suala la ardhi. Mhe. Spika, ardhi zinanunuliwa na tunaouza ni sisi wenyewe, baina ya mtu na mtu ndiye anayeuza ardhi na mtu mwengine ndio akanunua ardhi. Kwa hiyo, kama kuharibu mazingira sisi ndio tunaoharibu lakini jee, kutengeneza nani anapaswa kutengeneza, ndio sisi, sisi. Kwa hiyo, ningewaomba jamii yetu iliyozunguka kwamba tulione hili suala kuwa linaleta athari kubwa mbele yake na baadae tutakuja kufika hatua tukose hata yale maji ya kunywa au tukose hata ile sehemu ya kufuga wanyama wetu na kujenga pia tutakosa, kwa sababu kujenga bila ya mpangilio mwisho wa siku ndio unakuta hata ile sehemu ya wewe mwenyewe kukiweka kile kibanda chako unakosa, lakini pia kufuga wale wanyama unakosa na pia kupata kile kianzio cha maji unakosa. Kwa sababu tunaambiwa kwamba ukishaukata mti mvua si aghlabu kunyesha pahali hapo, na kianzio cha maji tunajua kwamba kinasababishwa na mvua pia.

Kwa hiyo, tuwe makini juu ya hili lakini Wizara pia ilisimamie suala hili la utoaji wa viwanja na kujenga holela, kwa sababu tunajua kwamba hivi ndivyo vinavyosababisha athari kubwa na hatimae kufikia sasa hivi anayetaka kuunga maji alipe, anayetaka kuchimba kisima alipe, anayetaka kufanya nini maji alipe kutokana na suala hili. Hapo mwanzo hayakuwepo haya ya kununua maji wala kuwekeza maji, lakini sasa hivi tunawekeza maji, tunanunua maji, tunafanya kila kitu maji kwa kutoa pesa.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye suala la umeme *ZECO*. Suala la umeme hili nalo ni changamoto kubwa kwa wananchi, kwa sababu tunajua kwamba nishati ya umeme sasa hivi ndio kila kitu kwenye maisha ya binadamu nayo ikiwemo na maji lakini na uhai wa binadamu na umeme pia. Kwa sababu ndani ya nyumba yake mtu sasa hivi haiwi nzuri hata iwe ghorofa ya kilometer 200 kama haina umeme basi atakwambia nyumba yangu haijakamilika. Kwa hiyo, umeme nacho ni kipaumbele kwa wanadamu sasa hivi lakini suala hili nalo lina changamoto kubwa hasa wale maskini wenzangu na mimi wakulima na wakwezi inakuwa ni kikwazo kikubwa.

Mhe. Spika, kwa sababu mtu huwezi kuunga umeme kama nguzo ya umeme haijafika karibu yako au mwenye umeme hajakuwepo karibu yako. Kwa hivyo, ili uunge umeme ni lazima pawe kianzio kile cha umeme kimeshafika karibu yako ndio upate umeme, lakini je, kama kianzio kile cha umeme hakijafika karibu yako utapataje hiyo fursa ya kuunga umeme, huwezi kupata. Na

ukikimbilia huko kunakohusika mashaka yaliyoko huko hayamithiliki kwa sababu kama hujakuwa na milioni zaidi ya tano hujapata umeme.

Sasa niulize umeshakwenda mbio zako umepata mikopo ya riba na nini, umeshapata kibanda chako kituturu unataka na wewe mwako muwe mweru mweru vipi utaupata umeme huo ukiwa una shilingi milioni tano, huwezi kuupata. Kwa hiyo, ningeiomba sana *ZECO* iwe na ule uzoefu wa tangu pale mwanzo wa kuzika zile nguzo za umeme kwa kuweza kuwasaidia wananchi na baadae mwananchi yule anapohitaji kuunga ule umeme yeye awe na zile purukushani nyengine za kutafuta *wire* na viti vyengine vinavyohusika ndani ya nyumba yake. Lakini kwa kumtegemea mwanchi yule masikini, hali yake duni aweze kununua nguzo pengine hapo kwake nguzo 10 zinazotakiwa ili apate umeme, nambie nguzo moja inagharimu shilingi milioni moja na nusu. Jee, mwananchi yule ataimiliki wapi pesa ile ya kuweza kupata umeme nguzo 10 mpaka afikishe kwake.

Hili kwa kweli ni mtihani na tujitahidi sana kuweza kuwasaidia wananchi wetu kuona wanaishi katika maisha bora na yaliyo imara zaidi kwa kuweza kusaidiana kwa sababu mpaka Mwenyezi Mungu katuamrisha juu ya hilo kwamba, *"Al-Muslim Waqul-Muslim Layadhwilimuhu Walanusalimuun". (Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hapa ningeomba sana wizara hizi zijitahidi juu ya kuwatendea mema wananchi wake kuweza kuwasaidia kutokana na hali walizonazo duni na hali za chini.

Mhe. Spika, nikimalizia hapo nimalizie kwenye suala la barabara. Mheshimiwa tuna barabara zetu za ndani ambazo ni changamoto kubwa kwa wananchi wetu. Barabara hizi kwa sasa hivi gari kufika tabu, lakini pia hawa wananachi wenyewe kutembea kwa miguu ni shida, barabara hizi zinatumika muda wote asubuhi, mchana na jioni.

Mhe. Spika, hapa ninaizungumzia barabara moja iliyopo Kizimbani-Bumbwisudi kutokezea Kitundu. Hizi njia zinatumika muda wote hususan njia hizi zinatumiwa na wakulima na wakwezi na wanapata tabu sana wakati wa kuvuna yale mazao yao. Kwa sababu mwananchi anajitahidi akishavuna yale mazao yake alfajiri afike Mwanakwerekwe kwenda kupata huduma ya mauzo, lakini barabara hizi unamkuta mwananchi yule ahangaike kutafuta gari ya ng'ombe mpaka afike barabarani mazao yale yameshatumbuka tumbuka, yameshaharibika, barabarani kwenyewe akishafika kwanza hiyo foleni ya gari kuisubiri masaa matatu, kwa sababu tu ya ubovu wa barabara ndio maana

zinasababisha hata zile gari zinakuwa ni shida kwenda kule kwenye ile mitaa. Kwa hivyo, tunaiomba wizara hapa itizame barabara hizi ijapokuwa kwa kiwango cha fusi tu, sifikirii kama mwananchi yule atakuwa ana lazima kwamba atiliwe lami iliyokuwa hakuna uwezo, kwanza japo lile fusi ikaweza kuziba yale mapengo yaliyokuwemo mule ndani ya zile barabara wakaweza kujisaidia.

**Mhe. Spika:** Muda Mheshimiwa.

**Mhe. Hidaya Ali Makame:** Mhe. Spika, ahsante namalizia. Kwa hivyo, naiomba sana hapa wizara ilitizame na hili suala la barabara za ndani kwa kushirikiana na Halmashauri zilizopo kwenye wilaya zetu.

Kwa kumalizia niunge mkono ripoti hii ya kamati kwa asilimia mia moja ahsante sana.*(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Hidaya Ali Makame. Sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said atafutiwa na Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajiandae.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Mhe. Spika, ahsante kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia niunganishe hapo kwa kukushukuru wewe kuweza kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu. Lakini pia niwashukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Hamza Hassan Juma rafiki yangu kwa jinsi alivyotoa ripoti leo na kuisoma kwa vizuri kabisa na maneno mengi na kutufungua macho.

Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa jimbo la Tunguu kutoka Shehia zangu zote 13 kutoka Uzi, Ng'ambwa, Kae Pwani, Tindini, Kae Bona, Kikungwi, Bungi, Jumbi, Dunga Kiembeni, Dunga Bweni pamoja na Ubago.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kwenye ripoti hii nilipokuwa naiangalia nikakuta hadidu rejea ambazo kamati imezipitia, lakini ningefurahi kuona kwamba katika moja ambayo wangeitumia ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu kuna maeneo mengi ambayo ni ya Muungano yamo ndani ya hizi taasisi ambazo zimo na kwa njia moja au nyengine tungependa kuyaona ambayo yangeweza kuzungumziwa zaidi ndani ya ripoti. Naamini zingeweza kutusaidia ikiwa ni ripoti yetu ya mwanzo labda kushauri kwa miaka ya mbele *Inshaallah*

tutapata kuona zaidi na mengi ya undani. Lakini kwa kweli hii ripoti ni nzuri kabisa.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nataka nichape siasa kidogo leo. Kumekuwa kuna maneno mengi yanazungumzwa huko mitaani juu ya utawala wa nchi hii na watu wengi wanazungumza. Mimi ndani ya Baraza lako hili natambulikana kama ni *Chairman of the Commonwealth Parliamentary Association*, maana yake mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Tawi la *Branch* ya Zanzibar juu ya Jumuiya ya Madola kwenye Mabunge yetu, ambapo pia nimekwenda mpaka Mauritius kwenye mkutano. Nilipokwenda kule salamu nilizopewa zote kuhusu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni Dkt. Ali Mohammed Shein. Sasa mimi huwa nashangaa sana watu wanavyozungumza huko nje, sisi tumejipanga kwa ajili ya wananchi na ukiulizwa Spika ni nani, Spika wetu tunamjua kipenzi chetu ni wewe hapo, tukiulizwa Jaji wetu Mkuu tunamfahamu ni nani. (*Makofi*).

Kwa hivyo, nchi hii kuna msemo ambao ulitumika zamani hasa kwa Waziri Mkuu wa Uingereza Tonny Blair. Baada ya kukaa miaka kumi alifikiria angeweza kuwa yeye pia Rais wa *European Union*, lakini kwa bahati mbaya hakuweza kutizama wapi alikotoka na hili kwa Kizungu ni neno wanatumia linaitwa *"the some sort of syndrome"* ni eneo ambalo mtu anakuwa anaamini yeye maisha yupo hapa duniani kaja ku-*save* dunia. Katika hili pengine kuna watu wana matatizo ambayo haya yanaitwa "*him hire syndrome"***,** mtu anahisi yeye ndio kaja ku-*save* dunia.

Kwa hiyo, watu watambue tu kwamba sisi Rais wetu ni Dkt. Ali Mohammed Shein na ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na hapa mtu yeyote kama anataka kitu ni mwaka 2020. Mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu na sitoki hapa tutabanana hapa hapa mpaka mwaka 2020 na tupo kwa ajili ya kuwaletea wananchi wetu maendeleo. Kwa hiyo, mimi ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka jimbo la Tunguu na Rais wangu ni mmoja Dkt. Ali Mohammed Shein na yeye ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mapiduzi. Sasa wacha nipige kazi ambayo inanihitajia mbele yangu juu ya ripoti. *(Makofi).*

Mhe. Spika, naanza na Shirika la Nyumba, nilitoa mawazo yangu wakati wa Mkutano wa Bajeti na ripoti hii kwa kweli imetueleza kuhusu changamoto, lakini nataka nitoe mawazo lakini mawazo unapoyatoa sijui kama serikali wanakuwa wanayafanyia kazi, wanasema tu tumeyapokea na lugha yao ni kwamba ushauri tumeuchukua tutaufanyia kazi. Sasa sijui wanakuwa wanakwenda mbele kiasi gani.

Nilitoa mfano katika maeneo ya Kiinua Miguu au pale Chuo cha Mafunzo. Ukiangalia Chuo cha Mafunzo kwa kweli hali ilivyo sasa hivi ni *potential land, prime location* kwa biashara pia kwa wawekezaji wa aina tofauti. Kama inawezekana kile chuo kipo ndani ya himaya na mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tuangalie uwezekano wa kukihamisha ili tutumie maeneo hayo, lakini hukuti mtu anazungumza utasikia ushauri tumeupokea.

Mhe. Spika, pia Nyumba za Kilimani na Nyumba za Mjerumani na humu zimetajwa kwa hali yake pamoja na Pemba. Kwa hivyo, shirika hili tunapoliangalia sisi tuangalie tunakokwenda huko pamoja na ukiangalia ndani kwenye ripoti, naomba niangalie hapa kwenye ukurasa wa 5 Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Hapa wamezungumza jinsi ya idara inakusudia kupanga miji midogo 14 Unguja na Pemba pamoja na kupanga maeneo ya wazi zaidi ya 15. Lakini kwa bahati mbaya au nzuri hapa hayakutajwa lakini naamini katika *hansard* mengine tutayakuta kwa sababu hii ilikuwa ni *summary*. Lakini haya ndiko tunakoelekea na kwa uhamiaji wa watu na jinsi watu wanavyozaliana tutahitaji maeneo mengi na huko tunakokwenda suala la maji, mchanga, mawe, yote tuweze kujipanga kwa haya, lakini nahisi nitagusia kwa hapo tu kidogo na mengine tutakutana kwenye bajeti.

Suala jengine ninalotaka nizungumze masuala ya barabara. Nitoe tahadhari na nilizunguma katika kipindi cha nyuma barabara inapotoka kutoka Fuoni kuelekea sasa kwenda zake Tunguu, najua serikali inapata mchakato kukamilisha pamoja na barabara ya kutoka Mwera-Pongwe kuja zake mpaka Jumbi. Hipa mvua zinakuja, kwa hiyo ningeomba sana serikali na Mhe. Naibu Waziri ndugu yangu hapa Mhe. Mohammed Ahmada wale watu kule wanapata tabu sana wana mazao yao, tope zinakuwa nyingi mvua zikija wanakwama njiani. Kwa hivyo, kidogo angalau irekebishwe barabara ili angalau wale wananchi wapate afueni wakati serikali ipo katika harakati za kukamilisha.

Pia nilizungumza suala la matendo yaliyowatokezea wananchi wa Mkoa wa Kusini wakati wa ujenzi wa barabara kutoka Mwanakwerekwe kuja Fuoni. Naomba sana ujenzi wa barabara utapoanza kutoka Fuoni kuelekea mpaka Tunguu mambo yafanywe kwa mpango na wananchi wapate kujuilishwa, tuna Vyuo Vikuu vingi kule wananchi wanakwenda na kurudi. Kwa hivyo, mipango yote iwekwe rasmi katika *TOR* na katika hayo masuala ya *letter of special interest* kwa hao wanaotaka kuja kutengeneza barabara juu ya masharti hayo yaelezwe kabisa, ili angalau wanapofanya jambo lolote iwe athari iweze kuwa *minimum* kwa wananchi kuendelea na maisha yao vizuri na waendelee kuipenda serikali yao kwa ajili ya mambo mazuri kama haya kuwajengea miundombinu hasa katika barabara hiyo.(*Makofi*).

Lakini leo nataka nizungumze kuhusu masuala ya bandari. Kwa kasi wakati miji inapokua hakuna kitu ambacho tunakuwa tunafeli wakati mwengine kama mipango, ukijiuliza kwa upande wa Kaskazini utaambiwa Bandari ya Mkokotoni ni bandari tu ya kawaida. Lakini ukiangalia Mkokotoni bandari ile katika miaka ya mbele itakuwa ni muhimu katika ku-*serve* kwa wananchi wa Mkoa wa Kaskazini. Tunajua kuna *project* nyingi kubwa zitakuja kufumka kwa upande ule, lakini ile bandari itakuwa ni muhimu kuwaunganisha watu kutoka Kisiwa cha Pemba, Tanga pamoja na maeneo ya Kaskazini Unguja. Lakini pia kwa upande wa Mkoa wa Kusini pia wananchi kuna safari zitakuja kuanza miaka inayokuja. Kwa hivyo, maeneo haya yaanze kuwa *target* kabisa ili pawe eneo.

Lakini sambamba na haya waanze kupanga wapi *helicopter* zitakuwa zinatua. Mimi mwenyewe nina mpango wa kuwanunulia wananchi wangu *helicopter* miaka ya mbele, naamini nitakaa miaka mingi. Nitapenda wananchi wangu baadae wanapanda *helicopter* Mwenyezi Mungu akinijaalia kama nitapiga vipindi vitatu au vinne wawe wanasafiri kwenda Dar es Salaam, wanaingia katika *helicopter* yao, wanapanda ndege ndogo za kutua baharini. Kwa hivyo, mipango hii inabidi serikali, mipango hii nikianza kuipanga serikali ndio watakaokuwa wananikwamisha wao kwa sababu watakuwa hawajajipanga. Mimi nitatafuta fedha nitaweza kupata *helicopter* lakini wapi pa kutua watanambia hakuna eneo. Sasa hii ndio mipango tunakuwa tunafeli. Kwa hivyo, mimi naiomba sana serikali inieleze nataka kujua kwenye Kisiwa cha Uzi, wapi patakuwa pana *helipad* mipango ijulikane na mapema sio tunakaa tunachelewa mpaka mtu anakuja hapa mwekezaji anasema haya tafuteni eneo, katafute eneo, sisi ndio tunamwambia mtu wapi aende akafanye. *(Makofi)*

Kwenye suala la umeme. Umeme mimi nataka nilipongeze sana Shirika la Umeme wanafanya kazi vizuri, waziri pokea pongezi zangu pamoja na Katibu Mkuu, naomba sana suala hili la *infrastructure tax* ambayo imepangiwa haya kupeleka masuala ya umeme miradi vijijini na wamepanga mara hii kupeleka umeme kwenye Kisiwa cha Fundo waendelee na bidii hiyo hiyo Mwenyezi Mungu awasaidie sana awape ngufu, najua wameweka bajeti zaidi ya shilingi bilioni moja wapige kazi na maeneo mengine katika Mkoa wa Kusini hasa jimboni kwangu wayaone. Hapa nataka ninukuu kwenye ukurasa wa tisa (9) kifungu cha 2 kinasema kwamba:

"Shirika linaendelea kutumia mfuko wake kwa kazi za kusambaza umeme vijijini, kazi ambayo kikawaida ilitakiwa kufanywa na Serikali Kuu au mfuko maalum kwa ajili ya kazi hiyo".

Kwa hivyo, shirika bado linaendelea kutumia fedha zake kupeleka umeme vijijini, hivyo wazidi kukazana.

Suala la ardhi kwa upande wa Tunguu. Maeneo mengi yamekuwa yanasimamiwa kutaka kukatwa viwanja, naomba sana Mhe. Waziri tufanye ziara moja tukaangalie hasa kwenye upande wa Tunguu wa ndani kuna uvamizi.

Upande mwengine kwenye suala la maji kwa maeneo ya Michamvi, nilisikia hapa mawazo yakitembea. Nashauri waangalie uwezekano wa kuchukua maji kutoka Chwaka, mpige *water pipes* za chini kwa chini mpaka Michamvi inawezekana. Najua Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kafanya kwenye kisiwa chake cha Tumbatu.

**Mhe. Spika:** Muda Mheshimiwa.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Suala jengine ni masuala ya magari mengi yanayokuja mjini. Upande mmoja wahamasishe kwa upande wa ukataji wa tiketi katika Shirika la Meli pamoja na Kampuni za Bakhresa, wauze huduma za kupata tiketi ziendelee kupatikana katika maeneo tofauti na huku upande mwengine.

Mhe. Spika, namalizia. Chengine naomba sana *public toilet* matatizo watu wanajisaidia kila pahala, ipangwe sheria muhimu kwa mambo haya.

Jengine masuala ya bodaboda. Mhe. Spika, dakika mbili namalizia nakuomba.

**Mhe. Spika:** Muda Mheshimiwa kuna *list* kubwa sana.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** *Two minutes I promise,* nakuomba namalizia na *summarize*.

**Mhe. Spika:** Hapana Mheshimiwa.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Dakika moja ni-*wind-up*.

**Mhe. Spika:** Hapana. Waheshimiwa wanaotakiwa kuchangia ni wengi na sio wote ambao watapata, *actually* nataka kuwashauri wale ambao wameomba mwisho mwisho basi bora waanze kupeleka mchango wao kwa maandishi.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Mheshimiwa kwa kumalizia mifuko ya *plastic* kazi nzuri imefanyika.

**Mhe. Spika:** Usiendelee Mheshimiwa tafadhali naomba ukae.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante. Namwita sasa Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis atafutiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Saada Ramadhan Mwenda ajiandae.

**Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis:** Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kusimama hapa kwa wakati huu na mimi nikaweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Spika, nianze kuchangia ripoti hii katika Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira na Idara ya Mazingira. Miongoni mwa changamoto zilizoelezwa katika ukurasa wa 13 kuna changamoto ya uhaba wa jengo ambapo hupelekea mpaka wafanyakazi kukosa hata pa kukaa wakati wakiwepo kazini. Hii ni changamoto kubwa kwa sababu changamoto hii inawapelekea wale wafanyakazi kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo na hivyo ufanisi wa kazi kutokana na mazingira kama haya unakuwa haupo. Kwa hiyo, niiombe wizara ifanye jitihada za makusudi kuhakikisha kila mfanyakazi anawekwa sehemu yake ya kazi na aweze kutekeleza majukumu yake vizuri ya kuwasaidia wananchi kuwapa huduma zinazostahiki.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije ukurasa wa 17 Idara ya Usafiri na Leseni. Imeelezwa katika ripoti hii kwamba Idara ya Usafiri na Leseni ina jukumu la kusimamia usalama kwa watumiaji wa barabara. Lakini Mhe. Spika, naamini sote tunatambua kwamba haki ya kutumia vyombo vya usafiri na kutumia barabara ni haki ya watu wote, lakini kwa hivi sasa serikali imejitahidi kujenga mabarabara mengi lazima tuipongeze, kwanza naipongeza kwa hilo. Lakini katika kujenga barabara zake haikuzingatia kama kuna watu wote ambao wataweza kutumia barabara ile, mazingira ya barabara zetu hayako rafiki kwa kutumia watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, cha kusikitisha barabara hizi nyengine zimejengwa zamani lakini nyingi zimejengwa hivi karibuni, na tukinukuu Kifungu cha Sheria, Sheria Nam. 9 ya mwaka 2006.

Kifungu cha 12(1) kinasema kwamba:

"Watu wenye ulemavu watakuwa na haki ya kutopata kizuizi kuwa na mazingira rafiki yatakayowezesha kuwa na fursa ya kufikia katika nyumba za umma na vifaa kwa ajili ya matumizi ya umma, barabara na mambo mengine ya burudani".

Kifungu cha 12(2) kinasema kwamba:

"Masharti ya kifungu cha kwanza cha kifungu hiki yatatumika na kuwabana wamiliki wa majengo ya umma yaliyopo na huduma kwa matumizi ya umma barabara na mambo mengine".

Mhe. Spika, tumeshuhudia watu wenye ulemavu wakinyanyaswa sana na madereva na makonda wa magari na sheria hii ipo toka mwaka 2006, hadi hivi sasa hatujasikia kama kuna dereva au makondakta wa daladala waliopewa adhabu kwa kitendo cha kuwanyanyasa watu wenye ulemavu. Ni kweli jambo hili la kusikitisha. Watu wenye ulemavu hawachukuliwi hasa wenye ulemavu wa viungo, wakikutikana na *wheel chair* hapakiwi kwa sababu atakuwa ni mzigo atamchelewesha dereva safari yake. Lakini vile vile kondakta anaona ni kazi kukibeba kile kigari akakipachika juu ya gari yake. Kwa kweli haya ni manyanyaso na huu ni uonevu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, lakini isitoshe, barabara zetu hakuna hata alama moja inayoonesha kwamba watu wenye ulemavu wanatakiwa wapite hapa. Kama tunavyojua watu wenye ulemavu tupo wa aina tofauti. Kuna wenzetu wengine hawaoni lakini wenyewe wamewezeshwa na wanaweza kutembea bila ya kutegemea mtu mwengine, tukitegemea kwamba mazingira yatakuwa rafiki mwenyewe ataweza kufika kila pahala ambapo anahitaji kwenda. Lakini kutokana na hili wanashindwa mtu mwenye ulemavu wa uoni anaweza akakaa muda wa saa nzima hajakata barabara, kwa sababu hawezi kumwita mtu njoo unisaidie. Kwa hivyo, mpaka asikie kishindo ndio ajue hapa mtu anapita, sasa hili ni tatizo naomba serikali ilione.

Vile vile mazingira ya barabara hayamruhusu mtu mwenye ulemavu ambaye anatumia baiskeli ya maringi matatu au *wheel chair* akaweza kutumia, inabidi atumie barabara ile ile ambayo wanatumia watu wote. Changamoto

iliyokuwepo Mhe. Spika, watu hawa huwa mara nyingi wanapata ajali kwa kugongwa na magari na tumeshuhudia wengine wakifa kabisa, anagongwa na kigari chake anafariki na ubaya zaidi akigongwa yeye hagongwi peke yake anagongwa na msaidizi wake ambaye anamsukuma. Kwa hiyo, hii ni hatari na naiomba wizara izingatie sana suala hili inapojenga barabara au inapojenga majengo ya umma izingatie mahitaji ya watu wenye ulemavu, kwa sababu wanapata shida sana kutoka na mazingira mbali mbali.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nije katika changamoto nyengine. Changamoto nyengine iliyopo katika suala la mawasiliano. Hivi sasa hivi Mhe. Spika, kuna vuguvugu ambapo mitandao yetu tunayotumia watu wanaitumia vibaya na inapelekea sasa hivi baada ya kurahisisha zile huduma za mtu kutuma wa *Tigo pesa* au *Ezy- Pesa* tunaogopa, kwa sababu tunatapeliwa sana, wengine wanasema wengine hawasemi. Lakini cha kustajabisha Mhe. Spika, ukishatapeliwa ukenda kule katika ile kampuni ambayo unahisi simu hii ni mfano ya ya Kampuni ya *Tigo* au *Zantel* wanakujibu kwao wao hawana uwezo wa kumpata huyo mtu. Hili Mhe. Spika, ni tatizo na watu wengi hivi sasa hivi tumekuwa tunakaa kwa hofu ukipigiwa simu na mtu unaiogopa. Kwa hivyo hili ni tatizo kubwa.(*Makofi*).

Mimi ningeomba kwa vile haya Makampuni tumeyasajili sisi hapa kwa hiyo, tuyafanyie utafiti makampuni yaliokithiri katika vitendo hivi tuyafungie kwa sababu hawawezi kutoa huduma kwa watu. Haiwezekani kampuni anaimiliki mtu kapata tatizo anakwenda hawezi kupata msaada kwake. Kwa hivyo, hizi kampuni sisi zitakuwa hazitufai na Mhe. Spika, hizi kampuni walisajili *line* ya kila mtu inawezekanaje mtu katapeliwa pesa zaidi ya milioni moja, milioni mbili anakwenda kwenye kampuni wanasema wao hawana uwezo wa kumsaidia.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, mimi kwa mawazo yangu nahisi naiomba wizara ichukue hatua za kutosha iangalie ni kampuni gani iliokithiri na vitendo hivi ifungwe isiweze kutoa huduma kwa sababu haiwezi kuhudimia wananchi wake.

Mhe. Spika, naomba niunge mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*).

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis. Sasa ninamwita Mhe. Rashid Makame Shamsi atafutiwa na Mhe. Saada Ramadhan Mwenda na Mhe. Suleiman Makame Ali ajiandae.

**Mhe. Rashid Makame Shamsi:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuichangia ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Nianze kutoa shukurani sana kwa Mwenyekiti wa Kamati na kamati yake kwa ujumla kwa uwasilishaji mzuri wa ripoti hii ambayo imesheheni mambo mengi sana. Tuipongeze sana kamati hii kutokana na kazi yake nzuri.

Mhe. Spika, nije katika ripoti yenyewe kwenye ukurasa wa 11 nimuombe Mwenyekiti kidogo katika ukurasa huo kwenye kifungu kama sikosei cha 6 kilikuwa kinazungumzia juu ya Tozo ya Ada ya Bandari, kama nimekosea lakini kubwa zaidi ni Tozo ya Ada ya Bandari kuhusu mafuta. Nafikiri hizo takwimu zina matatizo kidogo kwa sababu zinaonesha kwamba tozo ni kubwa kuliko bei ya mafuta yenyewe. Kwa hivyo, naomba sana waiweke sawa ili na *hansard* iwe vizuri.

Vile vile Mhe. Sika, nije katika suala la Idara ya Mipango Miji ambalo limezungumziwa katika ukurasa wa 6 na wa 7. Mhe. Spika, wenzetu katika maoni na maagizo kifungu cha 6, Kamati inaitaka wizara impatie eneo jengine mmiliki wa *FK Enterprise Company* ili kupitisha mradi mkubwa wa uwezeshaji ambao tayari kuanza katika eneo la uwekezaji sehemu ya Nungwi.

Mhe. Spika, hapa nina wasi wasi kidogo kwa sababu maoni haya au maagizo ambayo wenzetu wameyatoa hayakujitokeza katika changamoto. Sasa sijui kuna vigezo gani vya kuweza wenzetu kui-*convince* wizara impatie eneo jengine huyu mmiliki. Mimi nafikiri kwanza tungeweza kumjua huyu mmiliki ni nani ni mwekezaji wa ndani, mwekezaji kutoka nje, na halafu aoneshe uwezo wake amepewa maeneo mangapi ili tuweze kujiridhisha kwa sababu hatuwezi kumuongeza eneo tu pengine huku kuna maeneo mawili matatu wakati hajayaendeleza. Kwa hivyo, tungependa tupate kuona uwezo wake halafu serikali iwe-*convinced* kuweza kumuongeza eneo na awe tayari kweli kuwekeza au huyo kishaekeza tuweze kuona kwamba anastahiki kuweza kupewa eneo jengine.

Mhe. Spika, nikiacha eneo hilo nije kwenye Sekta ya Mazingira. Kwanza niwapongeze sana watu wa mazingira kwa juhudi kubwa sana wanaoichukua kuweza kuhakikisha mazingira yetu ya visiwa hivi yanakuwa salama na hususan kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika suala la kutokomeza mifuko ya plastiki niwapongeze sana. Mhe. Spika, pamoja na pongezi hiyo bado kuna kazi kubwa kidogo ya kuweza kulizungumza suala hili la mazingira.

Nije hapo hapo kwa upande wa plastiki hivi sasa wenzetu wa Tanzania Bara au Muungano wametuiga na hivi sasa wanapiga vita mifuko ya plastiki. Lakini juzi nimemsikia Mhe. Waziri Anayeshughulikia Mazingira Mhe. Januari Makamba akizungumzia suala la plastiki za viroba au pombe za viroba,

kwamba hili linachafua sana katika miji yao na wenzetu tayari wameshapiga marufuku pombe hii ya viroba na wafanyabiashara wa pombe hii kwa sababu wamefungiwa na wana *stocking* kubwa sana, nina hofu sana viroba vingi vitakuja Zanzibar. Kwa hivyo, kutakuwa na mambo mawili, kutakuwa na uchafuzi wa mazingira kwa viroba vya pombe hivi, lakini vile vile vitaweza kuathiri mienendo ya vijana wetu. Niombe sana serikali kuanzia hivi sasa hatujachelewa na sisi tupige vita suala la pombe za viroba kuingia katika nchi yetu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nielekee sasa katika suala la uchimbaji ovyo wa mchanga. Suala hili la uchimbaji mchanga. Kwa kweli nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa kuweza kupiga vita magari ya ng'ombe. Hali ile imepelekea mazingira yetu kidogo kupumua. Lakini kutokana na wakati huu wa serikali kutoa tamko juu ya uchimbaji wa mchanga hususan katika Mkoa wa Kaskazini, mchanga ambao ni wa biashara naitahadharisha sana serikali yetu kwamba kuna uwezekano sasa na inawezekana ishaanza, kwa sababu hivi sasa bei ya mchanga imepanda na bei ya tofali imepanda. Kwa sababu wajengaji wengi ni wanyonge itaonekana kwamba hivi sasa kuna uchimbaji wa mchanga unatokea katika maeneo ya maakazi ya watu na hususan kwa kutumia vigari vya *carry* kwa sababu magari ya ng'ombe hayapo.

Leo kwenye mawio nimesikia katika eneo la Bungi kwenye minara yetu kuna uchimbaji ya mchanga ambao unaendelea na hiyo ni hatari kwa minara yetu lakini kwa mazingira yetu. Kwanza nimuombe Mhe. Waziri wa Habari kuweza kulifuatilia suala hili la uchimbaji wa mchanga katika minara hiyo, lakini vile vile kwa Wizara inayohusika tuweze hivi sasa kuwa doria, kwa sababu huku tunadhibiti lakini kuna wengine wajanja wanaanza kuchimba katika maeneo kwa kutumia gari ndogo za *carry*. Kwa hivyo, tutaona huku tumezuia lakini kwa upande mwengine huku kunafunguka.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nije sasa au nimalizie katika suala zima la Sekta ya Maji. Niipongeze sana Wizara niipongeze sana vile vile Mamlaka ya Maji (*ZAWA),* kwa juhudi wanazochukua katika kuona kwamba wananchi wake wanapata maji bila tatizo. Na niipongeze serikali chini ya uongozi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kutokana na mipango mizuri ambayo ametueleza juu ya suala la utatuzi wa tatizo la maji ambayo serikali imejipanga. Nina imani kwamba baada ya muda si mrefu basi kuna uwezekano wa kupata maji ya kutosheleza.

Lakini nije katika suala hili la uvamizi wa vianzio vya maji. Ukweli lazima tujiulize kwa nini tatizo hili lilitokea. Vianzio vya maji vyengine vipo tokea

Ukoloni lakini leo tunajiuliza kwamba vyanzo hivi vimevamiwa, kwa kweli lazima tujiulize watendaji wa Shirika, watendaji wa Taasisi inayohusika. Mimi nafikiri bado kuna haja ya uwajibikaji, tatizo limetokea lakini kwa upande mmoja lazima serikali tujilaumu kwamba tulikuwa wapi. Kwa hivyo, nisihi sana taasisi inayohusika hayo maeneo ambayo bado yamebakia basi tuyadhibiti kwa kuyajengea senyenge ili kuweza kuona kwamba tunaendelea kuitunza raslimali hii. Lakini ikiwa tunaimba tu juhudi hazipo, mimi nafikiria itafika wakati sasa vyanzo hivi vikakauka kabisa. Kwa hivyo, niiombe sana taasisi inayohusika kuweza kuweka ulinzi na kuweka *becon* na senyenge ili kuona kwamba maeneo yetu haya tunayadhibiti.(*Makofi*).

Baada ya kusema haya Mhe. Spika, nishukuru kwa nafasi uliyonipa lakini na mimi niungane na wenzangu katika kui-*support* ripoti hii asilimia mia kwa mia.

Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa mchango wako.Waheshimiwa Wajumbe wachangiaji bado wengi na sikusudii kuwamaliza wote. Kwa hivyo, wengine na hasa mlioleta mwisho waanze kuchangia kwa maandishi kwa sababu baada ya hapo nitawaita Waheshimiwa Mawaziri ambao wameomba.

Baada ya hapo sasa naomba nimwite Mhe. Saada Ramadhani Mwendwa atafuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali an Mhe. Viwe Khamis Abdalla ajiandae.

**Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Lakini pia nikushukuru na wewe kwa kuweza kunipa nafasi hii nikazungumza machache niliyokuwa nayo ndani ya moyo wangu. Mhe. Spika, mimi niko ukurasa wa 12 kwenye mazingira. Kwanza nawapongeza Kamati ya Mazingira kwa kazi kubwa wanaofanya kwa muda huu kufika kuwa mji wetu unaonekana kuwa ni mzuri tunawashukuru sana na waendelee wasichoke.

Lakini kubwa hasa niliotaka kuzungumza Mhe. Spika, watu wa Mazingira nilikuwa nawaomba sisi watu wa mitaa ya Chumbuni, Shaurimoyo, Mto pepo, tuna mitaro ya michirizi ile ya maji ambayo kuwa inatoka juu kulekea baharini Maruhubi. Mhe. Spika, mitaa ile watu wengi sana wamejenga nyumba lakini tatizo la wananchi wetu mitaro yao ya maji machafu lakini na mpaka maji ya kukoshea vyombo na kufulia wanaelekeza kwenye mto ule. Linapotokea tatizo

la kipindupindu kinakuwa kikubwa eneo letu sisi, ndio maana mnasikia sana kipindupindu kinatokea kule kutokana na maji machafu wanayomwaga kule ndani ya mto. Kwa hiyo, nilikuwa nawaomba mazingira kama walivyoweza mifuko na nawaomba wajitahidi wao wakishirikiana na Halmashauri au Manispaa zao ili waliondoe hili tatizo wahakikishe wale wananchi waliopeleka michirizi yao kwenye mto wa maji machafu waweze kuiondoa, ili tupate usalama yanapokuja maradhi basi tuweze kuepuka nayo. .(*Makofi*).

Mhe. Spika, nina suala jengine nilitaka kuomba liko kwenye Mawasiliano. Mawasiliano Mhe. Spika, sisi Mwenyezi Mungu ametualia wananchi wa Mtoni-Amani tumepata barabara nzuri mbili zote kwa pamoja zimeungana. Kwa hivyo, tunaishukuru sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kutufanyia barabara nzuri kama hii. Lakini kubwa tu nilitaka kumuomba Mhe. Waziri atuangalie kwa jicho la huruma wananchi wa Mto pepo na Chumbuni Mwenyezi Mungu ametujaalia uwezo vile vile serikali imetupa skuli mbili tunayo ya Mtopepo na ya Chumbuni. Kwa hivyo, watoto wa Mtopepo wanavuka barabara wanaenda Chumbuni na wa Chumbuni wanavuka wanakuja Mtopepo.

Lakini tatizo kubwa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, sisi pale barabara ile ni nzuri lakini magari mengi yanayopita ya mchanga yanapita njia ile, lakini hakuna chochote kidhibiti cha wale watoto pale kila siku haimalizi wiki watoto wamepata ajali. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kama kuna uwezekano basi na sisi atupatie japo askari akae pale watoto wakipita kwenda skuli basi ili usalama upatikane wa watoto na wazee watu wazima wanaoweza kupita njia ile namuomba sana Mhe. Waziri.(*Makofi*).

Mhe. Spika, jengine hili ni lalamiko nadhani kwa wanawake wote walioko mitaani wanatusikiliza suala la maji. Mhe. Spika, suala la maji Mkoa wa Mjini/Magharibi bado lipo wizara inajitahidi sana Mheshimiwa toka aje anajitahidi sana tushukuru Mhe. Rais kutuwekea mwanamke Waziri kwa sababu anaijua ile shida ya maji na anajitahidi, lakini bado namuomba Wizara yake iendelee wanawake wa Chumbuni bado tunanyonyoka nywele maji hatuna.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja ripoti ya Mwenyekiti, lakini nampongeza sana Mwenyekiti na Kamati yake kwa masuala makubwa hayo baada ya kuyaibua na kuyaleta kwenye meza ili tuyachangie na kuweza kuyafanyia kazi.

Mhe. Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa kwa mchango wako na kwa kuokoa muda pia. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali atafuatiwa na Mhe. Viwe Khamis Abdalla na Mhe. Nassor Salim Ali ajiandae.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati iliyowasilishwa mbele yetu.

Mhe. Spika, pia niwapongeze Wajumbe wa Kamati hii pamoja na Mwenyekiti wao mashuhuri Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kutuwasilishia ripoti hii nzuri iliyojaa kila kitu ndani yake.

Mhe. Spika, mimi niende katika Shirika la Bandari. Kwanza nilipongeze Shirika la Bandari kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha kwamba mizigo ya wananchi pamoja na wao wanafika salama katika bandari zile. Mhe. Spika, Zanzibar tuna Bandari Kuu tano ikiwemo Malindi, Mkokotoni, Wesha, Mkoani na Wete.

Mhe. Spika, niombe tena Shirika la Bandari hapo hapo kuhakikisha Bandari ya Wesha ili kuondoa msongamano wa mizigo inayokwenda kwenye Bandari ya Mkoani kwa wale ambao kwamba iko Pemba, basi Bandari ya Wesha wengeifanyia matengenezo ya kupatikana kina kikuwa cha maji ili zile meli za mizigo zikaweza kufika pale na wafanyabiashara wengi wao wanatoka Chake Chake ili wakapata kushusha mizigo yao kwa usalama.

Mhe. Spika, niende kwenye Sekta ya Nishati (*ZECO)*. Mhe. Spika, sekta ya Nishati hususan umeme ni nyenzo muhimu katika kukuza uchumi wa maendeleo ya jamii. Pia nilipongeze Shirika la Umeme kwa kuhakikisha kwamba wanaitekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kupeleka umeme katika visiwa vidogo vidogo kama vile Tumbatu, Shamiani Muwambe, Kojani, Kisiwa Panza na Makoongwe.

Lakini pia vile vile niwaombe watu wa Shirika la Umeme kwa sababu kuna tatizo kubwa sana ambalo kwamba linajitokeza wakati wananchi wetu wanapokwenda kuomba kuunga umeme hutoa chochote baadhi ya *time* nyengine ndio wakaweza kuingiwa. Lakini ukiangalia saa nyengine saa vile vifaa vipo kila kitu kipo, sasa mimi sijui ni kitu gani kinachofanya kwamba mpaka *time* nyengine yule mwananchi anayetaka umeme ateseke mpaka ikibidi *time* nyengine kutoa chochote. Kwa hivyo, niliombe Shirika la Umeme

kuhakikkisha kwamba wafanyakazi hawa baadhi yao wanawachukulia hatua ili kuhakikisha kwamba kitendo hichi wanakikomesha.

Mhe. Spika, niende kwenye Shirika la Nyumba. Mhe. Spika, kupitia Shirika la Nyumba pale Chake Chake maeneo ya Miembeni kuna majumba mengi pale ambayo kwamba ni mabovu na mengine yameshaanza kuanguka lakini bado watu wanaendelea kukaa na shirika lipo sijui hatua gani wanazichukua, ili labda kuhakikisha kwamba mpaka litokee tatizo kwamba nyumba zile zinaangukia watu ndio yatari waanze kuchukua hatua. Kwa hivyo, niombe Shirika la Nyumba kwamba zile nyumba ambazo kwamba zote ni mbovu hazistahiki kukaa wananchi basi wahakikishe kwamba nyumba zile hazikaliwi.

Mhe. Spika, niende kwenye Mamlaka ya Maji. Mhe. Spika, maji kama tunavyojua ni muhimu katika maisha ya binadamu. Lakini na wao niwapongeze Mamlaka ya Maji (*ZAWA)* kwa kutupatia maji katika miji na vijiji. Lakini Mhe. Spika, katika jimbo langu la Ziwani kuna kijiji cha Kichanjaani Kilimani, Kichanjaani Depu na Mkumbuu hadi Ngagu, wananchi wa kule Mhe. Spika, hawapi maji na mradi wa maji uko umetoka ufadhili kutoka China wanatumia tangi liliopo Gombani wananchi wa Ndagoni kutumia maji yale. Lakini inasikitisha kwamba mpaka usiku wanakesha akina mama wale hawapati maji wanasumbuka.

Pia niwaombe watu wa Mamlaka ya Maji wajitahidi katika suala hili la maji kuhakikisha kwamba wananchi wale wawatizamie tatizo lile ni nini zaidi, kwa sababu naona hakuna kinachokwamisha kwamba bomba zipo za kutosha, tangi lipo lile kubwa na linahifadhi maji si chini la laki tatu naa. Sasa sijui kilichosababisha kwamba wananchi wangu wa kule maeneo ya Kichanjaani Depu na Kichanjaani Kilimani hadi Ngagu Mkumbuu ikawa wanakosa maji kila siku.

Mhe. Spika, niende kwenye Sekta ya Barabara. Sekta ya barabara nayo ni muhimu lakini vile vile Ndagoni kuna changamoto, kama ukitizama Ndagoni kwenye nishati ya umeme, umeme umetoka Tanga lakini mpaka hadi leo Mhe. Spika, nathubutu kusema kwamba tangu dunia kuumbwa Ndagoni barabara hakuna. Kwa hivyo, niiombe wizara husika ambayo inashughulikia masuala ya nishati kule ndiko kwenye umeme.

Pia Mhe. Haji Omar Kheir yupo hapa wizara yake kule ndiko kwenye Vikosi wanakolinda ule umeme. Vile vile Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuhakikisha kwamba kule Ndagoni barabara ile inashughulikiwa na inatengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante (*Makofi)*

**Mhe. Spika**: Ahsante sana Mhe. Suleiman Makame Ali, sasa naomba nimwite Mhe. Viwe Khamis Abdalla, atafuatiwa na Mhe. Nassor Salim Ali Aljazira na Mhe. Zulfa Mmaka Omar ajiandae.

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona na ukaweza kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia ripoti ya Kamati ya Mawasiliano.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa hotuba yake nzuri na uwasilishaji wake pamoja na ufuatiliaji wao wa kutosha.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu na Mamlaka ya Maji (*ZAWA)* Pemba. Nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanafikiwa na huduma hii ya maji. Lakini Mhe. Spika, zipo changamoto zilizokuwa bado zinawakwaza wananchi katika huduma hii ya maji. Wakati wa bajeti ya Mhe. Waziri nilichangia kuhusu tatizo la maji ambalo lipo katika kijiji changu cha Kiuyu Minungwini. Mhe. Waziri alinijibu kwamba tatizo hili tayari limeshaondoka. Lakini mara tu baada ya kumaliza bajeti, mimi mwenyewe nilisafiri nilikwenda Pemba na nilikwenda mpaka kwenye Mamlaka ya Maji (*ZAWA)* Machomanne nikafuatilia suala hili, na siku niliyofika pale niliukuta mchikichi ambao kuwa umetolewa kwenye kisima kile kinachohudumia wananchi wa Kiuyu Minungwini mpaka wananchi wa Kiuyu Kigongoni. Lakini tatizo hili Mhe Spika, mpaka leo tatizo hili lipo na bado linawakwaza wananchi.

Mhe. Spika, wanaopata shida ni wanawake na kama tunavyojua wanawake ndio ambao wana huduma zote katika jamii, hasa wanawake wa vijijini ambao wana kazi nyingi. Mwanamke atoke asubuhi aende bondeni, aje ahangaike na huduma hii ya maji. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri suala hili la tatizo la maji ambalo liko katika kijiji kile cha Kiuyu Minungwini, basi nimuombe Mhe. Waziri alifuatilie kwa kina ili tatizo hili liweze kuondoka kwa sababu kisima kipo na hivi karibuni kuna mradi ambao uliweza kuchimba kisima chengine katika maeneo ya hapo hapo kilichopo kisima hiki. Lakini nilipokwenda kule *ZAWA* waliniambia kwamba kisima hiki kilichochimbwa kwa kupitia huu mradi kinahitaji shilingi milioni tano. Kwa hivyo, niiombe serikali wajitahidi, hii shilingi milioni tano basi waweze kuwafikishia ili waweze kutatua changamoto hizi. Pamoja na yote hayo maji hayapatikani, lakini inapofika

mwisho wa mwezi wananchi hawa wanadaiwa pesa za mwisho wa mwezi ili waweze kulipia katika Shirika hili la Maji (*ZAWA).*

Mhe. Spika, nikitoka niende kwenye Shirika la Umeme. Niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwaletea wananchi huduma hii ya umeme mpaka vijijini. Lakini kuna changamoto ambazo zinawapata hawa wananchi ambao wako vijijini, kwa sababu vituo vyote vya umeme viko mijini kwenye Mawilaya, Wilaya ya Wete, Wilaya ya Chake Chake na hapa Unguja kipo mjini Unguja. Lakini Mhe. Spika, wakati mwananchi anapotaka kununua umeme ni lazima apande gari aende akaitafute huduma hii ya umeme. Kwa hivyo, niiombe serikali waweze kuwafikishia wananchi huduma hii ya ununuzi wa umeme vijijini ili kuwarahisishia matumizi haya ya umeme.(*Makofi*).

Mhe. Spika, vile vile niende kwenye Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Niipongeze Wizara hii kwa kujenga barabara nyingi Unguja na Pemba. Pia niwapongeze Wizara hii ya Mawasiliano kutokana na ahadi ambayo aliiweka Mhe. Rais katika Kijiji cha Kiuyu Minungwini kuwa atawafikishia barabara katika kijiji chao hiki, kwa hivyo niwapongeze Wizara hii ya Mawasiliano kwa mara ya kwanza ahadi hii wameanza kuitekeleza, lakini bado kuna changamoto ambayo bado hawajaimalizia. Kwa hivyo, niwaombe wizara wajitahidi barabara hii waimalize ili waweze kuwaondoshea wananchi wakati wa mvua usumbufu, kwa sababu itakapofika wakati wa mvua kama barabara hii bado hawajaimwagia fusi basi wananchi ambao wanaishi katika kijiji kile watashindwa kutoka katika kijiji kile na kwenda katika safari zao za muhimu katika maisha yao ya kila siku.(*Makofi*).

Mhe. Spika, hivi karibuni Mhe. Waziri alitoa tangazo la kuhusu viwanja ambavyo wananchi hawajajenga basi itakapofika muda viwanja hivi watavichukua. Niiombe serikali waangalie kwa makini, kwa sababu wananchi wa Zanzibar wengi ni maskini, mwananchi anahangaika miaka 20 kutafuta kiwanja baada ya kukipata kile kiwanja anahangaika tena kutafuta pesa ya kuweza kujengea kile kiwanja chenyewe. Tukiangalia sasa hivi wanawake na wao pia wamechangamka na wao wanahitaji kumiliki mali. Mhe. Spika, mwanamke anatoka asubuhi anakwenda bandarini anabeba beseni la samaki anauza, mwengine anakaa usiku mzima anakanda unga ili aweze kupata kununua kiwanja na aweze kuishi na watoto wake. Leo hii serikali inatoa amri ya kuwa viwanja itakapofika mwezi wa tatu basi viwanja vile vitarejeshwa kwenye serikalini.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, pia niwapongeze wale Wajumbe wote wa Kamati pamoja na Mwenyekiti wao na Makamo Mwenyekiti.

Naunga mkono ripoti hii ya Kamati kwa asilimia mia. *(Makofi).*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Viwe Khamis Abdalla. Sasa naomba nimwite Mhe. Nassor Salim Ali atafuatiwa na Mhe. Zulfa Mmaka Omar na Mhe. Said Omar Said ajiandae.

**Mhe. Nassor Salim Ali (Al Jazira):** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kamati ambayo kwa kweli iko chini ya Mwenyekiti Jemedari Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Spika, kwa vile mimi ni Mjumbe wa Kamati hii nitakuwa sina mchango mkubwa, lakini nimesema nizungumze mawili au matatu, ili na mimi niweze kupeleka ujumbe wangu kwa kuweza kuongezea nyama ripoti hii.

Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, na zaidi imezidi kujengeka na imani na Rais wetu wakati juzi alipokuja kuzungumza na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili kuwa na imani ya kuondoa tatizo la maji kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nimezungumza hivyo kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi katika Jimbo la Kikwajuni, ambalo liko katika Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini/Magharibi. Lakini baada ya maelezo matamu, maelezo mwanana yenye ukweli na yenye msingi wa kuondoa tatizo la maji katika Mkoa wa Mjini/Magharibi, Mhe. Rais juzi alitufurahisha na kwa kweli tunamuunga mkono kwa juhudi zake katika kuondoa tatizo la maji kwenye Mkoa wa Mjini/Magharibi. Mhe. Spika, juhudi hizi zinaongezwa nguvu na Waziri husika Mhe. Salama Aboud, na mimi nasema kweli wanawake wanaweza, hongera sana Mhe. Waziri. *(Makofi).*

Mhe. Spika, changamoto ya maji katika Mkoa wa Mjini/Magharibi ni kubwa na Zanzibar kwa ujumla, lakini hali halisi ambayo inasababisha tatizo hili la maji, inatokana na upungufu wa vianzio vya maji. Mimi nikiwa shuhuda. Katika Mkoa wa Mjini/Magharibi vianzio vya maji vinatokana na chemchem za Mwanyanya pamoja na Mtopepo. Lakini chemchem hizi zimekuwa na hali mbaya ya utoaji wa maji au vianzio vya maji kupungua katika maeneo haya.

Vile vile hata kwa Pemba Mhe Spika, kuna maeneo ya vianzio vya maji chemchem za maji kama vile Kwapweza, Kiguuni, Bunguni na Gawani. Mhe. Spika, maeneo haya yamekuwa ni mapungufu ya maji katika chemchem hii, lakini yote haya ni kutokana na hali halisi ya tabia nchi. Mimi niiombe serikali kuhakikisha katika maeneo haya ya chemchem yanapandwa miti, yanaongezwa miti na kuondoa na kuwazuwia wananchi kutokujenga nyumba katika maeneo haya.

Mhe. Spika, nije katika sisi Wawakilishi pamoja na Wabunge. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na Wabunge ambao wanachangia katika kupunguza tatizo la maji katika majimbo yetu. Vile vile nitoe ushauri kwa Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwamba tuwe na tabia na ukaribu zaidi na wataalamu wetu wa *ZAWA*, tatizo ni kwamba tunanunua vifaa vya maji bila ya kuwashirikisha wataalamu wetu wa *ZAWA*, ndio inafikia wakati tunanunua vifaa ambavyo havina ubora, baada ya siku mbili tatu mabomba yale yanapasuka. Kwa hivyo, niwaombe, nichukue fursa hii katika mchangio wangu huu kuwaomba Wawakilishi wenzangu na Wabunge wale ambao wanatokana na CCM, kwa sababu Wawakilishi wa CCM tunatekeleza vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi, katika kuleta maendeleo kwenye majimbo yetu. Kwa hivyo, niwaombe sana Wawakilishi wenzangu na Wabunge kununua vifaa kwa kuwashirikisha wataalamu wetu wa *ZAWA*, ili kuondokana na kununua vifaa ambavyo havina ubora.

Vile vile nije katika suala zima la Mamlaka ya Usafiri wa Baharini. Mhe. Spika, suala hili nimesema nilizungumze kidogo kuhusiana na Chuo cha Mabaharia (*DANOS*). Mhe. Spika, chuo hiki kimekua ni mkombozi wa ajira kwa vijana wetu. Nazungumza hivi kwa ushahidi kwa sababu mimi tayari nimeshapeleka vijana takriban wanne na wamepata ajira kwa kupitia kampuni hii. Mhe. Mwenyekiti, alizungumza hapa kwa kuwaomba Wawakilishi kuwapeleka vijana wetu katika chuo hiki. Lakini Mhe. Spika, chuo hiki kina matatizo, kina changamoto. Kwa hivyo, niiombe serikali ili wakae na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuliondoa tatizo ambalo linalokikabili chuo hiki, kwa sababu faida kubwa wanaipata vijana wetu wengi, vijana takriban 1,500 wanapata ajira kwa kupitia chuo hiki, ni Wazanzibari na ni Watanzania. Kwa hivyo, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunakiunga mkono na kuondoa matatizo yale ambayo yanakikabili chuo hiki.

Vile vile Mhe. Spika, nije katika suala zima utunzaji wa barabara (*UUB)*. Mhe. Spika, niipongeze serikali sana. Mimi nimetembea sana Unguja na Pemba nikiambatana na Mwenyekiti wangu Jemedari Mhe. Hamza Hassan Juma. Tumetembea Pemba nzima, barabara zote kubwa na zote za ndani. Kwa kweli

serikali yetu imefanyakazi kubwa ya kujenga barabara, kilichobakia Pemba ni barabara ya Wete hadi Chake Chake, na Ole Kengeja, na barabara hizi zikimalizika basi Pemba itakuwa kama Ulaya. Hili ninalozungumza ni mashahidi sote kwa sababu sote tunakwenda kwenye ziara mbali mbali za Kamati, tunapita kwenye kichochoro hiki na kile.(*Makofi*).

Vile vile Mhe. Spika, mbali na Pemba hata Unguja. Lakini Mhe. Spika, niombe kitu kimoja, barabara yetu tuliyoijenga ya Fuoni, barabara ile ni ya kisasa na ni barabara nzuri. Lakini niiombe serikali kwamba barabara ile tuiweke taa ili mji wetu uzidi kung'ara. Kwa bahati nzuri mambo yanakwenda vizuri kesho kutwa barabara ile inaishia Tunguu na mji wa Tunguu siku hizi unazidi kunawirika, yote ni kazi nzuri anayoifanya Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein, lakini vile vile ni kazi nzuri inayofanywa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, niiombe serikali barabara ile tuitie taa ili mambo mazuri yaweze kunawirika.(*Makofi*).

Mhe. Spika, la mwisho kuhusu Shirika la Nyumba. Shirika hili tumelianzisha kwa nia njema na ni tegemeo kubwa sana katika kuweka mazingira, maisha na makazi bora kwa wananchi wetu, na nina imani kwamba shirika hili litafanyakazi vizuri na kuweza kuondoa matatizo ambayo yanawakabili wananchi wetu. Lakini nyumba za maendeleo ziko katika hali mbaya. Nyumba za Maendeleo za Kengeja, Mkoani, Chake Chake na vile vile za Unguja nyengine. Lakini ile ya Kengeja iko katika hali mbaya, inaweza ikaleta maafa. Kwa hivyo, niiombe serikali kuhakikisha kwamba inachukua juhudi binafsi ili kuhakikisha nyumba ile inafanyiwa ukarabati ili kuondoa kutokutokea maafa.

La mwisho Mhe. Spika, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, lazima tuseme ukweli, Serikali yetu imefanya kazi kubwa na lazima sisi tukiwa *back benchers,* tuwaunge mkono Mawaziri wetu na Serikali yetu kwa jumla, kwa sababu kazi wanayoifanya ni kubwa katika kuleta maendeleo, hususan katika kipindi hiki cha mwaka 2015/2020 na kuendelea. Mikakati mikubwa ambayo wanaifanya serikali yetu, sisi tunaona, tunakwenda huko. Mhe. Spika, ni tofauti na kipindi cha nyuma lakini sasa hivi ni kazi tu tunakwenda, ule msemo unaosema hapa kazi tu kweli unatekelezeka. Kwa kweli ni kwa sababu ya usimamizi mzuri wa Rais wetu. (*Makofi*).

Juzi Mhe. Spika, niwaweke wazi kwa sababu wananchi wamekuwa wakizungumza maneno mengi. Juzi kulizungumzwa sana maneno yamezungumzwa kwenye mitandano, lakini sisi tulikuja tu kumuona Mhe. Rais na tulimuomba sisi ili tuonane na yeye, ili kuondoa matatizo yetu ndani ya majimbo yetu, hakuna jengine ambalo tulizungumza ni matatizo ya ndani ya

majimbo yetu, na ametuhakikishia Mhe. Rais na tuna imani na yeye na tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu Mhe. Rais ampe maisha marefu ili atuletee maendeleo katika kipindi hiki mpaka mwaka 2020, na nina imani mwaka 2020 Chama cha Mapinduzi kitashinda ushindi wa kishindo, kwa sababu ya maendeleo tunayoyafanya.

Hongera sana na ninamshukuru sana Mhe. Waziri, watendaji wako pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji wanafanyakazi nzuri, hongereni sana.

Mhe. Spika, naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia mbili. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Mjumbe, sasa naomba nimwite Mhe. Zulfa Mmaka Omar, atafuatiwa na Mhe. Said Omar Said na Mhe. Mussa Ali Mussa ajiandae.

**Mhe. Zulfa Mmaka Omar:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika ripoti hii.

Mhe. Spika, nianze na Idara ya Usafiri na Leseni. Mhe. Spika, niipongeze Idara ya Usafiri na Leseni hasa Pemba kwa operesheni yao ya kamata-kamata *T-One*, niwaambie kwamba kazi wanayoifanya tunaiona na ni nzuri, kwa sababu sasa hivi tunaona kwamba barabarani ukitembea huko wakati mwengine unakuwa huna amani kwa hawa waendesha *T- One*. Lakini niwapongeze kwa juhudi zao walizochukua za makusudi kuwakamata wale wote wanaovunja amani ya barabara kwa *T-One*, na niwaambie kwamba kazi ile iendelee siku hadi siku. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nikitoka hapo katika Idara ya Usafiri na Leseni. Mhe. Spika, ukifanya jambo zuri unatakiwa usifiwe. Watu hawa wanafanyakazi asubuhi na jioni, wakati mwengine wanakwenda kufanyakazi usiku, lakini sasa wakitoka barabarani kule kufanyakazi na wakifika katika eneo lao la Ofisi kwa kweli ni kilio kidogo.

Mhe. Spika, Idara ya Usafiri na Leseni kwa kweli Ofisi yake kwa upande wa Pemba ni ndogo sana. Katika ofisi ile chumba kimoja wapo watu wa aina tatu ambao wanafanyakazi tofauti. Chumba kimoja hicho hicho utakuta kwamba kuna watu wa *route*, chumba hicho hicho kuna watu wa leseni ya biashara, kwa kweli ni msongamano mkubwa kwa wafanyakazi chumba kimoja, kitu ambacho kinafanya kwamba wanafanyakazi katika mazingira mabaya ya hewa na mambo mengine.

Kwa hivyo, naiomba serikali kwa kupitia Wizara hii, watakapokuja na bajeti yao ya mwaka huu ambao tunakwenda, basi jengo lile waliangalie kwa imani kubwa, kwa sababu wana jengo lao zuri ambalo wamehamishwa na kupelekwa katika jengo ambalo ni dogo. Kwa hivyo, waweke pesa kidogo ili lile jengo ambalo wamelihama litengenezwe ili na wao wajisikie kwamba wanafanyakazi na wanajaliwa katika seriakali hii. Pia niiombe Serikali hii pale pana sehemu ya Karakana tunajua kwamba magari yetu ya Serikali yanatakiwa yatengenezwe katika hizi Karakana zetu. Lakini la kusikitisha Karakana zile hazina vifaa vya kutengeneza magari yetu. Pemba tunaijua hali yake ya kisiasa, unalichukua gari la Serikali unakwenda kulipeleka gereji ya nje, hujui hali yake ni ipi ya kisiasa. Hivi Mheshimiwa mtu yule anaweza kulifanya lolote nani tutamlaumu hatuna. Kwa hivyo naiomba sana sehemu ya Karakana iangaliwe ili iweze kufanyakazi na magari yetu ya Serikali pamoja na watu binafsi yaweze kufikishwa pale na kutengenezwa kwa urahisi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba nije katika Shirika la Bandari. Mimi nataka nigusie gati Mkoani. Katika gati ya Mkoani kuna tatizo moja ambalo linasumbua kidogo, ukitoka katika gati hadi ukifika eneo la kupandia gari ni eneo kubwa sana kwa kutembea kwa miguu, wale wanaotembea na magari basi kadhia ile haiwezi kuwafika, lakini pale unashuka meli umepanda kwenye meli tokea saa mbili, unashuka pale saa nane na nusu ukishuka pale wakati mwengine kuna mvua, unakuta kwamba mwanamke ana watoto, wawili mmoja kabeba wawili kakamata huku kuna mvua kidogo ni hatari. Kwa hivyo naiomba Serikali pale katika gati ya Mkoani kuna ile daraja ambayo wanaitumia watu kwa kupita kwa miguu, ile daraja waiboreshe waitie na mabati kwa juu au hata maturubali ili wakishuka katika meli wasiroe na mvua wala wasipate kupigwa na jua wafike katika gari wakiwa katika hali nzuri.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika Idara ya UUB. Mimi nataka niwapongeze Idara ya UUB tunaona kwamba barabara nyingi sana zilizotengenezwa na UUB zina viwango vya hali ya juu kulikoni barabara nyengine ambazo wanawapa wakandarasi wa nje kutengeneza. Mhe. Spika, tunajua kwamba UUB vifaa vyao ni vibovu na vichakavu, lakini Idara hii inafanyakazi kwa mashine hizo hizo mbovu wakati mwengine wanatumia mikono yao, akili zao zote wanazifikisha pale na pesa ambazo wanaingiziwa katika Mfuko huu ni ndogo, unakuta kwamba wanatengeneza barabara kubwa lakini pesa ni ndogo. Kwa hivyo Idara hii tuipongeze kwa kazi yao wanayoifanya, naamini kwamba nchi yao wanaipenda na Serikali wanaipenda. Kwa hivyo tuwaombe Serikali vile vifaa vya UUB ni vibovu tusitumie pesa hizi kuwapa watu wa nje kututengenezea barabara badala yake pesa ile tununue

vifaa, ili na wao waweze kuzitengeneza barabara hizi kwa pesa za chini lakini zilizokuwa zina kiwango cha juu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika Shirika la Meli. Katika Shirika la Meli mimi nawaomba kwa kweli sasa hivi kuna matatizo ya kuuza tiketi mikononi suala hili linasumbua, kwa sababu unaweza ukenda pale panapouzwa tiketi ukaambiwa hamna, lakini ukienda nje unazikuta kwamba tiketi za matapeli kibao hapa hatujafanikiwa Mheshimiwa. Na tukitizama kama hii meli yetu ya MV Mapinduzi II hawa upande wa pili hawa Mheshimiwa watani wetu meli ile baada ya kuja tu walisema kwamba meli lile ni bovu, lakini ukiangalia sasa hivi hawa upande mwengine hawa wao wanakimbilia mbio kwenda kununua tiketi hizi sisi tulioisifu wakati mwengine tunakosa.(*Makofi*).

Kwanza niwapongeze sasa hivi wanajua kwamba ile meli ni mpya ni nzuri na wao wanapanda humo humo, ila tuombe wananchi wetu ile meli yetu ni nzuri tuendelee kuitunza. Pia meli ile naomba ifanyiwe marekebisho kidogo ya mlango, mlango ni mdogo wakati wa kushuka wakati mwengine watoto wanasumbuka, unakuta wenye nguvu zao vijana shababi wanashuka huku wakijisikia. Lakini sasa Mheshimiwa kuna watoto, kuna wanawake wajawazito wakati wa kushuka wanasumbuka sana, unamkuta mtoto anabanwa hadi roho inakuuma. Kwa hivyo tunaiomba Wizara ile meli waifanyie marekebisho ya mlango. Pia katika meli ile kuna mlango mkubwa ule ambao ukishushwa wanaweza watu kushuka kwa urahisi. Kwa hivyo ifanye jitihada za makusudi kuijengea vizuri mlango meli ile ili watu waweze kushuka kwa urahisi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nikitoka niende katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mhe. Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege tuipongeze pia kwa kukusanya mapato yake vizuri na kuzidi kwa asilimia. Lakini sasa Mhe. Spika, Mamlaka haya ya Viwanja vya Ndege wana changamoto ambazo na wao zinawakabili, pesa zile wanazikusanya kwa wingi lakini pesa zile ambao wanazikusanya asilimia 80% tunakuta kwamba imeingia Serikali kupitia *ZRB.* Mheshimiwa asilimia 80% kwa wao kuitoa ni kubwa. Kwa hivyo watu wale waangaliwe asilimia ile ishushwe angalau ifike 70 au 65 ili asilimia kidogo ibaki pale ili waweze kujiendesha katika mambo yao katika viwanja vile vya ndege ikiwemo masuala ya mishahara na mambo mengine ya umeme.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, naomba niende katika Shirika la Umeme. Niipongeze Serikali yetu kwa kupeleka umeme hadi katika mikarafuu. Hilo ni la kupongeza sana. Mhe. Spika, sasa hivi umeme sehemu zote upo ila kwa hapa niombe Mheshimiwa sifa hizo nzuri, lakini kuna sehemu ndogo Mheshimiwa

katika sehemu ya Mbweni, Shirika la umeme hawatutendei haki, eneo lile kila siku ni lazima umeme uzimwe. Kwa kweli ikifika wakati mwengine ikifika saa 12 kupika ni mashaka, umeme unarudi chini unakuwa haupandi. Kwa hivyo niliombe Shirika la Umeme sehemu ile hili ni tatizo ambalo kila siku linajitokeza, liangaliwe tena kwa jicho la imani ile sehemu kuna wananchi ambao wanatumia umeme lakini unasumbua sana maeneo yale.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa Muda.

**Mhe. Zulfa Mmaka Omar:** Ahsante Mhe. Spika, nikimalizia niunge mkono kwa asilimia mia moja pia niunge mkono watayarishaji katika idara hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.(*Makofi*).

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Zulfa Mmaka Omar. Sasa naomba nimwite Mhe. Said Omar Said na Mhe. Mussa Ali Mussa ajiandae.

**Mhe. Said Omar Said:** Mhe. Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Jaalla Subhana Wataala kwa kuniwezesha jioni hii kufika katika kikao hiki kitukufu. Pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia ripoti hii ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Spika, sitomtendea haki kama sitompongeza Mhe. Hamza Hassan Juma Mwenyekiti wa Kamati hii ambaye ni mwenyekiti mahiri, Mwenyekiti mzoefu, Mwenyekiti Mbunifu, mwenyekiti ambaye aliwashirikisha wana kamati wote katika uandaaji wa ripoti hii tokea mwanzo hadi mwisho namshukuru sana.

Kwa kuwa mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati basi na mimi sitokuwa na mengi isipokuwa nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Ujenzi, nimpongeze Katibu Mkuu wa Mawasiliano, lakini kwa kuwa, "gogotupu haliwaki, gogo na uchanja", niwapongeze watendaji wote wa Wizara ya Mawasiliano kwa kuweza kuunganisha barabara kutoka Wingwi mpaka Mzambarauni. Na kuwafanya wananchi wa Wingwi kuweza kuifikia Wete kwa wakati muafaka, nawapongeza sana.

Pili nichukue nafasi hii ya kipekee kwa kumpongeza Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kuweka *transformer* katika Kijiji cha Kinazini nampongeza sana. Lakini kwa kuwa nyongeza huenda juu ya fungu na kwa kuwa fungu tayari ameshaliweka, basi nimuomba sana Mhe. Waziri akamilishe taratibu zilizobakia ili wananchi wa Kinazini na wao wapate huduma ya umeme kabla ya kufikia bajeti, ikifika bajeti tuzungumze mambo mengine kwamba mwanzo paliwekwa nguzo tano, walikuwa na wasi wasi sana

wananchi kwa nguzo tanzo zile. Lakini ninamshukuru sana Mhe. Waziri kuongeza nguzo hizo na *transformer. (Kicheko/Makofi).*

Kwa hivyo, tunamuomba sana atumalizie ili wananchi wa hapa na wao wafaidi matunda yao ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia anisaidie na mimi nikipita pale pasiwe giza kwa sababu mimi hupita Kinazini wakati wa kwenda Finya, kwa sababu kule Finya nina ubalozi mimi kule. Kwa hivyo ninavyopita pale itakaposimama gari ya Mwakilishi waione, waone kuwa eeeh! ile ni gari ya Mwakilishi wetu, namuomba sana Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika Mahakama ya Ardhi. Mhe. Spika, Mahakama ni moja kati ya mihimili mitatu ya nchi, kama hivyo ndivyo ni wajibu wetu kuilinda mihimili hii na kuitetea kwa nguvu zetu zote. Kama hivyo ndivyo jengo la Mahakama halihitajiki hasa kuitwa jengo la Mahakama ya Ardhi, halifai kabisa kuitwa jengo la Mahakama, kama mwenzangu aliyetangulia ameliona hilo kwa sababu tumekwenda tumeliangalia, tumeona kwamba halifai kabisa kwa sababu mbili kuu za chapchap.

Moja lile jengo la muda mrefu sana lakini sababu ya pili lile jengo la ghorofa, tuangalie migogoro ya ardhi wahusika wa migogoro ya ardhi si vijana lakini wengi ni wazee. Tumchukulie mzee kutoka Nungwi mwenye matatizo ya ardhi baada ya kuuliza uliza akaambiwa aah! mpaka uende Mahakama ya Ardhi. Sasa akajikongoja kongoja mpaka akafika pale pengine amekuja kwa ukongojo, akafika pale anaambiwa panda juu ya ghorofa haya mzee atapandaje juu ya ghorofa. Yeye amekuja na mgogoro wake akifika pale anaongezewa mgogoro tatizo jengine la kupanda juu, hilo la pili. Kwa hivyo ningeomba sana Mhe. Waziri muhusika atayarishe sehemu nyengine, jengo jengine pale pahamwe moja kwa moja kama ni sehemu ya Mahakama ya Ardhi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, ilivyo mtu akitokewa na mgeni, jambo la mwanzo amuonyeshe choo, jambo la mwanzo kabla ya kumpikia chai muonyeshe choo kwanza, pale ndio pa kujisaidia, pengine anakwambia bora niende kabisa kwa sababu kuna wengine hawapendi kukuuliza choo kiko wapi. Kwa hivyo kwanza akifika mgeni muonyeshe pahali pa kujisaidia aah! basi aa kitako hapo. Mhe. Spika, jengo zima hakuna choo, hee! Mahakama hiyo sisi tulishangaa tulisema lakini ndipo hapa tunaambiwa ndio Mahakama hii ya Ardhi, hee! haifai wala halifai jengo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, hakuna hata kifaa cha kuwekea kumbu kumbu za taarifa za watu, mafaili yako chini keshokutwa yanaliwa na mchwa na kesi huwa inachukua muda mrefu, kwa sababu kesi yoyote ile lazima kuwe kuna ufuatiliaji, haiwezi

ikatolewa hukumu kwa sababu hukumu inatolewa kwa uadilifu. Kwa hivyo lazima pawe na ufuatiliaji pengine inaweza ikafika mwaka mzima faili lipo. Lakini kwa kuwa faili halipo katika mazingira mazuri inaweza ikafika hiyo siku ya kesi faili lote limeshaliwa na wadudu pale sasa ushahidi haupo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, tungeomba sana Mahakama ya Ardhi itembelewe na wahusika wengine mbali ya Kamati ili waone huo ukweli, kwa sababu utakapoambiwa tu fulani anakusalimia na yuko hospitali, anakwambia ukamuangalie, wewe utamwambia aah! inshaalla Mwenyezi Mungu atamuokoa atamuafu basi yamepita, lakini siku utakayotoka ukenda wewe hata ukawa na milioni unataka umpe.

**Mhe. Spika:** Muda Mheshimiwa.

**Mhe. Said Omar Said:** Ahsante kwa hivyo naomba sana. Nikitoka hapo nakwenda Idara ya Usafiri na leseni haraka haraka.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**Mhe. Said Omar Said:** Mheshimiwa baada ya hayo naunga mkono ripoti ya Kamati kwa asilimia mia. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa naomba nimwite Mhe. Mussa Ali Mussa.

**Mhe. Mussa Ali Mussa:** Ahasante sana Mhe.Spika, na mimi kwa kuniona ukanipa nafasi hii ili nichangie ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Mimi kwa leo sitakuwa na mambo mengi sana nataka niende kwenye barabara ya Ole/Kianga.

Mhe. Spika, barabara hii ujenzi wake ulianzia 2013 na mpaka leo ni 2017 hapajapatikana hata kilomita moja iliyotiwa lami, barabara hii ujenzi wake umekuwa ukisua sua kwa sababu maalum zinazotambulika si kwa sababu ya vifaa, vifaa ni hivyo hivyo vilivyojengewa barabara ya Kiwani, ndivyo hivyo hivyo vifaa viliviyojengewa barabara ya Wambaa, ndio vifaa hivyo hivyo vinavyojengewa Barabara ya Ole/Kianga.

Mhe. Spika, lakini la kushangaa barabara hizi zote zinazojengwa na UUB zinapoanzishwa wananchi wote wanaitwa kuambiwa kwamba jimbo lenu linataka kupita barabara na likipita barabara kuna vitu vitaathirika, kuna majumba yataathirika, mengine tutayavunja kuna minazi itaathirika, kuna

miembe itaathirika, kuna miti mbali mbali ambayo wananchi wanaitegemea kwa maendeleo yao itaathirika. Lakini watu wa Ole hawakufanyiwa hivyo hawakuitwa kwa sababu wanazozitambua wenyewe wajenzi wa barabara hiyo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, ulipofika wakati wa ujenzi ma-*bulldozer* yameingia kama vile Mapinduzi yamevamia kupindua tu, kumepinduliwa miembe ya watu, kumepinduliwa majumba ya watu hakuna aliyeitwa au Sheha aliyehusishwa katika ujenzi wa barabara ile. La kushangaa na la ajabu wakati barabara ile inaendelea alikuja Mhe. Makamu wa Rais Balozi Seif Ali Iddi akafika Kituo cha Dodeani akawambia jamani mnajenga barabara majengo ya watu mmeyaangalia, haitozuka lawama kama iliyozuka katika barabara ya Gando? Wakajibu Mheshimiwa tumeshazungumza nao, wakijibu hayo nipo wala sikuhadithiwi. Tumeshazungumza nao na hakuna malalamiko yoyote yatakayotokezea na majengo tutayalipa yale yatakayoathirika na tutakayoyavunja.(*Makofi*).

Pale kuna mambo mawili, kwanza kuna serikali halafu kuna na mradi wa barabara. Majengo yatakayovunjwa yatalipwa na serikali, na yatakayoathirika yatalipwa na mradi wa barabara. Lakini linaloathirika linapwa na serikali na linalovunjwa linapwa na serikali. Sasa twende kwenye ulipaji. Nyumba ilioyothaminiwa milioni 14 ikija kulipwa inakuja kulipwa milioni nne na nusu. Hebu Mhe. Spika, nambie leo dunia hii ya leo wakati huu tulionao kuna nyumba ya milioni nne na nusu, hata kiwanja Pemba hupati tena milioni nne na nusu, wacha nyumba, kiwanja hupati!(*Makofi*).

Sasa serikali imebeba lawama kwa sababu ya watu fulani. Nina uhakika kwamba pesa hizi zilizofanyiwa tathmini mwanzo 2014 ndizo zilizotoka lakini sizo pesa walizopewa wananchi. Nyumba ya Mheshimiwa X ilifanyiwa tathmini milioni 65, siku ya kuvunjwa Mheshimiwa X aliitwa kabla haijavunjwa akaambiwa nyumba yako haitovunjwa tena utalipwa milioni 10 lakini itakatwa, basi Mheshimiwa X kwa sababu ni mwanachama wa Chama cha Mapinduzi na anataka maendeleo na anataka barabara na ana hamu ya barabara akasema nyumba ikatwe. Kabla ya nyumba haijakatwa Mheshimiwa X akatolewa katika vyombo vya habari barabara ya Ole Kianga haifanyiki kazi kwa sababu nyumba ya Mheshimiwa X imetuzuia. Sasa nyumba ya Mheshimiwa X haipo na barabara ya Ole Kianga haijajengwa hata nusu mita na nyumba ya Mheshimiwa X imeshavunjwa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, lakini ukweli wa barabara ile hauzungumzwi, ile barabara imeekewa mkono inang'ojewa ije ijengwe tarehe 33, kuna tarehe 15 na 33

Mheshimiwa nataka unielewe vizuri, zamani kulikuwa na 15 na tarehe 25, sasa imebadilika kuna tarehe 15 na 33, maana uongo ukizidi unabadilika inakuwa shaba sasa ule uwongo ushabadilika ushakuwa shaba. Sasa viongozi wa barabara ile kuanzia ma-*engineers*, baadhi yao wanangojea tarehe 33 sio vifaa, vifaa vipo na barabara ipo na kila siku inabanwa. Vile ilivyotanuliwa mwanzo sasa hivi imebanwa vyengine na ikiwa nasema uwongo nawaomba tukiondoka hapa wote twende, iundwe Kamati hapa na mimi katika hiyo kamati nitagharamia nauli ya watu watano. Tukaangalie vipimo hivi ndivyo vya mwanzo na hivi ndivyo vya sasa. Leo nashangaa kuja hapa Mkuu wa Kamati anasifiwa kwa kuisifu barabara ile. Hii si barabara nataka uiangalie barabara Mhe. Spika, inayotoka Mlandege kuja Darajani ile yenye maduka, ndiyo barabara inayojengwa Ole kwenda Kengeja ,iko ndani ya mivungu ya vitanda, kitanda changu unakiona barabara hiyo. (*Makofi*).

Sasa barabara ile watu wenyewe ulemavu watatembea vipi, watoto wachanga watatoka vipi majumbani mwao. Kamati hili hawakuliona, ina maana mwaka huu ijengwe barabara ya Ole na mwakani ije ijengwe hiyo hiyo na mwaka wa mwakani ije ijengwe hiyo hiyo. Hebu twambieni wenzetu wa Kamati kabla sijaiunga mkono hii Kamati mutueleze rasmi barabara ile serikali hii na ijayo na serikali ni hii hii ya Chama cha Mapinduzi, hakuna eti serikali ya tarehe 33, msidanganywe bwana. Maana yake wamekaa kwamba kuna serikali ya tarehe 33 itakuja kujenga barabara ya Ole/Kengeja si kweli, Wallahi si kweli. (*Vicheko*).

Serikali ya Dkt. Ali Muhamed Shein ndiyo serikali itakayojenga barabara ya Ole/Kengeja na imeshaanza, kwa hivyo hizo pesa zitumiwe vizuri na hizo zilizotumiwa tunataka mahesabu. Leo sio pahali pangu hapa pakutaja watu ambao wanahujumu pale. Lakini Mhe. Spika, nitakuja Ofisini kuonana na wewe nikueleze hujuma zilizokuwepo kati ya barabara ya Ole/Kengeja pesa zitakwenda magunia kwa magunia barabara ile haijengwi.(*Makofi*).

Na bahati mbaya ukiwa juu ya tawi ng'ombe si mkali, kwa sababu ng'ombe ana miguu minne hapandi juu. Sasa wewe umeshapanda juu ya muwembe ushakaa juu ya tawi, sasa waliokuwepo chini wote utawaambia ng'ombe si mkali leo bwana tuondokeni. Ndivyo hawa wanavyoambiwa ndugu zangu.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa muda.

**Mhe. Mussa Ali Mussa:** Mheshimia uangalie na uzee. *(Makofi na Vicheko)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Mussa Ali Mussa mchango wako mzuri sana lakini muda si rafiki sana na wewe.

**Mhe. Mussa Ali Mussa:** Basi Mheshimiwa sitaki nivutane na wewe. Na mimi sijui nikwambieje, lakini haya nishachangia.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe nilikusudia muda huu Mhe. Mussa awe ndio mchangiaji wa mwisho, lakini nashawishika kuwapa watu watatu kwa sababu wamenileta kwa maandishi wangependa kuchangia dakika tano tu.

Kwa hivyo nitamwita kwanza Mhe. Abdalla Ali Kombo, halafu nitamwita Mhe. Maryam Thani Juma na Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) watu watatu hawa watachangia dakika tano tano, baada ya hapo tutawapa Waheshimiwa Mawaziri.

**Mhe. Abdalla Ali Kombo:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nakushukuru sana, pia namshukuru kamanda wa Kamati, Makatibu Bi. Fatma na Mussa Choko, wafanyakazi wa Wizara zote wakiongozwa na Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Pemba Bwana Baucha. Ahsanteni sana.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia habari ya kuuzwa kwa Meli ya MV. Maendeleo, nina (a) na (b):-

(a) Kwanza naishauri Serikali isiuze Meli mpaka pale ambapo itanunua Meli, vyenginevyo tutaendelea kuuwa watu kwa sababu hakuna jahazi lolote la Unguja na Pemba ambalo nitashindana na MV. Maendeleo.

(b) Mhe. Spika, MV. Maendeleo kweli ni mbovu tunaambiwa ime-*depreciate* haifai, ingawaje sisi baada ya miaka 60 tunazichukua nyengine. Lakini ukweli wa mambo ni kwamba MV. Maendeleo inachukua tani 600, MV. Mapinduzi II inachukua tani 200. MV. Maendeleo kiuchumi kama MV. Mapinduzi II itaweka milioni moja MV. Maendeleo inaweka milioni kumi. Hayo ni maneno ya waalamu wa Shirika la Meli lakini MV. Maendeleo ni kwamba popote inaweza ikafunga gati, ikapakua na ikatia mzigo haina mashaka. MV. Mapinduzi II haya yote haiwezi. Sasa hivi kuna mpango wa Mapinduzi II kwenda Mombasa kutengenezwa lakini

kutengenezwa kwake tutabakia hivyo hivyo kwamba kila inaposimama kuwe na *pantoni*, sasa itabili tuwe na *pantoni* Pemba tuwe na *pantoni* Unguja tuwe na

*pantoni* Dar es Salaam na kama itakwenda Mtwara tufanye hivyo.

Lakini wasi wasi wangu tena mwengine, meli hii hii ikiuzwa, Serikali yetu itakuja kukodi Meli hii hii kwenda kupakia mizigo.

Mhe. Spika, juzi tulikuwa Mombasa nashukuru nilipata muda wa kuzungumza na ma-*engineers* ama mafundi wa meli na hawa mafundi nimeona meli ikitengenezwa na boti ya Rwanda na meli imekwisha, wakatwambia meli ya MV. Maendeleo mkinunua *engine* itafanya kazi muda tena wa miaka 35. Sasa mimi naishauri Serikali msigeuke jiwe kwa kutizama nyuma lakini ikae tena itazame faida ya MV. Maendeleo na Mapinduzi II. Naiomba sana Serikali kwa ukunjufu na imani yangu basi ikae itafakari tena kitu hiki cha kuuza Meli ya Maendeleo.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, naingia kwenye barabara kidogo tu. Kuna barabara ya Msingini Chake Chake Pemba ni barabara muhimu sana kwa sisi ambao tumesoma Field Castro ni barabara ambayo Marehemu Mzee Kitwana muda wote kama saa hizi tunachukua chakula chetu kwa miaka yote, mimi ningeomba nayo itengenezwe, naikumbuka sana. Lakini pia kuna barabara ambazo mipango miji imezitaja kwamba kuna maeneo sasa hivi Chwaka, Bambi, Mpapa, Gamba, Makunduchi, hii ni miji ambayo mipya.

Ningeomba Serikali sehemu ya Makunduchi, mimi kwangu Magogoni aah! alhamdulillahi kesho kutwa kazi inaanza sina tatizo, lakini ningeliomba Serikali kuna kilo mita 6 za kutoka Kajengwa kwenda Mzuri barabara ambayo Dkt. Kikwete aliahidi ikishawekwa kifusi ataweka lami. Dkt. Kikwete ameondoka hakuna kitu sasa wasi wasi wangu vitu vidogo vidogo kama hivi asije akenda Dkt. Shein akaanza kuombwa tusaidiwe vitu vidogo sana kama hivi. Naiomba Wizara ijitahidi kuitengeneza hii barabara kilo mita 6 au kuweka lami kutoka Kajengwa mpaka Mzuri. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Abdalla Ali Kombo. Sasa naomba kumwita Mhe. Maryam Thani Juma naye atupe mchango wake kwa dakita tano.

**Mhe. Abdalla Ali Kombo**: Mhe. Spika, naunga mkono ripoti ya Kamati hii asilimia mia kwa mia bila ya matatizo. Ahsante sana *(Makofi).*

**Mhe. Maryam Thani Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa dakika hizi chache kuzungumza machache ya Ripoti ya Kamati hii.

Mhe. Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye masuala ya barabara. Katika kutembelea Kamati hii iliona kwamba barabara ya Wete/Chake Chake kupitia Idara hii ya UUB iwalipe fidia wananchi hao waliopo pembezoni mwa barabara hii ya Wete/Chake Chake kabla ya kuanza utengenezaji wa barabara hii.

Mhe. Spika, hili ni muhimu sasa kwa sababu yasije tokezea yale ambayo yametokezea katika ujenzi wa barabara ya Wete/Gando. Mhe. Spika, jambo hili napenda nilizungumzie sana kwa sababu katika utengenezaji wa barabara ya Wete/Gando walipopita kutathminiwa na wakaambiwa kwamba nyumba hizi zinatakiwa wahame, walitathminiwa watu wale lakini baadae baada ya kuhama majumba yale hadi hii leo nilipolizungumzia juzi alipokuja Mhe. Rais, watu wale hawajalipwa lakini namshukuru Mhe. Rais kwa maagizo yake, alioagiza kwa watendaji pamoja na Naibu Waziri kulishughulikia jambo hili. Pamoja na Mhe. Baucha ambaye yupo nadhani hili analisikia walisimamie kwa kina wahakikishe wananchi wale waliokuwa hawajamaliziwa kulipwa fidia zao katika barabara ya Wete/Gando walipwe fidia zile ili wasiwakatishe tamaa wananchi wangu wa jimbo la Gando.

Mhe. Spika, nazidi kulitilia mkazo kuhusu barabara ya Wete/Chake-Chake. Watu hawa Mhe. Spika, walipwe kabisa kutokana na matatizo yasije kujitokeza baadae ya kutengenezwa barabara hii. Vile vile niendelee katika suala hili la barabara ambayo ipo katika kijiji cha Chozi. Nimwambie Mhe. Waziri hichi kijiji akitambue cha Chozi. Kijiji hichi tokea nifahamu kwangu hakijafikishiwa barabara hata kwa njia ya fusi, hakijafikishiwa umeme Waziri wa Maji naye anisikie, pamoja na maji tokea nifahamu kwangu kijiji hichi. Nawaomba Mawaziri hawa wakiangalie kijiji kile kwa macho ya huruma hawana umeme, hawana maji, hawana hata barabara ya fusi. Walione hili kwa jicho la huruma ili kuwatetea nao wananchi wale wafaidi matunda ya Serikali yao ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi).*

Mhe. Spika, niende katika suala la Bandari. Vile vile naipongeza Kamati hii kuitembelea kujua matatizo ambayo yanatukumba Bandari yetu ya Wete na pia napenda kulizungumzia hili niipongeze kwa wazo lao ambao wamelishauri Serikali ya Mapinduzi, kushirikiana na wawekezaji binafsi katika kutujengea bandari ile ya Wete. Mhe. Spika, hili jambo ni muhimu sana kwa sababu bandari hii itakapokamilika na ujenzi huu kupitia wawekezaji wetu na pia na mimi nashauri udhibiti mzuri wa matumizi wa bandari yasimamiwe na Shirika hili la Bandari hata kama wawekezaji hawa watakuja kuwekeza kutujengea gati

ile ya Wete na mimi nawashauri sana Serikali ijitahidi kutufanyia jambo hili haraka haraka kwa sababu tunasumbuka, tunapotaka kusafiri siku ya usafiri wa kuelekea Mkoani kila msafiri huko kishapigishwa na gamu ya kutaka kusafiri kuelekea Mkoani wa ajili ya safari ya kuelekea Unguja.(Makofi).

Hilo nalisisitiza Mhe. Spika, tufanyiwe kwa haraka ili wananchi wote wasipate usumbufu kutokana na Rais wetu wa Zanzibar amekusudia kutuondolea usumbufu wananchi wote wa Zanzibar bila ya kujali itikadi zetu za kisiasa.

Mhe. Spika, baada ya hayo naiunga mkono Ripoti hii asilimia mia moja. *(Makofi).*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa namwita Mhe. Mohommed Said Mohammed.

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Mhe. Spika nikushukuru sana kwa kuniona na mimi nitakwenda ndivyo sivyo, lakini alimradi niweze kukamilisha dakika zangu tano.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Kamati yote, lakini kubwa viongozi sisi wa Afrika siku zote tunapenda kusifiwa, lakini tunashindwa kuambiwa yale maovu yetu lakini leo nataka niseme machache sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kwanza kabisa kwa udhati wa nafsi yangu sijawahi kuipongeza Mamlaka ya Maji tangu kuundwa kwake na mimi niingie Barazani. Lakini leo nasema naipongeza kwa dhati kabisa. Kuna sababu ambazo naipongeza Mamlaka ya Maji. Mamlaka ya Maji sasa hivi imegatua madaraka yake imepeleka Wilayani, itakuwa karibu na wananchi lakini vile vile itakusanya mapato ili ijiongezee kupunguza lile *gape* ambalo la uendeshaji. Mhe. Spika, Mamlaka hii imefikia miaka 11 sasa lakini tulikuwa hatuna au hatuoni faida yake kwa sababu tu inatumia pesa nyingi kuliko zile ambazo zinazokusanywa. Lakini sasa kilio chetu wamekijua wamepeleka madaraka zile Wilayani na tunaamini katika miezi hii wataweza kukusanya vizuri sana, niwapongeze sana. Lakini vile vile visima kumi vilivyokuwa vya Welezo ningewaomba kati ya vile vinne walivyovitia *machine* basi na vile sita vilivyobaki wajidahidi, lakini vile vile takwimu halisi wanotupa kwenye Mamlaka ya Maji mimi nadhani si takwimu halisi wajitahidi sana wakitumie kitengo chao *monitoring and evaluation* kuweza kupata *data* za uhakika, wanapotwambia *data* za uhakika na sisi tunajua kipi wamekosea kipi tufanye ilimradi twende.

Lakini Mhe. Spika nije kabisa kwenye ripoti ya mwenyekiti, mwenyekiti anasema naomba ninukuu baadhi yake

"Kamati yangu ilifika katika eneo la uwekezaji Nungwi ambalo hadi sasa mwekezaji mmoja wa Kampuni ya *Spice Islander* anashindwa kufanya shughuli zake kutokana na mgogoro na mgongano wa maamuzi ya utumiaji wa ardhi".

Mhe. Spika niliwahi kuleta hoja nikasema maeneo hatarishi ya uwekezaji lakini nilikwenda *specific* katika viwanja, sasa leo Makamu wa Pili wa Rais anaungana na mimi moja kwa moja kuhusu *Spice Islander*.

Mhe. Spika, naomba unipe muda kidogo nirudie baadhi tu ya vipengele ya hizi barua, anasema anamuandikia Waziri wakati barua hii imetoka tarehe 2 Oktoba, ambayo mwanzo wake chimbuko lake ilikwenda tarehe 17 Oktoba na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk wakati ule Mwenyekiti wa Kamati ndio aliyesaini sasa. Makamu wa Rais anaungana na mimi kwenye hoja yangu, nataka kusema baadhi:-

"Natumai umeyapata mapendekezo hayo nakala nimeziambatanisha kwa rejea yako ya mara moja kwa kina tumetafakari hatua zilizochukuliwa kutokana na mapendekezo hayo, kwa kweli Wizara yako ikiendelea na mtindo huu ni wazi kabisa kuwa tutaweza kuwavunja moyo na kuwapoteza wawekezaji ambao wamekuwa na hamu ya kuwekeza katika nchi yetu baada ya kuhamasisha waje nchini kwetu kuwekeza hasa katika sekta ya utalii. Mimi nakubaliana na *(Makamu wa Rais anasema siyo mimi)* mapendekezo hayo na ninakuomba uchukue hatua zinazostahiki kuwarejeshea *Spice Islander Limited* eneo hilo ili waweze kuendeleza na ujenzi wa mradi wao madam tayari kibali cha *ZIPA* wanacho siku nyingi" *(Makofi).*

Mhe. Spika, nimekuwa nikiganda hapa, utendaji gani, uwajibikaji upi wa Serikali yetu wakati Makamu wa Pili wa Rais anaagiza anakubaliana na hoja zetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini tunawaita wawekezaji waje. Inashangaza sana na hapa ndio niliposema nitasema yale mapungufu yetu tusikubali tu kila siku kuambiwa mazuri, lakini yale mabaya ambayo yapo tukubaliane nayo uwajibikaji hapa uendelee. Mhe. Waziri nikuombe umeingia, Mhe. Jembe na kila kitu endelea kufanya kazi na naamini unaweza kuwapa hawa mara moja.(*Makofi*).
Lakini Mhe. Spika, niingie katika Shirika la Nyumba haraka haraka...

**Mhe. Spika:** Muda Mheshimiwa.

**Mhe. Mohamed Said Mohamed**: Kuna nyumba zetu za Kilimani niwapongeze sana, nimpongeze Mkurugenzi tulifanya ziara na Naibu Waziri, Mkurugenzi wa Nyumba, Mkurugenzi wa Manispaa kuona hali halisi ya wananchi wa Kilimani wanaishi katika hali ngumu sana. Mhe. Spika, ningeomba hata wewe na Baraza lako tukufu twende ukaone sehemu ambayo kama wanadamu wanaishi pale haifai, na sasa kuna lugha nashindwa hata kuitumia kinyesi kiko nje kabisa pale chini.

Mhe. Naibu Waziri nimekwenda naye mara nyingi, wananchi wale wanapata tabu nachelewa sana kusema mwezi wa tatu huu na Masika inaingia wanatapata tabu sana. Naomba Serikali msikie kilio hiki cha wananchi tukisema siye mkiona mtu mzima analia kuna jambo.

Mhe. Spika nakushukuru.(*Makofi*).

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe sasa nianze kumwita Mhe. Juma Makungu Juma Naibu Waziri wa Maji ili atowe mchango wake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Ahsante Mhe. Spika baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nikushukuru na wewe pia kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia ama kukazia mawili matatu kwenye Ripoti ya Ujenzi na Mawasiliano. Lakini pia niwapongeze kwa dhati Kamati hii kwa kazi kubwa na ngumu na nzuri ambayo wametuwasilishia kwenye Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, mimi niende kwenye ukurusa wa 9, hapa kwenye changamoto zinazolikabili Shirika la Umeme. Moja kuna deni kubwa limewekwa hapa ambalo linadaiwa Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) bilioni kumi na tisa milioni tisa thalathini na saba mia tisa na kumi na tisa na pesa hizo za juu. Hii ni kweli lakini pia imetajwa sababu kwa nini *ZAWA* inadaiwa deni hili. Nasema kutokana vituo vya uzalishaji wa maji. Hapa nilikuwa nataka nioneshe haja ya wananchi wetu kuchangia maji kwa sababu *ZAWA* pana kazi kubwa ya kufanya na taasisi hizi ziko kama *chain* zinategemeana, kutoilipa *ZAWA* au kutoichangia ZAWA kuiathiri tu *ZAWA*, athari yake inakwenda kwenye taasisi nyengine lakini na taifa kwa jumla. Kwa mfano hapa pesa hizi ambazo wanadaiwa na *ZECO*.

*ZECO* wanashindwa kulipa deni ambalo wanadaiwa na *TANESCO* lakini chanzo utakuta ni huku kwenye wananchi. Sasa mimi niombe na niwaombe

sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa ujumla tukamataneni mikono na *ZAWA* kusudi kwa pamoja tunashinda kupunguza tatizo hili la maji katika maeneo yetu.

Lakini Mhe. Spika, pia niende kwenye suala la hati umiliki wa matumizi ya ardhi. Kuna malalamiko mengi kwamba hizi hati zinachelewa kupatiwa wananchi lakini nimekuwa nikisema hapa kwamba kuna utaratibu mpya wa hati mpya ambao uko hatua za mwisho kwa ajili ya kuwafikia wananchi, na tumesema kuna hili kwa sababu ya kupunguza ile migogoro ya ardhi, lengo ya hizi hati mpya ni kupunguza migogoro ya ardhi.

Lakini hati peke yake haitosaidia, lazima lile ambalo naendelea kusema la kufuata sheria liendelee kufuatwa. Kwa mfano tumesikia baadhi ya Wajumbe wakilalamika namna ya urasimu ama rushwa katika baadhi ya mashirika. Lakini naomba nitanabahishe kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, na wananchi kwa ujuma wanapofuata huduma basi wapate katika taasisi husika, wende ofisini na sio wakimkuta mtu aidha sokoni ama sehemu nyengine kwa vile tu anafanyakazi kule wakamalizana huko, lawama hili halitobebwa na taasisi husika, atakuwa ni jukumu la mwenyewe aidha mwananchi na huyu mtu ambaye wamekutana huko, malalamiko tuliyokuwa tunayapokea na tunaomba sana tuletewe taarifa hizo ni zile urasimu ama malalamiko mengine yoyote ambayo yanahusiana na rushwa lakini yaliyokuwa yamefanyika kwenye ofisi husika.

Lakini Mhe. Spika tukitoka hapo niende kwenye suala la uwekwaji wa nguzo katika viwanja vya michezo. Kweli kuna baadhi ya viwanja vina nguzo za umeme lakini kuna haja maalum zimelazimisha kuwepo pale, vyenginevyo maana yake Shirika la umeme Zanzibar litakuwa na wajibu wa kila siku ikitokezea ile haja liende na nguzo na nyaya, kwenda rudi, kwenda rudi. Lakini kwa busara kabisa ikaoneka ni vyema zile nguzo zibakie pale lakini uwekaji wake umezingatia sana kuathiri vile viwanja husika.

Lakini Mhe. Spika nimalizie kwa upande wangu kusema kwamba ni kweli kuna Wazee ama Washauri wa Mahkama ya Ardhi wanadai na hasa kwa upande wa Unguja, hili tunalifamu na hatujalidharau lakini pia tushukuru sana Kamati kwa kukumbusha lakini pia kwa Wajumbe kulikazia kukumbusha hili.

Kwa ufupi niseme tumekumbuka Inshaallah. Baada ya hayo Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante sana *(Makofi).*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Juma Makungu Juma Mhe. Naibu Waziri wa Maji. Sasa naomba nimwite Mhe. Mohamed Ahmada Salum Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nichukue nafasi hii kushukuru kwa kunipa nafasi na mimi angalau nichangie kwa uchache sana yale ambayo yameelezewa na Kamati yetu pendwa ya Mawasiliano na Ujenzi.

Kwanza mimi nichukue nafasi hii kwa kushukuru sana Wajumbe wote wakiongozwa na Mwenyekiti mahiri Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Shaurimoyo. Kusema la ukweli tulikuwa nao usiku na mchana kwenye shida kwenye raha, lakini mwisho wa siku yeye ametoka Iran na kuja kuisimamia mwenyewe taarifa hii, nampongeza sana kwa hili kwani hili ni jembe lisolo mpini.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kusema la ukweli wizara yetu ni wizara ambayo ni kiungo kikubwa sana katika uchumi wa Zanzibar na vile vile kufikia maendeleo ya dira ya 2020. Najua Wajumbe wengi wamezungumza kwa hisia pale ambalo wameona changamoto na vile vile wametoa hongera na pongezi pale ambapo wameona sisi tumefanya kazi vizuri. Nina imani kubwa sana chini ya uongozi mahiri wa Dk. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nina imani kubwa sana tutafikia hatua kubwa sana ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM.(*Makofi*).

Mimi naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi watuamini, wawe tayari kutuunga mkono na kuonesha mashirikano ya kutosha kabisa katika kuhakikisha kwamba yale tuliyoahidi kwa wananchi basi tunayatekeleza kwa vitendo ili baadaye 2020 ije kuwa hamna mtu wa kusema kwamba CCM haikufanya, kitu lakini CCM imefanya kitu na inabidi ipewe tena fursa ya kuongoza na nina imani kubwa sana CCM itaendelea kuongoza daima na Mapinduzi daima. *(Makofi).*

Kwa ufupi changamoto ni nyingi zilizozungumzwa lakini napenda kuwatoa wasi wasi wananchi pamoja na Baraza lako tukufu hili, wamezungumzia kuhusu *Terminal two*, nataka kuwatoa wasi wasi kwamba *Terminal two* nitatumia juhudi na maarifa yote kuhakikisha kwamba ujenzi ule wa unaendelea. Ni karibuni tu tulikuwa na Mhe. Makamu wa Rais katika ziara ya China tukakutana na watu wa *Exim Bank* na nina imani kubwa na karibuni tu Mhe. Waziri wa Fedha alipokwenda China amekuja na salamu nzuri sana kwa Wawakilishi na wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, wale wote waliokuwa

wakitegemea kwamba mkono wa binadamu utaanguka ili fisi aukamate au aumeze basi wamechelewa.(*Makofi*).

Kweli kama nilivyojibu jana zipo changamoto ambazo zimetokeze na nikazungumza kwamba changamoto zile zote tutazifanyia kazi na vile vile Mshauri Elekezi yule ametuwekea utaratibu mzuri sana hadi kufika pale jengo lilipofika, basi nina imani kubwa sana, ule ni ushauri wake na ushauri ule umekubaliwa mpaka *Exim Bank* nao wakakubali kuendelea kuufadhili ule mradi.

Mhe. Spika, Waingereza wanasema wana msemo wao, '*better late than never'*. Kwa hivyo hata kama tunachelewa lakini afadhali kuliko kuwa hatuna kitu. Kwa hivyo, nina imani kubwa sana kawia lakini tutafika na uwezo wake Mwenyezi Mungu.

Tukija suala la M.V. Mapindui II, kama nilivyojibu jana napenda kuwatoa wasi wasi wananchi ile meli ina viwango vyote vya ubora na iwapo sisi hivi sasa tuichokorowe kwa aina yoyote lawama itakuja kutuangukia sisi na hiyo lawama inayotuangukia sisi, basi itakuwa ni aibu kwa taifa letu. Nakuombeni sana ile meli kwa hivi sasa tuiwacheni kama ilivyo maumbike yake afadhali tuangalie miundombinu tutaitengeneza vipi lakini kwa ile meli naokuombeni sana, ile meli imejengwa kwa kiwango cha kimataifa ni meli ambayo iwapo utaitoboa sehemu nyengine yoyote basi kuna hatari kuja kuzama kama *M.V. Skagit* basi watakaokuja kulaumiwa ni sisi Serikali.

Kwa hiyo, mimi nawashukuru sana Kamati wamekwenda Mombasa wamepata ushauri kama huo tunaukubali ushauri wao lakini kwa hili tunaomba waiache ile meli kwa hivi sasa iendelee vile vile. Sisi hivi sasa tuko katika mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba M.V. Maendeleo II pamoja na meli hii ya mafuta tuko katika utaratibu wa kutaka kuhakikisha kwamba katika bajeti ya 2017/2018, basi kama tulivyoahidi katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwamba tunanunua meli mpya tutatekeleza ahadi hiyo chini ya uongozi mahiri wa Dk. Ali Mohamed Shein. Msiwe na shaka tumejipanga na Inshaalah ikija bajeti ya 2017/2018 mtaona mambo na sasa hivi tuko katika hatua nzuri, Kamati yetu inaendeleza vizuri na kazi na karibuni tunatakutana na Mhe. Waziri wa Fedha kwa ajili ya mipango zaidi. Lakini hili ni agizo la Mhe. Rais na sisi hatuwezi kulikataa na tutalitekeleza kwa haraka sana.(*Makofi*).

Mhe. Spika, Wajumbe wametushauri kuhusu M.V. Maendeleo hii ambayo sasa hivi ipo. Ni meli chakavu, mimi juzi nimeitembelea kusema la ukweli tukatoa

agizo tuisitishe isifanye safari yoyote. Kwa hivyo hivi sasa uamuzi uliotoka tuendelee na utaratibu wa kutaka kuiuza M.V. Maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wako waliosema kwamba wamekwenda Mombasa wakapewa ushauri huo, basi mimi pale itakapokuja kutoka *tender* kuja kuuzwa ile meli, basi wajipange ili wainunue na nina imani kubwa sana itatusaidia vile vile kwani tutakuwa tuna meli nyengine zaidi. Lakini kwa sisi Serikali tumesema hatuihitaji tena ile meli pamoja na M.V. Ukombozi tutafute meli mpya za kisasa, ikiwa mashirika binafsi yameweza, makampuni binafsi yameweza, kwa nini Serikali tushindwe, nina imani kwa hili hatutoshindwa.

Mhe. Spika, vile vile limezungumzwa suala la barabara. Natoa ahadi kama alivyosema Mhe. Rais Ilani yetu ya Uchaguzi imezungumzia barabara ambazo zimetajwa mle na vile vile viporo ambavyo vilivyokuwepo hapo kabla. Mhe. Rais ni msikivu anaumwa sana tulipokuwa tunatembelea barabara ya Jendele hadi Unguja Ukuu Kaibona kwa kuumwa na kuona sisi tunavyotengeneza barabara tukiwa na vifaa chakavu, akaenda moja kwa moja kuangalia ule mtambo wetu wa lami, baada ya kuuona akatoa agizo kwamba Wizara inahitaji kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuwapa watu wa UUB wafanye kazi, kwa sababu zile kazi wanafanya UUB kama mulivyowapongeza hapa, ni kazi za kupigiwa mfano, wanafanya kazi katika mazingira magumu, vifaa chakavu lakini licha ya hivyo barabara ya Jendele mpaka Unguja Ukuu Kaibona akipenda Mwenyezi Mungu mwezi wa Machi tunaimaliza. (*Makofi*).

Kwa vifaa hivyo hivyo chakavu tumeweza kumaliza barabara ya Kiwani Mgagadu na nashukuru sana wananchi kule ambao wameweza kuruhusu vipando vyao tusivilipe fidia ili ile barabara ifike kwa sababu ni barabara ya muda mrefu, lakini nawashukuru sana na ni karibuni tu Mhe. Rais atakwenda kuifungua barabara ile ili kuwaonesha Wazanzibari na wale wengine waliokuwepo nje kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein ni Serikalini makini na itaendelea kufanya mambo makini hadi 2020 kwenye uchaguzi mwengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile nizungumzie kuhusu Shirika la Nyumba, tumepewa ushauri na sisi tunajiopanga sasa hivi tunataka kuona kwamba na tunajenga nyumba za bei nafuu ili wananchi wetu hasa wanyonge wakwezi na wakulima nao wanafaidika na matunda matukufu kama walivyofaidika katika majumba ya hivi sasa ya Michenzani, Kengeja, Mkoani, Wete, Gamba, Bambi, Mpapa na sehemu nyengine ambazo majengo yale yamejengwa na muasisi wetu mpaka Makunduchi samahani sana, yalojengwa na muasisi wetu marehemu Abeid Amani Karume. Tuna nia ya dhati na Inshaallah kwa uwezo wake Mwenyezi

Mungu tunajipanga na baada ya muda nina imani kwamba tutafanikiwa kwa hili.(*Makofi*).

Kwa hivyo ushauri wao wa mambo ya *Motel bank* na mambo ya kuwaomba wenzetu wa Shirika la Nyuma Tanzania Bara, sisi tutakaa na Wakurugenzi wetu wamekuwa kila siku wakienda kuomba ushauri, na ushauri nina imani karibuni utaleta tija. Kwa hivyo niwatoe wasi wasi nina imani kwamba watakuwa pamoja na sisi katika kuhakikisha Shirika la Nyumba tunalipa uwezo zaidi pamoja na ushauri wakati wa kutekeleza majukumu yake. Kwa hivyo nataka niwatoe wasi wasi tunajua kuna changamoto, uhaba wa fedha lakini kupanga ni kuchagua na nina imani kubwa sana kwa vile tulivyojipanga basi tutafika hatua nzuri sana.

Mhe. Spika, wameelezea kuhusu uchakavu wa majengo tumeuona tunakiri hayo kama ulivyosema kuna ugumu fulani, lakini tumeanza na *Pilot Project* wenzetu walikuwepo tulipokwenda Pemba kule Chake Chake na ile *Pilot Project* walofanya kule kwa gharama nafuu basi nitaomba watendaji wangu wa Shirika la Nyumba waje kutoa ushauri, ili maeneo aliyosema Mhe. Mohamed Said Mohamed kama Kilimani basi ule uchafu tunauondoa kwa gharama nafuu. Mhe. Spika, wenzetu wamejipanga kule kwa gharama nafuu sana wameweza kufanya hiyo kazi na nina imani kubwa sana na Unguja tutaifanya kazi ile kwa gharama nafuu na Inshaallah tutafanikiwa na haya matatizo ya maji taka pia yataondoka.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka nizungumzie jengine ambalo limezungumzwa sana kuhusu barabara ya Ole/Kengeja ni ya kilomita 35. Napenda kuwatoa wasi wasi wananchi ile barabara tutaijenga na katika bajeti hii tumekusudia kujenga kilomita 11. Kwa hiyo, Mhe. Mussa kama kuna watu wanataka kuleta jambo lolote au kuhakikisha kwamba ule mradi unakwama, basi mimi nawaambia kama ulivyoweza kufanikiwa mradi wa Mgagadu/Kiwani na ule mradi utafanikiwa na kama kuna mtu tukijua sisi analeta *sabotage* yoyote basi hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake. (*Makofi*).

Mhe. Spika, vile vile tumezungumzia kuhusu watu ambao katika Shirika la Nyumba wanaotumia nafasi zao katika kuwatapeli watu. Mimi namuomba mheshimiwa aliyesema kwamba tatizo linakuja vipi? Mtu anakwenda kukutana na wafanyakazi wa Shirika la Nyumba mfano anaambiwa kuna nyumba fulani ya kilemba alete kiasi fulani, wanafanya makubaliano huko wanapokwama sasa ndio unaona wanakuja kwetu kutuelezea yale mambo. Sasa iwapo wangeliona lile jambo mapema lingeweza kuja kwetu hayo ni katika masuala ya rushwa. Kwa hiyo, tungekwenda kuonana na taasisi za Kutoa Rushwa tukawaambia

waweke mtego, yule mfanyakazi tukamkamata. Lakini unanambia suala hilo baada ya miezi 11 kupita inakuwa tayari na wewe mwenyewe umeridhia, kwa hiyo inakuwa ngumu kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, vile vile kwa ufupi nizungumzie kuhusu Mhe. Mwantatu amenigusa hisia sana kuhusu watu wenye ulemavu kupata tabu wakati wa kupita kwenye njia zetu pamoja na wenye ulemavu wa uono. Tunachukua changamoto hii na tutahakikisha kwamba tunaifanyia kazi ili na wao pia wajione ni sehemu ya jamii na wao wakafaidike na matunda yetu ya Mapinduzi.(*Makofi*)

Kuna suala amelizungumzia kuhusu utapeli unaofanyika hivi sasa. Kwa mujibu wa sheria ile ya Makosa ya Mtandao ambayo sisi tumeridhia tarehe 28 Septemba, 2016. Sheria Nam.14 ya 2015 inasema hivi, "Baada ya muhusika kwenda Polisi, Polisi anapopata yale madai ni wajibu wake sasa kufuatilia katika kampuni hiyo ya simu ambako kumetokea lile tatizo kwa kushirikiana na watu wetu wa *TCRA* ili kuhakikisha sasa huyu mdai anapata huduma zote mpaka tuhakikishe kwamba yule ambaye amemtapeli yule muhusika tunampata na tunampeleka kwenye vyombo vya sheria".

Kwa hivyo, mimi niwaombe sana na pia nitumie Baraza hili lako Tukufu kutoa elimu. Limezungumzwa suala kwamba kuna watu wanawadhalilisha viongozi katika mitandao. Sheria ile tayari tumeshairidhia, kwa hivyo naomba sana Wawakilishi wanapoona jambo kama hili waisaidie Polisi kuwapelekea taarifa, Polisi kwa kutumia taratibu zao nina imani kubwa sana watachukua hatua baadae wale wahalifu wote kupelekwa katika vyombo vya sheria.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na napenda kuwaarifu kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 108(15) ambacho kinatutaka sisi tulete taarifa kuhusiana na ripoti hii mwezi wa Septemba au Oktoba basi tutaifanya kazi hiyo, lakini niwapongeze sana Kamati ile ushauri wao tumeupokea na tutaufanyia kazi na vile vile niwashukuru sana Wajumbe kwa ushauri wao.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naye aweze kutoa mchango wake kidogo.

Mheshimiwa karibu sana.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema aliyetujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana hapa saa hizi.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya uongozi wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira tunapenda kutoa shukurani zetu za dhati kwa Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano yao makubwa na mazuri waliyotuonesha katika kuleta ufanisi na maendeleo ndani ya sekta zetu unapatikana. Mhe. Spika, shukurani zangu maalum napenda nizitoe kwa wachangiaji wote 25 ambao wamekuwa makini kabisa katika kujadili, kufafanua na kuhakikisha changamoto zilizojitokeza zinaboreshwa na kufanyiwa kazi ipasavyo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, shukurani za pekee naomba pia nizitoe kwake binafsi Naibu Spika na Wenyeviti wote pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa umahiri wenu katika miongozo mbali mbali ndani ya Baraza hili. Mhe. Spika, leo sikusudii kujibu hoja zilizotolewa na Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu ili naomba nizipokee hoja hizi na niende kuzifanyia kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba na mimi sasa hivi niweze kutoa michango yangu kwa ufupi sana kwa baadhi ya sekta ambazo ziko chini ya wizara yangu. Mhe. Spika, naomba nianze na sekta ya nishati na nianze na *ZECCO*. Niendelee kwa kuomba tena kuwashukuru Wajumbe wote waliotoa pongezi na ushauri kwa namna moja au nyengine kwa Shirika letu la Umeme (*ZECO)* kwa kweli wanastahiki pongezi hizo kwa kazi kubwa wanazozifanya ila naomba niseme mambo mawili katika sekta hii. Nianze na suala la kiwango cha mshahara kwa mtumishi ambaye ameonekana hana *master degree*.

Mhe. Spika, kiwango cha mshahara katika mashirika ya umma yanakuwa *co-ordinated* na *Board of Directors* kutokana na kiwango cha elimu, lakini *experience* aliyonayo na unyeti wa kazi anayoifanya, na hili si suala geni katika mashirika ya umma na tukiangalia muhusika yeye ni *co-operate secretary* wa *Board of Directors*. Kwa hivyo, mpango wa viwango vya mishahara ni moja ya jukumu leo kwa mujibu wa sheria na kanuni. Mhe. Spika, hata hivyo hili naomba bado niendelee kulipokea na nitaendelea kulihakiki, kwa sababu kiwango ambacho nimekiona katika kile kielelezo ilikuwa ni *grade II RL25* ambayo imethibitishwa na hiyo *Board of Directors*.

Lakini katika suala la *ZECO* pia nilikuwa naomba sana nizungumzie suala la deni la *TANESCO* ambalo limezungumzwa hapa limefikia bilioni 63. Lakini

naomba niwajuulishe Wajumbe mpaka kufikia Januari, 2017 kwa barua niliyoipata juzi siku mbili nyuma tunadaiwa bilioni 121 na *TANESCO,* naomba kuweka hesabu sawa.

Mhe. Spika, suala hili lipo katika mazungumzo katika ngazi ya Mawaziri, sisi binafsi Mawaziri wa wizara mbili hizi tumeshakaa na tulivyokaa tulitoa maagizo kwa Shirika la *TANESCO* na Shirika la *ZECO,* kuna kazi tuliwapa na tumewapa muda pia na tukawaambia wazungumze yale watakayokubaliana na yale yasiyokubaliana, wapitie kwa Makatibu Wakuu wetu kupeleka taarifa na hatimae kutuwasilishia sisi Mawaziri. Na kazi hii tumeitoa kabla ya tarehe 30 Machi basi kazi hii iwe tushakabidhiwa ili tuweze kuifanyia kazi ipasavyo. Ninaamini kabisa kwa makubalino tuliyokubaliana na mwenendo ambao tumeanza kwenda nao basi nina hakika Mhe. Spika na Wajumbe kwamba tutalimaliza kwa busara kubwa bila ya kuwa na tatizo lolote.

Mhe. Spika, katika sekta ya nishati naomba pia nizungumzie suala la *ZURA*, suala ambalo lilikuwa lina utata kidogo kuhusu kuchangia Dola 10 kwa kila lita moja ya mafuta kwa mafuta yanayoletwa Zanzibar ambayo inakuwa ni tofauti ukiangalia na maeneo ya jirani yale yanayopita pale. Kwa kweli suala hili tumeliona na mimi mwenyewe binafsi tayari tushalipeleka tumekaa na Waziri mwenzangu kuona tufanya nini, lakini kwa bahati mbaya sana hatujaaza kulifanyia mazungumzo tumekubaliana tulimalize la *ZECO,* lakini hili tuliliacha katika ngazi ya chini kabisa *EWURA* na *ZURA* wenyewe waweze kuzuangumza halafu sisi tuweze ku-*interact* lakini sisi binafsi kama Waziri bado hatujaanza kulifanyia kazi lakini kwa mwelekeo huu tutaendelea kuongeza jitihada ya kuweza kulifuatilia suala hili.

Mhe. Spika, katika sekta hii ya nishati naomba nizungumzie pia kuhusu suala la TUKUZA ambalo limezungumzwa. Kwa kipindi ambacho mimi nimeingia madarakani mpaka leo tushafunga mita 5,690 katika maeneo mengi ya Mjini kama vile Sogea, Kwaalimsha, Mikunguni/Nyerere, Mikunguni/Amani, Ziwatuwe na Saateni. Na katika mwezi huu wa Machi tumejipanga kwenda Makunduchi na Kizimkazi. Kwa hivyo, *speed* ya kufunga mita za TUKUZA zinaendelea na tuna *operation* kabisa mkakati madhubuti ya operation TUKUZA kuhakikisha kwamba mita zile za zamani zote tunaziondoa katika nyumba za makaazi na kuhakikisha kwamba wananchi wote wanatumia TUKUZA.(*Makofi*).

Lakini vile vile nizungumzie suala la *ZURA* zile sheria za migongano. Wiki moja nimekwenda kufungua semina *ZURA* ya *Board of Director* tatu ya *ZURA, ZAWA* na *ZECO* ambazo zilikaa pamoja kuona namna gani wataboresha

utendaji wao wa kazi, kwa sababu kweli naomba nikiri kwamba sheria nyengine zinakizana. Kwa hivyo, moja ya maazimio ni kuangalia zile sheria ambazo zinagongana ili hatimae zifanyiwe kazi, na bahati nzuri Waziri wa Katiba na Sheria alishatoa agizo kwamba zile sheria ambazo tunaziona kwamba zinataka kufanyiwa *amendment* basi zifanyiwe na ziweze kuwasilishwa kwake. Kwa hivyo, hiyo inaendelea kufanyiwa kazi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, naomba niende kwenye sekta ya ardhi kwa ruhusa yako. Hapa naomba kidogo nieleze kidogo. Mimi naomba kwamba sisi sote tunajua kama ardhi ni mali ya serikali na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hapa tupo kwa ajili ya kutunga sheria, kusimamia sheria lakini pia tunazo tuweze kuzisimamia zile sheria tunazozitunga pia na kupitisha na kuidhinisha bajeti ambayo serikali kuu inaitoa katika taasisi zake, ikiwemo mishahara ya watumishi wa serikali. Na ninaomba niseme kwa kuwa viwanja vya serikali wakati vinatolewa vina utaratibu wake, sio kama vinatolewa tu kama vile vyengine. Ili mtu upate kiwanja cha serikali lazima uombe na ukiandika barua ya maombi unapewa fomu ya kuweza kutoa taarifa zako, na katika fomu zile zina nafasi nyingi na maelezo mengi, lakini moja ni *source of income* ya kujenga, lakini utajenga kwa kipindi gani na maswali mengi ambayo yamo ndani ya fomu ile. (*Makofi*).

Lakini ukishakumaliza kuijaza fomu ile ukirejeshewa, ile kamati ikishakukaa kuzipitia kwa wale wanaonekana kwamba wanaweza kwa hivyo wanapewa vile viwanja kwa *provision certificate* shahada ya muda ya matumizi ya hati, hawapewi *right of occupancy*, wanapewa shahada ya muda ambayo kutokana na sheria ambazo zimetungwa ndani ya Baraza hili, Sheria Nam. 12 ya 1992, kifungu cha 33 (1), (2), (5) ambacho kinaeleza wazi waliweka utaratibu ndani ya Baraza hili namna gani ya kutumia zile. Lakini yule akipewa kile kiwanja wakati anapewa ile *provision certificate* anatakiwa akubali masharti na kuweza kuweka *sign* yake. Na muhusika anakubali masharti na anaweka *sign* yake, *unless* kama kwenye taarifa ya fomu alivyojaza hakutoa taarifa sahihi lakini anakubali na kuchukua.

Lakini nini kimetokea kupelekea hapa tulipofika. Miji yetu haikuwi watu wanalalamika miji haipangwi, lakini miji inapangwa, miji inakua. Naomba nianze viwanja vilivyotolewa mwaka 1984, miaka 33 sasa hivi vya Mpendae kuna viwanja 19 mpaka leo havijajengwa. Sasa kama tunaviwacha viwanja hivyo viendelee kukaa hivyo haiko sawa. Lakini kuna viwanja vilivyokaa miaka 20 mpaka 25 maeneo ya Magogoni, maeneo ya Mombasa na maeneo mengine bado havijajengwa. Viwanja vya mwisho vilikuwa ni viwanja vya Tunguu ambavyo sasa hivi vina miaka 5 ndio viwanja pekee ambavyo vina

muda mfupi, lakini viwanja vyengine vyote vya muda mrefu maeneo mengi bado hayajaendelezwa.

Lakini katika hali hiyo hiyo kuna maeneo mengi wamepewa wawekezaji ambayo watu wengi hapa yaliyazungumzia kwamba yamewekwa makuta, lakini hakuna uendelezaji, serikali inakosa mapato, wananchi hawafaidiki na ardhi ile. Kwa kweli si sawa hata kidogo kama hatutokaa tukasimamia sheria zetu. Kwa hivyo, tumefika pahala tumesema hapana, "*enough is enough"*, lazima tufike pahala tusimamie sheria tuone kwa pamoja tunafanyaje.(*Makofi*).

Mhe. Spika, katika haya maeneo ya wawekezaji tutaendelea pia kuyafanyia kazi kuhakikisha wale wote waliokuwa hawajaendeleza basi tutaendelea kuchukua hatua na utaratibu wa sheria kama ulivyo, na naomba niseme kwamba ufutaji wa viwanja ni kazi endelevu haijaanza leo na ipo na itaendelea kuwepo kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Kwa hivyo mpaka hapo Baraza hili lako tukufu Mhe. Spika litapokaa na kusema kwamba sheria hizi hazikidhi mahitaji. Sheria hizi sasa tuzibadilishe, tukishakubadilisha sheria basi tutaongozwa na sheria na ambayo tutaibadilisha ndani ya Baraza lako tukufu. Na naomba niseme Mhe. Spika, kwa ruhusa yako mimi nipo tayari kufuata mapendekezo yenu, kufuata ushauri wenu, tukisema tuweke miaka 50, miaka 20 basi sisi kama wizara tuko tayari kufanya hivyo. Lakini bado tutaendelea kusimamia sheria. (*Makofi*).

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kusema katika hili naomba kidogo nifafanue. Kuna changamoto nyingi sana ambazo tumeziona. Kwanza kuna ubadhirifu mkubwa kupitia viwanja ambavyo tunavitoa ndani ya serikali. Kuna watu wanamiliki viwanja vingi, kuna watu pale wameweka ile kama kitega uchumi kwamba leo nimechacha basi nikachukue milioni yangu hamsini niuze kiwanja. Hata hao wanyonge tunaowapigia kelele pale hawapo, lakini kuna watu wachache sana waliokuwepo, lakini kuna watu wako huko wamekaa wanasubiri serikali wanayoitegemea ije ndio waje kuendeleza. Sio sawa sisi kama viongozi na kama watu wa kusimamia sheria inabidi lazima haya tuyasimamie na tuyafanyie kazi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, mwengine unamuuliza kwa nini hujajenga mpaka leo miaka imekuwa mingi, anakwambia aah! serikali hii siwezi kujenga. Kwa hivyo, huwezi kufika pahala kama Waziri, kama kiongozi unayetakiwa kusimamia sheria ukimfikiria Mhe. Rais anatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na dhamira yake anaondoka akihakikisha kwamba miji hii iko vizuri, miji iliyopangwa inaonekana. Kwa hivyo, hili naomba niliseme na inshaallah Mwenyezi Mungu atatusaidia katika kulitekeleza hili. (*Makofi*).

Mhe. Spika, lakini naomba niende kwenye sekta ya maji, nakwenda haraka haraka kwa sababu sekta zangu ni nyingi. Mhe. Spika, katika sekta ya maji ZAWA, changamoto zipo nyingi sana lakini dhamira yetu kama serikali hasa ukizingatia umuhimu wa maji katika uhai wa binadamu na viumbe vyote ni kuhakikisha kila mtu anapata maji safi na salama mijini na vijijini. Dhamira ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein ni njema, jitihada mbali mbali tunazichukua na anazichukua kila anapokwenda basi anakwenda kuona namna gani atapata fedha kwa ajili ya kuekeza kwenye maji. Kwa hivyo, mimi naomba tumuunge mkono ili tuweze kuendeleza juhudi hizi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la ugatuzi kwa sasa hivi kila Wilaya kutakuwa kuna *full team* ya uongozi wa maji chini ya Afisa Wilaya husika. Waheshimiwa Wajumbe kwa kuanzia naomba mridhie kuanza na utaratibu huu ambao utakamilika mwaka huu. Hivyo, kwa kuwapa Maafisa kwa kila jimbo ushauri tunaupokea lakini kwa sasa hivi bado hatujafikia.

Mhe. Spika, pia niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kushirikiana, kazi hii ni yetu yote kwa pamoja katika kuhamasisha wananchi wetu kuchangia huduma ya maji ambayo inapatikana kwa mgao. Kwa sasa hivi wananchi wanachangia asilimia 35 tu ya maji na serikali inachukua mzigo wa kuchangia asilimia 65. Kwa maeneo ambayo hawapati maji kabisa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kushirikiana tuhakikishe juhudi zetu kama Mamlaka na wizara basi matatizo haya tutaweza kuyaondoa, na inshaallah katika hizi pesa za India na hizi *two billion* basi matatizo ya maji yatakuwa yameondoka. Lakini pia kama binadamu tukifikiria kwamba suala la maji ni suala nyeti ni suala ambalo lina thawabu kubwa kwa Mwenyezi Mungu na kila mtu anaihitaji thawabu ile. Kwa hivyo, mimi naomba bado kwa pamoja tushirikiane kuhakikisha kwamba suala hili linaendelea.

Mhe. Spika, lakini nimefurahi sana leo kwamba wachangiaji wengi waliosimama naomba niwashukuru sana kwa kuona umuhimu wa kuwepo vianzio vya maji salama, kwamba maeneo yale tuyatunze na wale watu waliovamia katika maeneo yale tuwachukulie hatua ipasavyo. Naomba niwashukuru Wajumbe na hili tutalifanyia kazi ili tuweze kugharamia ipasavyo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba nimalizie nimekwenda haraka sana, naomba niendelee kuwapongeza tena Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati pamoja na Wajumbe wote waliochangia kwenye taarifa hii. Naahidi Mhe. Spika, nitaendelea kufuatilia, kusimamia changamoto zote zilizotolewa michango na ushauri kwa kuzifanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, kabla sijaunga mkono hoja nilikuwa naomba niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi kutoka Pemba ambao majimbo yao yana matatizo kwa njia moja au nyengine ambayo yanahusu wizara yangu nitakuwa Pemba kuanzia tarehe 6 mpaka tarehe 10 ya mwezi huu, naomba tuungane, tushirikiane ili kwa pamoja tuweze kuzikabili changamoto hizi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Kamati kwa asilimia zote. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri. Naomba nimwite sasa Mheshimiwa Mtoa hoja Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma ili uje uhitimishe hoja yako.

Mheshimiwa kwa sababu ya muda nadhani unahitaji kama dakika tano tu, huhitaji dakika nyingi. Endelea Mheshimiwa. (*Makofi*).

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi naomba kukushukuru kunipa tena nafasi hii ya kuja kufanya majumuisho ya ripoti yetu hii ya Kamati, lakini vile vile nataka niwapongeze sana Wajumbe kwa jinsi walivyochangia ripoti hii na namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba ripoti yetu hii imeungwa mkono na Wajumbe wote kuanzia Wajumbe wa kawaida mpaka Mawaziri.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sasa kwa kuwa Kanuni zetu zinatwambia kwamba ripoti hizi Mawaziri wanazileta kwa maandishi katika kikao cha Septemba, mimi nitaomba tu ili niweke *hansard* sawa niweze kuwataja Waheshimiwa waliochangia ripoti hii na wengi wao wamezungumzia zaidi majukumu ya wizara lakini sio ile ripoti ya Kamati yenyewe kwa sababu ripoti wameiunga mkono. Isipokuwa nitatoa ufafanuzi kwa baadhi ya masuala mawili, matatu.

Kwanza nataka niwatambue Wajumbe ambao waliochangia. Mhe. Spika, Wajumbe wote walikuwa ni 52, nadhani Kamati yetu imepata bahati kubwa sana kwa sababu wizara zetu zote zinahudumia mahitaji ya wananchi siku zote.(Makofi).

Nitaomba nianze kuwataja Wajumbe hao kwa ruhusa yako, lakini nadhani nikiwataja wote itakuwa hizo dakika sijui kama zitakuwa zimebakia. Lakini nitaomba kwa haraka haraka nianze na Mwenyekiti wa Kamati ambaye ndio mimi Hamza Hassan Juma.

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
4. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
5. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali
6. Mhe. Asha Abdalla Mussa
7. Mhe. Mussa Foum Mussa
8. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
9. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
10. Mhe. Omar Said Abeid
11. Mhe. Suleima Sarahan Said
12. Mhe. Hidaya Ali Makame
13. Mhe. Simai Mohammed Said
14. Mhe. Mwantatu Khamis Mbaraka
15. Mhe. Rashid Makame Shamsi
16. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
17. Mhe. Suleiman Makame Ame
18. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
19. Mhe. Nassor Salim Ali
20. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
21. Mhe. Said Omar Said
22. Mhe. Mussa Ali Mussa
23. Mhe. Abdalla Ali Kombo
24. Mhe. Maryam Thani Juma
25. Mhe. Mohammed Said Mohammed
26. Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
27. Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji
28. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira

Pia kuna Wajumbe ambao Mhe. Spika, waliochangia kwa maandishi naomba niwatambue nao.

1. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
2. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
3. Mhe. Miraji Khamis Mussa
4. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma
5. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
6. Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

7. Mhe. Hamida Abdalla Issa
8. Mhe. Ali Salum Haji
9. Mhe. Ali Juma Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
10. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha
11. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
12. Mhe. Mgeni Hassan Juma
13. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
14. Mhe. Ame Ali Haji
15. Mhe. Khadija Omar Kibano
16. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
17. Mhe. Ussi Yahya Haji
18. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
19. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
20. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
21. Mhe. Shehe Hamad Mattar
22. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
23. Mhe. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
24. Mhe. Mussa Ali Mussa
25. Mhe. Ali Bakar Khamis
26. Mhe. Zaina Abdalla Salum

Mhe. Spika, kama kuna baadhi ya Wajumbe ambao pengine sikuwataja nitaomba basi vile vile na wao waingie katika *hansard* pengine labda wataleta majina yao baadae kidogo.

Mhe. Spika, kuna ufafanuzi kidogo ambao nilitaka niutoe nakubaliana na marekebisho katika ripoti yetu ambayo aliyatoa Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Simai Mohammed Said katika ukurasa wa 11 kweli pale kuna *typing error* tuliandika ile tozo inayotozwa mafuta kutoka Dar es Salaam ambayo ni tozo ya Dola 10 sio kwa lita, Dola 10 kwa kila tani ambayo inayoletwa hapa Zanzibar. Kwa hivyo, naomba katika *hansard* na katika kitabu chetu iweze kufanyiwa marekebisho.

Lakini vile vile Mhe. Rashid alitaka ufafanuzi huyu ambaye aliyepewa katika eneo la kule Nungwi alitaka tumtaje jina lake, mimi nadhani

**Mhe. Spika:** Mhe. Mwenyekiti nadhani ungehoji tu.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Niwahoji tu eeh.

**Mhe. Spika:** Eeh.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Basi mimi nafikiri labda nitamtaja tu huyu anaitwa Bi. Fatma kwa hiyo nafikiri Mhe. Waziri taarifa yetu ameshapelekewa na Mhe. Mohammed Said Mohammed ameitilia nguvu na pia kuna nguvu na pia kuna nguvu ya barua ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aliyemuagiza Waziri aweze kulitekeleza hilo nadhani Mhe. Waziri ataweza kulifanyia kazi. Lakini sasa Mheshimiwa kutokana na muda kwa sababu kuna Wajumbe karibu wanane walitaka ufafanuzi, lakini kiti chako nafikiri…

**Mhe. Spika:** Naomba utoe hoja tu Mheshimiwa, maana yake…

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Kiti chako kwa kuwa kimeniruhusu naomba kutoa hoja Mhe. Spika nawaomba Wajumbe wote waipokee ripoti hii na waunge mkono ili kuweza kutekeleza majukumu yetu.

Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kwa sababu wakati hatunao tena hoja imetolewa, naomba sasa niwahoji wale wote wanaokubaliana na ripoti ya mheshimiwa wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu ya muda mpaka hapa tutakuwa tumefikia mwisho wa shughuli zetu lakini ningependa kukumbusha jambo dogo tu, kumekuwa na kawaida mara nyingi mtu anapochangia mkipiga hayo mabao kwa sababu ya hili tatizo la *echo* huwa hatusikii. Kwa hivyo, mngepunguza kidogo hili suala la kupiga mabao wakati mtu anachangia.

Baada ya hayo machache napenda niahirishe shughuli za Baraza mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 1:44 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 02/03/2017 saa 3:00 asubuhi)*